# BAROMETA YA SIKILIZA!

## Mwongozo Wa Utekelezaji



Kupima jinsiwanawakena wasicha na walioa thiri wanamajanga na wanawake wanao fanya kazi katika dharura wanafikia uwezo Wao Bila unyanyasaji na ukosefuwa usawa

# Shukrani

**Barometa ya Sikiliza! ilibuniwa kwa misingi ya Nadharia ya Mabadiliko (tazama kurasa za 6) iliyobuniwa na mashirika ya kifeministi na mitandao ya haki za wanawake kutoka Kusini mwa Dunia na Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (IRC). Ni sehemu moja ya mradi wa Sikiliza! unaofadhiliwa na Wizara ya Marekani ya Mashauri ya Kigeni, unaolenga kukuza sauti na nguvu za wanawake na wasichana wakimbizi na wanawake wanaohudumu katika dharura, lengo lake likiwa kuchochea mageuzi ya kitaasisi, hatua za mashirika kwa ushirikiano, na kuongeza rasilimali za kupunguza unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono katika muktadha wa kibinadamu.**

Barometa ya Sikiliza! ilibuniwa na mashirika ya VOICE na IRC kwa kuzingatia mwongozo na weledi wa Baraza la Ushauri la Sikiliza!, la Mashirika ya kifeministi kutoka Kusini mwa Dunia na mitandao ya haki za wanawake. Baraza la Washauri,[1] lililoanzishwa ili kubuni Barometa, lilichangia pakubwa wakati wa kusanifiwa kwa Barometa, kwa kutoa ushauri. Mashirika matatu ya haki za wanawake na timu tatu za miradi ya nchi ya Ulinzi na Uwezeshaji wa Wanawake nchini Nigeria, Lebanon na Uganda, na shirika la VOICE, walifanyia Barometa majaribio na wakashirikiana katika kuirekebisha na kuikamilisha.

Mashirika ya Akkar Network for Development, Gender Equality Peace and Development Centre na Women's International Peace Center, VOICE na timu ya IRC ya WPE, yangependa kuwashukuru wanawake na wasichana kutoka Nigeria, Lebanon na Uganda kwa kushiriki hali zao na pia wafanyakazi waliojitolea kutoa usaidizi wa kibinadamu katika kila mojawapo ya nchi.

Sehemu ya Barometa ya Sikiliza! ilifadhiliwa na ruzuku kutoka Wizara ya Marekani ya Mashauri ya Kigeni. Maoni, matokeo na mahitimisho yaliyoandikwa hapa ni ya walioandika wala sio ya Wizara ya Marekani ya Mashauri ya Kigeni. Shirika la IRC linashukuru Ofisi ya Watu, Wakimbizi na Uhamiaji - Wizara ya Marekani ya Mashauri ya Kigeni kwa kufadhili Barometa ya Sikiliza! tangu mwaka wa 2018, kama tunu kutoka Serikali ya Marekani.

1 Wanachama wa Baraza la Washauri wanaweza kupatikana hapa: https://gbvresponders.org/womens-movement-building/listen-up/

# Baraza la Ushauri la Mradi wa Sikiliza

# Yaliyomo

**Shukrani** 2

**Tunakuletea Barometa ya Sikiliza!** 4

**Je, Barometa ni nini na madhumuni yake ni nini?** 4
Mwongozo wa Viwango vya Chini kabisa vya Barometa 5
Nadharia ya Mabadiliko 6

**Je, Barometa inalenga nani?** 7

**Barometa itumike wakati gani?** 7

**Je, tunapimaje usaidizi wa kibinadamu kwa kutumia Barometa?** 8
Matokeo Manne ya Nadharia ya Mabadiliko na Maeneo ya Kutathmini ya barometa 8

**Ufafanuzi** 10
Unyanyasaji wa kingono kazini 10
Udhalilishaji na dhuluma za kingono 10
Ukatili wa kijinsia 10

**Yaliyomo kwenye zana** 11
Muundo wa yaliyomo kwenye folda 11

**Sehemu ya 1. Mipango na Maandalizi** 15

**Kuandaa timu ya Barometa** 16
Viwango vya chini kabisa kwa timu ya Barometa kulingana na mbinu bora 16
Muundo wa timu ya ukusanyaji data ya barometa 16
Ni washiriki wa timu gani unahitaji katika shughuli ipi ya ukusanyaji wa data? 19

**Kupanga na kusanifu ukusanyaji wa data** 21
Ushirikishaji wa wadau 21
Kupanga ratiba 23
Kupanga bajeti 23

**Kuchagua maeneo yako na washiriki** 25
Mwongozo wa hatua kwa hatua: Hatua 6 za kukusaidia kuchagua maeneo yako na vikundi vya washiriki 25

**Kujiandaa kwa ukusanyaji wa data** 28
Hati muhimu za kukusanya na kukagua 28
Kuelewa njia za rufaa na mawasiliano za UWAKI 28
Mkutano wa siku 2 za mwanzo wa timu ya kukusanya data 29

**Mfano wa Ajenda ya Mkutano wa siku 2 wa Kujiandaa Kukusanya Data** 30

**Timu ya Barometa ya Sikiliza!** 37
Hadidu za Rejea (Inafaa kukamilishwa kila wakati kabla ya Utekelezaji) 37

**Tathmini ya Usalama ya Haraka** **40**

**Ratiba ya wiki 2 ya Utekelezaji wa Barometa ya Sikiliza! (mfano)** **43**

**Sehemu ya 2. Utekelezaji** **47**

**Mazingatio ya kimaadili na usalama kwa ukusanyaji wa data nyeti** **48**

Usiri na Faragha 48

Ulinzi wa data 48

Utoaji idhini baada ya Kufahamishwa 49

Hatari, faida na mazingatio ya usalama 50

**Muhtasari wa zana za kukusanya data na jinsi ya kuzitumia** **51**

Zana za Kukusanya Data 51

Majadiliano ya Kikundi Lengwa 51

Mahojiano ya watoa taarifa muhimu 52

Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia 53

Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi 54

Maoni ya Washiriki 54

Kuendesha Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Dokezo la Mwongozo 55

Mwongozo kwa Wanakili kumbukumbu 56

Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Dokezo la Mwongozo 57

Mwongozo wa Hatua kwa Hatua wa Kufungua Akaunti na Kutumia KoBo 59

**Sehemu ya 3. Uchambuzi wa Data** **61**

**Muhtasari: Maeneo manne ya matokeo ambayo Barometa hupima** 63

**Kutoka kurekodi data hadi uchanganuzi wa data: hatua 3** 64

Hatua ya 1: Kurekodi na kuchanganua data ya kiasi - tafiti za kuchunguza kwa kuangalia na mtazamo wa wafanyakazi 63

Hatua ya 2: Kukagua na kuchambua data kulingana na mada kwa misingi ya ubora - majadiliano ya vikundi na mahojiano ya watoa taarifa muhimu 67

Hatua ya 3: Uchanganuzi wa matokeo yako ya jumla ya Barometa 68

**Maagizo ya Hatua kwa Hatua ya Kutumia *Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data*(Excel)** **69**

**Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Jinsi ya Kuweka Alama** **72**

**Dokezo la Mwongozo wa Uchanganuzi wa Data ya Matini la Majadiliano ya Kikundi na Mahojiano ya Watoa Taarifa muhimu** **79**

**Sehemu ya 4. Utetezi na Usambazaji** **83**

**Muhtasari: Kutoa alama** **84**

**Kuanzia Kuweka Alama hadi Utetezi: Hatua 4** **86**

Hatua ya 1: Kuthibitisha Alama 86

Hatua ya 2: Kuandaa Mapendekezo ya Utetezi 87

Hatua ya 3: Kuandika Ripoti 88

Hatua ya 4: Kufanya Mabadiliko 89

**Viambatisho** 93

**Zana za Kukusanya Data** 94

Mwongozo wa Majadiliano ya Kikundi ya Washichana 95

Mwongozo wa Majadiliano ya Kikundi cha Wanawake 101

Kiolezo cha Kumbukumbu za Majadiliano ya Kikundi 108

Zana ya Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu 113

Kiolezo cha majadiliano ya watoa taarifa muhimu 116

Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia 119

Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi 128

Zana ya Washiriki ya Kutoa Maoni 137

**Karatasi ya Taarifa kwa Mshiriki wa Barometa na Idhini** 140

Karatasi ya Taarifa kwa Mshiriki wa Barometa ya Sikiliza! 140

Fomu ya Utoaji Idhini ya Mshiriki katika kipimo cha Barometa cha Sikiliza! 143

Barometer inaweza kutumika kama chombo cha utetezi vikundi vya wanawake, mashirika na mitandao, na GBV nyinginezo wahusika, kuwawajibisha wale kwa majibu ya kibinadamu kuwajibika kwa wanawake na wasichana.



Picha na A Oberstadt, IRC

# Tunakuletea Barometa ya Sikiliza!

**Jumuiya ya misaada ya kibinadamu inawaangusha wanawake na wasichana. Misaada ya kibinadamu haibuniwi au kuwasilishwa kwa kuwazingatia wanawake na wasichana au usalama wao. Kadhalika wanawake na wasichana hawashirikishwi vya kutosha katika kubuni au ufuatiliaji wa misaada. Mashirika, mitandao na makundi ya wanawake kutoka kwenye jumuiya za kitaifa na jamii zilizohamishwa makwao mara nyingi hazijumuishwi katika kutoa misaada ya kibinadamu. Uongozi wa wanawake waliohamishwa makwao pamoja na vikundi vya jamii vinapuuzwa. Wanaoshughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia pamoja na washirika wao—wakiwemo wanaofanya kazi katika kuzuia udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono—katika kutoa misaada ya kibinadamu, wanaoteta kuhusu matukio ya wanawake na wasichana wanaonyanyaswa pamoja na vikwazo wanavyopitia ili kupata misaada ya kibinadamu kwa usalama na usawa mara nyingi hupuuzwa au kunyamazishwa.[2]**

## Je, Barometa ni nini na madhumuni yake ni nini?

Barometa ya **Sikiliza!** ni zana ya kupanga na kutathmini inayochunguza hali walizopitia wanawake na wasichana ili kubaini kama mazingira ya misaada ya kibinadamu kwa dharura yanaweza kuzuia, kupunguza na kukabiliana na Ukatili wa Kijinsia, ikiwa ni pamoja na udhalilishaji na dhuluma za kingono, pamoja na unyanyasaji wa kingono. Kipimo cha Barometa kimeundwa ili kubuni tathmini ya haraka ya uwezo na udhaifu wa utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na wale wanaofanya kazi katika dharura za kibinadamu na wale walio katika eneo chanzo ambako msaada wa dharura unapelekwa, kwa madhumuni ya kuunda mapendekezo ya kutumika katika utetezi. Kipimo hiki hutumia zana na miongozo minne kukusanya na kukamilisha data: Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FGD); Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII); Orodha ya Mambo Kuchunguza kwa Kuangalia; na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi.

Kwa umahususi, Barometa inaweza kutumika kama zana ya utetezi kwa vikundi, mashirika na mitandao ya wanawake pamoja na wahusika wengine wa kukabili ukatili wa kijinsia, ili kuwawajibisha wale wanaohusika katika utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa wanawake na wasichana.

Kipimo cha Barometa kiliundwa na kugeuzwa na wataalamu wanaoshughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia, usawa wa kijinsia, dharura ya udhalilishaji, unyanyasaji na dhuluma za kingono, kwa kuzingatia Nadharia ya Mabadiliko iliyobuniwa na wanaharakati wa haki za wanawake walio katika maeneo ya Kusini mwa Dunia kwa ushirikiano na Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (IRC). **Barometa imegawanywa katika sehemu nne, kila moja ikiwa inaoana na matokeo tofauti yanayotarajiwa ya Nadharia ya Mabadiliko na inajumuisha Vipimo 21 vya Kielezo.** Matokeo yananuiwa kuwasaidia watumiaji watathmini wigo kamili wa misaada ya kibinadamu kulingana na maono ya jumla: kwamba wanawake na wasichana walioathiriwa na majanga na wanawake wanaofanya kazi katika dharura wanaweza kufikia uwezo wao, bila unyanyasaji na ukosefu wa usawa.[3]

2 Oxfam Canada, "Mtazamo wa ujanibishaji kifeministi: Jinsi Kanada inavyoweza kuunga mkono uongozi wa wahusikai wa haki za wanawake katika hatua za kibinadamu," (2018): https://www.oxfam.ca/wp-content/uploads/2018/06/a-feminist-approach-to-localization.pdf.

3 Barometa ya Nadharia ya Mabadiliko inaweza kupatikana hapa: https://gbvresponders.org/wp-content/uploads/2021/03/Listen-Up-Theory-of-Change-2019.pdf

## Mwongozo wa Viwango vya Chini kabisa vya Barometa

Viwango vya chini kabisa vya uzuiaji na kukabiliana na UWAKI, unyanyasaji wa kingono, na udhalilishaji na dhuluma za kingono vinarejelewa katika hati zote za mwongozo wa Barometa. Viwango vya chini kabisa vinawakilisha mbinu bora zifuatazo za kimataifa zilizoanzishwa na mashirika anuai:

- Interagency GBV Minimum Standards[4]
- Inter-Agency Standing Committee (IASC) GBV Guidelines[5]
- PSEA Minimum Operating Standards[6]
- Best Practice Guide Inter-Agency Community Based Complaints Mechanisms[7]
- GBV Accountability Framework[8]

4 https://gbvaor.net/sites/default/files/2019-11/19-200%20Minimun%20Standards%20Report%20ENGLISH-Nov%201.FINAL_.pdf
5 https://gbvguidelines.org/en/
6 https://interagencystandingcommittee.org/accountability-affected-populations-including-protection-sexual-exploitation-and-abuse/content-1
7 https://interagencystandingcommittee.org/accountability-affected-populations-including-protection-sexual-exploitation-and-abuse/documents-50
8 https://www.calltoactiongbv.com/call-to-action-in-the-field

# Nadharia ya Mabadiliko

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MAONO | Wanawake na wasichana walioathiriwa na majanga na wanawake wanaofanya kazi katika huduma za dharura wanaweza kufikia uwezo wao, bila unyanyasaji na ukosefu wa usawa. | | | |
| MATOKEO | Wanawake na wasichana waamini na kupata huduma za usaidizi salama, kwa siri na kwa uwajibikaji wanapopatwa na UWAKI, ikiwa ni pamoja na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. | Wanawake na wasichana wana ufikiaji na udhibiti sawa wa huduma na rasilimali za kibinadamu. | Wahudumu wa kibinadamu wanatumia mamlaka vizuri na wanaheshimu na kuthamini wanawake na wasichana. | |
| | | | Mfumo wa kibinadamu unapatia kipaumbele, nyenzo na unathamini juhudi za kushughulikia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono. | Mashirika ya kibinadamu huwajibisha wafanyakazi ili kushughulikia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono. |
| NJIA ZA MABADILIKO | Huduma za kutoa usaidizi[9] na njia za kuripoti na kupata rufaa ni salama, zinafikika na zinafaa kwa wanawake na wasichana[10]. | Huduma na bidhaa za kibinadamu zinahusisha na kuongozwa na wanawake na wasichana anuai. | Kuna sera za kuzuia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono na sera hizo zinatekelezwa ipasavyo katika viwango vyote vya mfumo wa kibinadamu. | Uongozi na wafanyakazi wa kibinadamu wanathamini wale wanaokemea na kuripoti unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono. |
| | Wanawake na wasichana wawe na nafasi salama na mitandao ya kijamii. | Huduma na bidhaa za kibinadamu zinalenga ipasavyo mahitaji ya wanawake na wasichana anuai. | Wakala na uongozi wa kibinadamu unathamini upigaji ripoti wa kweli na ulio wazi, bila athari hasi kwa anayeripoti au manusura. | Wahudumu wa kibinadamu wanatambua haki na mamlaka yao na wanayatumia kuendeleza usawa na kupunguza vurugu. |
| | Watoa huduma[11] wawe na ustadi, ujuzi na ari ya kuwasaidia wanawake na wasichana waliopatwa na UWAKI, ikiwa ni pamoja na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. | Hatua za kibinadamu hujumuisha na kutoa rasilimali ipasavyo kwa asasi za kiraia zinazoongozwa na wanawake na wahusika wa haki za wanawake wa eneo ili kuendeleza uwezeshaji na ulinzi wa wanawake na wasichana. | Wakala wa kibinadamu hukuza mafunzo ya namna ya kushughulikia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono kupitia kushiriki mbinu bora na mambo ambayo hayakufaulu. | Mashirika hukuza utamaduni wa heshima, ustawi na huruma kwa wafanyakazi wa kike wanaopitia unyanyasaji na vurugu. |
| | Jamii, familia na wafanyakazi wenza waamini na waunge mkono wanawake na wasichana kufichua UWAKI, ikiwa ni pamoja na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. | Juhudi za kushughulikia UWAKI, ikiwemo unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono, zinawajibikia wanawake, wasichana na wafanyakazi wa kike katika dharura. | Wakala na viongozi wa kibinadamu wanawawajibisha wanaodhulumu na hawawapatii kazi tena au kuwaruhusu kupata nafasi za kufanya maamuzi. | Wanawake na wanaume katika nafasi za uongozi ni kielelezo na wanaunga mkono juhudi za kushughulikia UWAKI, ikiwemo, unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono. |

9 Huduma za usaidizi zinajumuisha huduma za kiwango cha chini za kukabiliana na UWAKI kama vile mahitaji ya kiafya, kisaikolojia, kisheria na usalama wa wanawake na wasichana.

10 Huduma hutolewa kwa kuzingatia kanuni elekezi za GBV: usiri, kutobaguliwa, utu na usalama.

11 Afya, msaada wa kisaikolojia, watoa huduma za kisheria na usalama.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake wamewakilishwa kwa usawa na wanashiriki ipasavyo katika vikundo vya wahamiaji vinavyofanya maamuzi. | Uongozi wa kibinadamu[12] unahitaji na kuzawadi hatua zenye uwazi juu ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono. | Wahusika wote wa kibinadamu wanajua kwamba lazima wachukue hatua ili kuzuia na kushughulikia UWAKI, ikiwemo unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono. |
| | | Vikundi vya wanawake vinasaidia wanawake na wasichana anuai na vinaangazia mahitaji yao na mambo yanayowapatia wasiwasi. | Wanawake wanashikilia nafasi za uongozi na ufanyaji maamuzi katika mfumo wa kibinadamu. | |
| MASHARTI | Masuala ya wanawake na wasichana yathaminiwe na kupewa kipaumbele katika utoaji wa misaada ya kibinadamu. | | | |
| | Mashirika ya kibinadamu na uongozi utambue uhusiano kati ya ukosefu wa usawa wa kijinsia na ukatili wa kijinsia unaofanywa na wanaume, ikiwa ni pamoja na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono wa wanawake na wasichana. | | | |
| | Wahusika wa misaada ya kibinadamu kwa pamoja wapime athari za vitendo vya kushughulikia UWAKI, ikijumuisha dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. | | | |

## Je, Barometa inalenga nani?

Barometa ya **Sikiliza!** ni zana ya tathmini na utetezi ya haraka ambayo imeundwa ili kutumiwa na wahusika, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake inayofanya kazi ndani na kwa ushirikiano na jumuiya za wanawake. Panapowezekana, inapendekezwa sana kwamba wahusika, vikundi, mashirika au mitandao ya haki za wanawake inayotaka kutekeleza Barometa itambue na kushirikiana na shirika la kibinadamu linaloshughulikia UWAKI (liwe la kitaifa au kimataifa) linaloshughulikia dharura za kibinadamu katika kipindi chote cha utekelezaji wa Barometa. Majukumu, wajibu na shughuli zilizopo katika kutekeleza Barometa zimeundwa ili kushirikiwa miongoni mwa mashirika yanayoitekeleza. Muundo wa utekelezaji uliotolewa ni wa kiwango cha chini kinachopendekezwa na unaweza kuongezwa kwa urahisi kupitia ushirikiano mkubwa wa timu na rasilimali kama inavyotakiwa na dharura yenyewe.

Shirika la kibinadamu linaloshughulikia UWAKI (liwe la kitaifa au kimataifa) likiamua kutekeleza Barometa, basi linapaswa kutafuta ushirika sawa wa makundi, mashirika au mitandao ya haki za wanawake inayofanya kazi ndani na pamoja na jamii ambako mashirika hayo yapo. Kufanya hivyo kutasaidia kuhakikisha uongozi muhimu wa pamoja wa wahusika wa haki za wanawake kutoka katika jamii na mazingira ya dharura, na kwamba wanawake na wasichana wanaendelea kuwa muhimu katika mchakato ambao umeundwa kwa ajili yao na pamoja nao. Ni muhimu kuchanganya ujuzi wa wahusika, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake, na ule wa wahusika walio kwenye mfumo wa misaada ya kibinadamu.

Kupitia ushirikiano huu, wahusika, makundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake inaweza kuchangia mitazamo, uzoefu na utaalamu muhimu na wa kipekee kuhusu haki za wanawake, uanaharakati na Ukatili wa Kijinsia/ dhuluma dhidi ya wanawake na wasichana, huku pia ikitumia utaalamu wa vuguvugu pana la haki za wanawake kuchangia katika mfumo wa misaada ya kibinadamu. Wahusika wakuu wa misaada ya kibinadamu dhidi ya UWAKI wanaweza kuleta ujuzi wao kuhusu namna ya kushughulikia ukatili wa kijinsia katika hali za dharura na kusaidia katika ufikiaji wa mfumo wa misaada ya kibinadamu, taratibu za uratibu, huduma na rufaa za kupata huduma za kukabiliana na UWAKI.

Kipimo hiki pia kinaweza kutumiwa na wahusika, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake inayoweza kufikia mazingira ya misaada ya kibinadamu na inataka kutekeleza Barometa kwa kujitegemea. Kwa hivyo, Barometa inatoa mfumo wa msingi wa utekelezaji ambao unawazingatia wale ambao huenda wana rasilimali, muda na uwezo mdogo wa wafanyakazi.

12 Uongozi wa kibinadamu unajumuisha waratibu wa kibinadamu, wafadhili na uongozi wa mashirika yasiyo ya kiserikali na yale yaliyoungana.

# Barometa itumike wakati gani?

Barometa ni zana ya utetezi ambayo inaweza kutumiwa na vikundi, mashirika na vuguvugu za wanawake—ama kwa kujitegemea au kwa ushirikiano na mashirika ya kibinadamu yanayoshughulikia ukatili wa kijinsia—wakati wowote ambapo wanawake na wasichana na washirika walio kwenye mfumo wa misaada ya kibinadamu wana wasiwasi kwamba hatua za misaada ya kibinadamu zinadhuru wanawake na wasichana, na/au hakuna hatua za kutosha za kibinadamu zinachukuliwa ili kuhakikisha ufikiaji sawa na salama wa misaada ya kibinadamu kwa wanawake na wasichana.

Inaweza kutumika mara moja au mara kwa mara kunakili kimaadili hali za maisha ya wanawake na wasichana wakati wa utoaji usaidizi wa kibinadamu kwa lengo la kutetea kwa uongozi wa kibinadamu, wafadhili na wahusika wa misaada ya kibinadamu.

# Je, tunapimaje usaidizi wa kibinadamu kwa kutumia Barometa?

Barometa ina **zana na miongozo minne ya kukusanya data**[13] ili kupata taarifa zinazohitajika ili kukadiria utoaji wa misaada ya kibinadamu:

- **Mwongozo wa Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD):** Kuwahusisha wanawake na wasichana kutoka jamii zilizoathiriwa na dharura ya kibinadamu.
- **Mwongozo Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII):** Kufanywa na wahusika, makundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake ili kuelewa kazi zao na uzoefu wa kukabiliana na dharura, na vikwazo wanavyokabiliana navyo katika kufikia rasilimali zilizopo pamoja na taratibu za uratibu, wadau na watoa maamuzi.
- **Orodha ya Mambo Kuchunguza kwa Kuangalia:** Imeundwa ili kuangalia hati zilizopo za mawasiliano yanayohusiana na UWAKI na uzuiaji wa dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono; pamoja na mazingira na utoaji wa huduma ya usaidizi (k.m., kambi, mazingira yasiyo rasmi, mijini).
- **Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi:** Kufanywa miongoni mwa wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu ili kuelewa mitazamo yao kuhusu mfumo wa kibinadamu na hatua zinazochukuliwa na shirika ili kuzuia na kukabiliana na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono.

13 AngaliaSehemu ya 2: Utekelezaji.

**Barometa inatathmini maeneo manne ya usaidizi wa kibinadamu** ambayo yanaoana na matokeo manne ya Nadharia ya Mabadiliko ya Utafiti wa Sikiliza!:

## Matokeo Manne ya Nadharia ya Mabadiliko na Maeneo ya Kutathmini ya barometa

1. Wanawake na wasichana wa naaminina kufikia huduma za usaidizia mbazonisalama, zina usirina uwajibikajiwanapopitia UWAKI, ikiwemo unyanyasaji, udhalilisha jina dhuluma za kingono.

2. Wanawake na wasichana kutoka jamiizi lizo athiri wa wananafasi sawa za kufikia na kudhibiti hudumananyenzo za kibinadamu.

3. Wahudumu wa kibinadamu hutumia mamlakavizurina huheshi munakuthamini wanawake nawasichana najamiizilizo athiriwa.

4. Mashirika ya kibinadamu huwajibisha wafanyakazii likushughulikia unyanyasaji, udhalilisha jinadhuluma za kingono.

Maeneo haya manne ya matokeo yanashughulikia wigo kamili wa utoaji usaidizi wa kibinadamu unaounga mkono maono makubwa: **wanawake na wasichana walioathiriwa na majanga na wanawake wanaofanya kazi katika huduma za dharura wanaweza kufikia uwezo wao, bila unyanyasaji na ukosefu wa usawa**.

**Barometa hutumia "mfumo wa taa za barabarani"** (Rangi Nyekundu, ya Chungwa, ya Manjano na ya Kijani) ili kupima hali ya utoaji misaada ya kibinadamu kwa UWAKI na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono katika maeneo hayo manne. Pia hutumia mchango wa data ya fafanuzi iliyokusanywa kama sehemu ya Barometa ili kuongeza mitazamo na maelezo kwenye alama hizo.

Katika kila mojawapo ya maeneo haya manne, kuna vigezo tofauti ambavyo vinatathminiwa kimoja kimoja. Kila kigezo kina msururu wa vipengele ambavyo vitapata alama kutoka 1-4 (Nyekundu hadi Kijani):

**Nyekundu** | **Chungwa = alama** | **Manjano = alama** | **Kijani = alama 4**

Kutoka kwenye alama hizi, Barometa itatoa majibu mawili: ukadiriaji wa binafsi wa kila mojawapo ya maeneo hayo manne ya matokeo kutoka nyekundu hadi kijani; na, kujumlisha alama kutoka maeneo yote manne, alama ya jumla ya usaidizi wa kibinadamu unaotathminiwa.

| | |
|---|---|
| 91-100% | Mafaniki omakubwakati kavigezo vyote; inawakilishambinu bora nauwezothabiti wa mazingiraya usaidi zi wakibinada muwakuzuia naku shughulikia UWAKI, ikiwemounyanyasaji, udhalilishajinadhuluma za kingono; inazidiviwangovya chini |
| 67-90% | Mafanikio ya nayoridhisha katikavigezo vingi; inawakilisha uwezo wakuzuiana kushughulikia UWAKI, ikiwemo unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono; inazidiviwangov ya chini |
| 51-66% | Mafaniki omachachekati ka vigezo vingi; inawakilisha uwezo kiasiwakuzuia na kushughulikia UWAKI, ikiwemounyanyasaji, udhalilishajinadhuluma za kingono; juhudizaidizinahitajikailikufikiaviwangov ya chini |
| 0-50% | Mafaniki oyasiyotosha kwenyevigezo vyote; mazingira ya usaidiziwakibina damuhayazuii nahayashughulikii UWAKI, ikiwemounyanyasaji, udhalilishajinadhuluma za kingono; mipango bayananayakimkakatiinahitajikailikuboresha sera namazoea; viwangovya chini havijafikiwa |

Utaratibu huu utawapa watumiaji wa Barometa data pana na ya kina ambayo wanaweza kutumia kuandaa mapendekezo na mikakati ya utetezi, kulingana na mahitaji na vipaumbele vya miktadha yao ya kibinadamu.

## Muhtasari:

Taarifa kuhusukilakige zozina kusanywa kwa kutumiazana 4 za kukusanya data →

Kila kigezo kinape waalamakatiya 1 na 4 (Nyekunduha di Kijani) →

Alama zavigezo za maeneo 4 ya kutathminihujumli shwa; kilaeneo hupewa alama ya jumla →

Kisha alama zajumla za maeneo hujumlishwaili kupata alama ya jumla ya usaidiziwa kibinadamu

- *Kwa maelezo, angalia Sehemu ya 2: Utekelezaji na Sehemu ya 3: Uchambuzi wa Data.*

# ufafanuzi

## Unyanyasaji wa kingono kazini

Neno "unyanyasaji wa kingono" linaeleweka kuwa ni hali inayotokea ndani ya mashirika kutoka kwa mfanyakazi mmoja hadi mwingine. Unyanyasaji wa kingono unajumuisha aina yoyote ya uvamizi wa kingono au mtagusano wa kingono bila ridhaa ambayo hayaleti au kujumuisha kujamiiana. Mifano ni pamoja na jaribio la ubakaji, pamoja na kubusu kusikotakikana, kupapasana, au kushika sehemu nyeti na makalio.

*Aina hii ya tukio haijumuishi ubakaji (yaani, pale ambapo mtu ameingiliwa kwa nguvu).*

## udhalilishaji na dhuluma za kingono

Kwa madhumuni ya Barometa, tunatumia ufafanuzi ufuataoo uliowekwa katika Taarifa Rasmi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ya 2003 kuhusu ulinzi dhidi ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono:

"Neno 'udhalilishaji wa kingono' linamaanisha matumizi yoyote halisi au jaribio la kutumia vibaya nafasi ya udhaifu, utofauti wa uwezo, au uaminifu, kwa madhumuni ya ngono, ikijumuisha, lakini si tu, kufaidika kifedha, kijamii au kisiasa kutokana na kumtumia mtu mwingine kingono."[14]

"Neno 'dhuluma za kingono' linamaanisha tukio halisi au tishio la kimwili la kingono, iwe kwa nguvu au katika hali zisizo na usawa au za kulazimishwa."[15]
Katika hati zote za Barometa, tutarejelea udhalilishaji na dhuluma ya kingono ikiwa mada moja.

## Ukatili wa kijinsia

Barometa inafuata ufafanuzi na misimamo iliyoanzishwa na Azimio la Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake:

"Neno 'ukatili dhidi ya wanawake' linamaanisha kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia ambacho kinasababisha, au kinaweza kusababisha madhara ya kimwili, kingono au kisaikolojia au mateso kwa wanawake, ikiwa ni pamoja na vitisho vya vitendo hivyo, kulazimishwa au kunyimwa uhuru kiholela, iwe inatokea hadharani au katika maisha ya faragha."

Tunatambua kwamba "ukatili dhidi ya wanawake ni dhihirisho la uhusiano wa kihistoria wa ukosefu wa usawa wa mamlaka kati ya wanaume na wanawake, hali ambayo ilisababisha wanaume kuwabaguwa na kuwatawala wanawake na kuzuia maendeleo kamili ya wanawake, na kwamba ukatili dhidi ya wanawake ni moja ya mifumo kuu ya kijamii ambayo kwayo wanawake wanalazimishwa kuwa chini wakilinganishwa na wanaume."

Pia tunatambua kwamba "baadhi ya makundi ya wanawake, kama vile wanawake wa jamii za wachache, wanawake wa jamii za asili, wanawake wakimbizi, wanawake wahamiaji, wanawake wanaoishi vijijini au maeneo ya mbali, wanawake maskini, wanawake gerezani au kizuizini, watoto wa kike, wanawake wenye ulemavu, wanawake wazee na wanawake walio katika hali za migogoro yenye silaha, wako katika hatari kubwa ya kutendewa ukatili."[16]

14 TaarifaRasmi ya KatibuMkuuwaUmojawaMataifakuhusuulinzidhidi ya udhalilishajinaunyanyasajiwakingono (ST/SGB/2003/13): https://undocs.org/ST/SGB/2003/13.
15 Kama hapojuu.
16 Tamko la KutokomezaUkatilidhidi ya Wanawake (azimio la 48/104 la 20 Desemba 1993): https://www.un.org/en/genocideprevention/documents/atrocity-crimes/Doc.21_declaration%20elimination%20vaw.pdf

# Kuhusu zana hii

**Zana hii ni Mwongozo wa Utekelezaji wa kipimo cha Barometa cha Sikiliza!, ina mwongozo wa hatua kwa hatua na zana na nyenzo zote unazohitaji ili kutumia na kutekeleza Barometa. Unaweza kupata zana kwa kuipakua katika folda ya .zip inayopatikana hapa: https://gbvresponders.org/womens-movement-building/listen-up/ katika Kiarabu, Kiburma, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza na Kiswahili.**

## Yaliyomo kwenye zana

Zana hii imegawanywa katika makabrasha manne: 1) Mipango na Maandalizi, 2) Utekelezaji, 3) Uchambuzi wa Data, na 4) Utetezi na Usambazaji. Ndani ya kila folda, utapata hati ya mwongozo wa hatua kwa hatua ya sehemu hiyo, pamoja na zana na nyenzo zote unazohitaji kutumia Barometa zikiwa zimepangwa katika Sehemu hiyo na katika sehemu ya Viambatisho.

### Muundo wa yaliyomo kwenye folda

#### **Sehemu ya 1:** Mipango na Maandalizi

#### Hati ya Mwongozo: Mipango na Maandalizi

**Kuandaa timu ya Barometa**

- Viwango vya chini kabisa kwa timu ya Barometa kulingana na mbinu bora
- Muundo wa timu ya ukusanyaji data ya Barometa
- Ni washiriki gani wa timu unaohitaji katika shughuli ipi ya ukusanyaji wa data?

**Kupanga na kusanifu ukusanyaji wa data**

- Ushiriki wa wadau: wahusika wa usaidizi wa kibinadamu
- Kupanga ratiba
- Kupanga bajeti

**Kuchagua maeneo yako na washiriki**

- Mwongozo wa hatua kwa hatua: Hatua 6 za kukusaidia kuchagua maeneo yako na vikundi vya washiriki
  1. Shirikiana na wanawake na wasichana walio balehe
  2. Tambua vikundi vilivyoathiriwa katika dharura yako ya kibinadamu
  3. Tambua maeneo yaliyoathiriwa katika dharura yako ya kibinadamu
  4. Orodhesha maeneo yote yanayofaa kwa utekelezaji wa Barometa
  5. Usalama: Tathmini ya haraka ya hatari kwa maeneo tarajiwa
  6. Chagua maeneo ya utekelezaji wa Barometa

**Kujiandaa kwa ukusanyaji wa data**

- Hati muhimu za kukusanya na kukagua
- Kuelewa njia za rufaa na mawasiliano za UWAKI
- Mkutano wa siku 2 za mwanzo kwa timu ya Barometa ya kukusanya data

**Mkutano wa Kuanza Kukusanya Data**

- Rasimu ya ajenda
- Slaidi za uwasilishaji[17]

**Hadidu za Rejea kwa Timu ya Ukusanyaji Data**

- Hadidu za Rejea

**Tathmini ya Haraka ya Usalama**

- Tathmini ya Haraka ya Usalama

**Ratiba ya Utekelezaji**

- Mfano wa Ratiba ya Utekelezaji wa Wiki 2

## **Sehemu ya 2:** Utekelezaji

### Hati ya Mwongozo: Utekelezaji

- **Mazingatio ya kimaadili na usalama kwa ukusanyaji wa data nyeti**
- **Muhtasari wa zana za kukusanya data na jinsi ya kuzitumia**
- **Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Dokezo la Mwongozo**
- **Mwongozo kwa Wanakili wa Kumbukumbu**
- **Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Dokezo la Mwongozo**
- **Mwongozo wa Hatua kwa Hatua wa KoBo: Kuanzisha uchunguzi wa mtandaoni**

## **Sehemu ya 3:** Uchambuzi wa Data

### Hati ya Mwongozo: Uchambuzi wa Data

- **Muhtasari: Maeneo manne ya matokeo ambayo Barometa hupima**
- **Kuanzia kurekodi data hadi uchanganuzi wa data: hatua 3**
  1. Kurekodi na uchanganuzi wa data ya kiasi (idadi): Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi
  2. Kukagua data ya ubora (simulizi) na kuchanganua matini: Majadiliano ya Vikundi Lengwa na Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu
  3. Uchambuzi wa matokeo yako ya jumla ya Barometa

### Zana za Kurekodi, Kupima na Kuchambua data

- **Hati ya Kurekodi na Kupanga Data (Excel) kwa ajili ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi**
- **Maagizo ya Hatua kwa Hatua ya Kutumia Hati ya Kurekodi na Kupima Data**
- **Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Mwongozo wa Jinsi ya Kupata Alama katika Utafiti Huu**
- **Dokezo la Mwongozo wa Uchambuzi wa Data kutoka kwa Matini (kwa FGD na KII)**

## **Sehemu ya 4:** Utetezi na Usambazaji

### Hati ya Mwongozo: Utetezi na Usambazaji

- **Muhtasari: Jinsi ya kupata alama**
- **Kuanzia Kupata Alama hadi Utetezi: Hatua 4**

  Hatua ya 1: Kuthibitisha Alama

17 SlaidizaWasilisho la MkutanowaSiku 2 zinawezakupatikanakatika https://gbvresponders.org/womens-movement-building/listen-up/

Hatua ya 2: Kuandaa Mapendekezo ya Utetezi

- Kukamilisha Mapendekezo

Hatua ya 3: Kuandika Ripoti

- Kukamilisha Ripoti
- Mfano wa Muhtasari wa Ripoti

Hatua ya 4: Kufanya Mabadiliko

- Kusambaza Ripoti ya Utekelezaji
- Mbinu ya "SMART"
- Mazingatio
- Mpangokazi wa Utetezi

### Zana za Utetezi

## Viambatisho

### Zana za Kukusanya Data

- **Zana ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Wasichana walio balehe**
- **Zana ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Wanawake**
- **Kiolezo cha Kumbukumbu za Majadiliano ya Kikundi Lengwa**
- **Zana ya Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu**
- **Kiolezo cha Kumbukumbu za Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu**
- **Zana ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia**
- **Zana ya Uchunguzi wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Kwa tafiti za ana kwa ana (Hati ya Word)**
- **Zana ya Uchunguzi wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Kwa tafiti za mtandaoni (Hati ya Excel)**[18]
- **Zana ya Maoni ya Watoa Majibu**

### Karatasi ya Taarifa kwa Mshiriki wa Barometa na Idhini

- **Karatasi ya Taarifa kwa Washiriki wa Barometa**
- **Fomu ya Idhini (sampuli)**

18 Zana ya UtafitiwaMitazamo ya WafanyakaziLKwatafitizamtandaoni (Hati ya Excel) inawezakupatikanakatika https://gbvresponders.org/womens-movement-building/listen-up/

# Sehemu ya 1

# Mipango na Maandalizi



Picha na T Jump, IRC

# Kuandaa timu ya Barometa

**Hatua ya kwanza katika mipango na maandalizi ni kuchagua timu yako ya Barometa. Iwe unatekeleza Barometa kwa ushirikiano na shirika jingine au kwa kujitegemea, mwongozo ufuatao unaonyesha mahitaji ya chini kabisa kwa ajili ya timu yako.**

## Viwango vya chini kabisa kwa timu ya Barometa kulingana na mbinu bora

- **Timu ya kukusanya data ya wanawake pekee. Ni salama na inafaa zaidi kwa timu kuwa na wanawake watakaotagusana na wanawake na wasichana katika utekelezaji wa Barometa.** Hii ni pamoja na kuwa na wakusanyaji data wa kike watakaoendesha tafiti za ana kwa ana za mitazamo ya wafanyakazi na vikao vya Majadiliano ya Vikundi Lengwa. Si tu kwamba kufanya hivyo kunatoa safu ya ziada ya usalama kwa wanawake na wasichana, kuna uwezekano mkubwa wa wanawake na wasichana kuzungumza na wanawake wengine juu ya maswala yaliyojadiliwa katika zana husika - hasa wanawake ambao wameteuliwa ipasavyo ili kutekeleza jukumu hilo.
- Lazima kila mwanatimu awe:
  - o Angalau, amepokea **mafunzo kuhusu dhana kuu za ukatili wa kijinsia (UWAKI), kanuni zinazomlenga manusura, na mafunzo kuhusu kuzuia dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono**[19] ; na
  - o Ana **kiasi fulani cha uzoefu** katika kushughulikia masuala ya UWAKI na/au kuzuia dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono.
- Kila mwanatimu lazima awe **amefunzwa kuhusu utekelezaji wa Barometa** (angalia *Mkutano wa Kuanza Kukusanya Data,* na sehemu iliyo hapa chini).
- Kila mwanatimu anapaswa kufahamu njia na taratibu za rufaa ya UWAKI zinazopatikana katika eneo husika-kwa jumuiya na wafanyakazi wa misaada-na awe na nakala, zinapopatikana, za matoleo ya hivi karibuni na taarifa zake. **Ikiwa kuna nambari za simu za dharura, zinafaa kujaribiwa kabla ya shughuli ya kukusanya data.**
- Kila mwanatimu lazima aelewe na atie saini **Kanuni ya Maadili.**

  - *Tafadhali rejelea sera na mwongozo wa ndani ya shirika lako ili kuunda na kukubaliana kuhusu Kanuni ya Maadili ya timu yako ya Barometa. Ikiwa unafanya kazi na mshirika, pia rejelea sera za mshirika huyo ili uweze kuandaa Kanuni ya Maadili kati ya mashirika yenu.*

## Muundo wa timu ya ukusanyaji data ya barometa

Timu yako ya kukusanya data ya Barometa inapaswa kujumuisha **wanawake kutoka ndani ya kikundi chako, shirika lako au mtandao wako**, na **wanawake kutoka shirika unaloshirikiana nalo**, ikiwa lipo. Kwa mashirika yanayoshughulikia UWAKI katika muktadha wa kibinadamu yanayotekeleza Barometa, lazima wanawake kutoka kundi, shirika au mtandao unaoshirikiana nao wawe sehemu ya timu kama viongozi au washirikiane katika kuongoza.

19 Kwarasilimaliza UWAKI, angalia: https://gbvresponders.org/;kwanyenzozakuzuiaudhalilishajinaunyanyasajiwakingono, angalia: http://www.pseataskforce.org/.

Pia unaweza kujumuisha **wanawake waliofunzwa kutoka jamii za wakimbizi zile zinazowahifadhi** ili kuongoza Majadiliano ya Vikundi Lengwa, kukalimani lugha za asili katika Majadiliano ya Vikundi Lengwa ya wanawake na wasichana walioathiriwa na majanga, au kusaidia shughuli za Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia. Ni lazima wafunzwe kuhusu dhana za msingi za UWAKI na kanuni zinazomlenga manusura na wajumuishwe katika mkutano wa kuanza unaohusisha timu yako yote ya Barometa.

Utahitaji **angalau wanawake wanne katika timu yako ya kukusanya data ya Barometa** wakihudumu katika majukumu yafuatayo:




Unaweza kuongeza ukubwa wa timu yako kwa kuongeza Waratibu, Wanakili wa kumbukumbu au Wakalimani zaidi, kulingana na idadi ya wanawake waliopo katika shirika lako au shirika unaloshirikiana nalo.

Utahitaji timu kubwa zaidi ikiwa unataka kufanya zaidi ya shughuli moja ya ukusanyaji wa data kwa wakati mmoja (yaani, ikiwa unataka kufanya Majadiliano mawili ya Vikundi Lengwa kwa wakati mmoja katika sehemu mbili tofauti za kambi, utahitaji angalau Waratibu wawili na wanakili wawili wa kumbukumbu, kuna uwezekano wa kuongeza Mkalimani mmoja au wawili kulingana na mahitaji yako, na angalau Mfanyakazi/Msimamizi/Mtoa huduma mmoja wa masuala ya UWAKI anayeweza kuwa katika shughuli zote mbili).

## Wajibu na majukumu makuu

### KIONGOZI WA TIMU

- Angalau mwanamke mmoja katika timu yako anafaa kuongoza na kuratibu mchakato mzima wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data.
- **Mratibu**: Ikiwa hakuna mwanamke mwingine wa kuratibu, Kiongozi wa Timu anaweza pia kuwa Mratibu. Ni muhimu Mratibu awe na ujuzi na uzoefu unaohitajika katika kuendesha mazungumzo na wanawake na wasichana kuhusu masuala ya UWAKI na/au udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. Ataendesha vikao vya Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FGD), atahudumu kama mhoji wa vipindi vya Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII) na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi, na anaweza kufanya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.

### MNAKILI KUMBUKUMBU

- Mnakili Kumbukumbu ataandika kinachojadiliwa wakati wa vikao vya FGD na KII.
- Mnakili Kumbukumbu pia anaweza kufanya utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia ikiwa ana tajriba ya awali katika kufanya ukaguzi wa usalama.

### MKALIMANI

- Mtu huyu atakalimani wakati wa vikao vya FGD na KII na lazima awe mtu anayezungumza lugha ya wenyeji. Kama sehemu ya mkutano wa kuanza, hakikisha kwamba Mkalimani anaelewa jinsi ya kukalimani/ kutafsiri kwa usahihi na ipasavyo istilahi kuhusu UWAKI na masuala ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono.
- Mkalimani pia anaweza kufanya utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia ikiwa ana tajriba ya awali katika kufanya ukaguzi wa usalama.

**Kuchukua na kunakili data**

- Kila mwanatimu anayeendesha shughuli ya kukusanya data anawajibu wa kuweka data na kurekodi kumbukumbu zao mwishoni mwa kila siku ya kukusanya data. Anapaswa kutumia violezo na zana zilizotolewa ili kuweka data na kuhakikisha kuwa data yake imehifadhiwa katika folda zinazolindwa kwa nenosiri. Mara tu data ghafi inaporekodiwa, lazima kumbukumbu zote ziharibiwe siku hiyo. Manenosiri yanapaswa kushirikiwa tu na wanatimu wengine wa Barometa, ikiwa ni pamoja na Kiongozi wa Timu, ambaye atawajibikia data hiyo.

**MSHUGHULIKIA / MSIMAMIZI / MFANYAKAZI WA MASUALA YA UWAKI**

- Lazima mtu huyu awe amefunzwa na ana uzoefu wa kusaidia wanawake na wasichana manusura katika unyanyasaji unaotekelezwa na wanaume (aina zote za UWAKI, zikiwemo unyanyasaji unaotekelezwa na mpenzi na unyanyasaji wa kingono). Lazima aweze kuzingatia kanuni ya usiri wakati wote, kulingana na kanuni elekezi.
- Atatoa usaidizi kwa manusura ambao watafichua walichopitia wakati wa utekelezaji wa Barometa na lazima awepo mwanzoni na mwishoni mwa kila kikao cha FGD ili aweze kujitambulisha na kupokea ufichuzi wowote.
- Lazima awe na uwezo wa kutoa utaalamu na ujuzi juu ya uwezo na upatikanaji wa huduma na rufaa za UWAKI.
- **Muhimu!** Ikiwa hakuna mwanamke kama huyo anayepatikana kutoka katika shirika lako au shirika mnaloshirikiana nalo, angalau, Mratibu anafaa kutenga muda mwanzoni mwa kikao cha FGD na ashiriki habari kuhusu huduma na usaidizi ambao washiriki wanaweza kupata. Kwa mfano, ikiwa kuna nambari ya simu za dharura katika eneo hilo, wapatie nambari hiyo na habari muhimu kuihusu, na jinsi ya kuipata. Iwapo kuna maeneo yoyote salama ya karibu, yanayoaminika na yanayojulikana ya wanawake na wasichana, eleza kikundi mahali yalipo, jinsi ya kuyapata na huduma zinazotolewa huko. Kufanya hivi kunaweza kusaidia kujenga imani kati ya Mratibu na washiriki.

    - *Angalia Hadidu za Rejea za Timu ya Ukusanyaji Data kwa mfano wa Hadidu za Rejea.*

# niwashiriki wa timu gani unahitaji katika shughuli ipi ya ukusanyaji wa data?

Kila shughuli ya kukusanya data inahitaji idadi fulani ya washiriki wa timu ya Barometa ili kukamilisha. Hapo chini utapata mwongozo wa wanaofaa kuwa katika timu kwa kila shughuli: Majadiliano ya Vikundi Lengwa, Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu, Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi.

Washiriki wa timu yako ya Barometa wanaweza kuwa katika shughuli moja au zaidi ya ukusanyaji wa data iliyo hapa chini, kulingana na upatikanaji na uzoefu wao.

## Majadiliano ya vikundi lengwa na wanawake na wasichana

Utahitaji angalau wanatimu watatu ili kuendesha kila FGD: Mratibu, Mnakili wa Kumbukumbu na Mfanyakazi/ Msimamizi/ Mtoa huduma wa masuala ya UWAKI. Ikihitajika, unaweza pia kuwa na Mkalimani. Washiriki wote wa timu ya FGD lazima wawe wanawake pekee.




Kanuni elekezi za kuwasaidia manusura zinapaswa kuzingatiwa kila wakati.

## Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII)

Utahitaji **angalau wanatimu wawili kwa kila Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu:** Mhoji na Mnakili wa Kumbukumbu.




Ikiwa unahitaji ukalimani, jumuisha jukumu hili la ziada kwenye timu.

## Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia

Utahitaji **angalau washiriki wawili wa timu kufanya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia kwa kila sehemu/eneo unalozingatia.**

Katika baadhi ya miktadha, maswali ya kufafanua kwa watoa huduma au wanajamii[20] yanaweza kuhitajika wakati wa kuchunguza. Hakikisha kuwa kuna mkalimani, ikihitajika, ambaye pia ni sehemu ya timu ya uchunguzi.




**Muhimu!** Hakuna wakati mshiriki wa timu anapaswa kufanya utafiti wa kuchunguza kwa kuangalia akiwa pekee yake.

## Tafiti za Mitazamo wa Wafanyakazi

Unahitaji tu **mwanatimu mmoja wa kufanya utafiti wa ana kwa ana na wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu**.

20 Kwamfano: Majiyanapatikana mara ngapikwenyevituovyamaji?Je, kwawastaniinachukua muda ganikusubirimaji?

Anayeongoza \Utafiti



Kulingana na ukubwa na upatikanaji wa timu yako na jinsi unavyoamua kufanya Tafiti za Mitazamo wa Wafanyakazi (ana kwa ana au mtandaoni), unaweza kuteua washiriki 2-3 wa timu ambao wanaweza kufanya tafiti hizi na kutenga nyakati maalum za kufanya hivyo.

Pia unapaswa kuzingatia lugha zinazohitajika kwa ajili ya utafiti wakati wa kuamua ni nani anafanya tafiti.

**Muhimu!** Waratibu wa utafiti **wasiwe** ni wa kutoka shirika wanalochunguza ili kuhakikisha usiri na kuhakikisha kuwa wanaoshiriki hawana wasiwasi.

# Kupanga na kusanifu ukusanyaji wa data

## Ushirikishaji wa wadau

Ushirikishaji wa wadau ni sehemu muhimu ya Barometa na hufanyika katika hatua tatu tofauti za utekelezaji:

1. **Katika hatua ya mipango na maandalizi** – kabla ya ukusanyaji wa data kuanza (*sehemu hii*)
2. **Katika hatua ya uchambuzi wa data** – baada ya ukusanyaji wa data kukamilika (*angalia Sehemu ya 3*)
3. **Katika hatua ya utetezi na usambazaji** – baada ya mapendekezo kukamilika (*angalia Sehemu ya 4*)

### Je, kwa nini wadau washirikishwe?

Ushirikishaji wa makundi mbalimbali ya wadau unaweza:

- Kuleta uungwaji mkono na imani kwa Barometa na madhumuni yake;
- Kukusaidia kupata muktadha wa mpango wako wa utekelezaji;
- Kukusaidia kukagua na kuthibitisha matokeo ya data yako na kuandaa mapendekezo;
- Kuibua fursa za utetezi wa pamoja (angalia *Sehemu ya 4. Utetezi na Usambazaji* kwa maelezo zaidi); na
- Kuongeza uwezekano kwamba watakubali mapendekezo yako ili kuboresha utoaji usaidizi wa kibinadamu kwa wanawake na wasichana (pia angalia *Sehemu ya 4. Utetezi na Usambazaji*).

### Wadau gani unafaa kushirikiana nao na lini?

Kutambua wadau wa kushirikisha kunafaa kufanyika kabla ya kuanza kwa ukusanyaji wa data, ili waweze kuelewa Barometa, kipi utakuwa ukifanya na zana hiyo na jinsi wanavyoweza kushiriki.

**Wahusika wa kitaifa na wa kimataifa wa kibinadamu:**

- Hawa wanaweza kujumuisha: mashirika ya Umoja wa Mataifa, mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGO), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, wawakilishi wa Kikosi Kazi/Kikundi cha Mtandao wa Kuzuia Unyanyasaji na dhuluma za Kingono (PSEA); Wawakilishi/waratibu wa makundi madogo ya kukabiliana na UWAKI—ikiwa ni pamoja na wale wanaotoa huduma za kukabiliana na UWAKI katika jamii ambapo Barometa itatekelezwa.
- Ikiwa unashirikiana na shirika la kibinadamu linaloshughulikia UWAKI, kuna uwezekano kwamba tayari utakuwa umeunganishwa na wengi wa wahusika hawa. Iwapo unatekeleza Barometa kwa kujitegemea, inashauriwa uwasiliane na mratibu wa masuala ya UWAKI katika eneo lako (pale inapofanya kazi) ili uunganishwe na jumuiya ya kibinadamu inayoshughulikia UWAKI. Vinginevyo, moja ya mashirika ya Umoja wa Mataifa (Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) au wahusika wa kibinadamu wa UWAKI wanaweza kukusaidia kwa taarifa.
- Madhumuni ya kuungana na kundi hili la wadau ni kuwafahamisha kuhusu Barometa na mipango yako; kujumuisha utaalamu wao wa kushughulikia UWAKI katika miktadha ya kibinadamu; na muhimu zaidi, kukusaidia katika kufikia mfumo wa kibinadamu na taratibu za uratibu wa kukabili UWAKI—hasa huduma zilizopo za UWAKI na rufaa kwa huduma za kukabiliana na UWAKI katika utoaji usaidizi wa kibinadamu. Utahitaji habari hizi na miunganisho hii ili uweze kuwaelekeza wanawake na wasichana wanaofichua ukatili au wanaohitaji msaada wakati wa utekelezaji wa Barometa kwa huduma zinazofaa na zinazopatikana. Hatua hii ni muhimu, hata kama unaweza kutoa huduma fulani katika shirika lako au shirika unaloshirikiana nalo.

- Kikundi hiki cha wadau pia kinaweza kukusaidia kumtambua mwanamke aliyehitimu ambaye anaweza kuwa Mfanyakazi wa Masuala ya UWAKI wakati wa ukusanyaji wa data na Majadiliano ya Vikundi Lengwa, ikiwa wewe au shirika unaloshirikiana nalo hamna mfanyakazi kama huyo.

**Wahusika na wawakilishi wa Serikali (ikiwa tu ni salama na inafaa kwako kujihusisha nao):**

- Kundi hili linaweza kujumuisha wawakilishi wa Wizara ya Masuala ya Wanawake/ Usawa wa Jinsia au idara sawa ya serikali inayoshughulikia haki za wanawake.
- Unaweza kutumia mazungumzo haya na wawakilishi wa serikali ili:
    - Kuuliza kuhusu changamoto na mitazamo yao kuhusu dharura, hasa inayohusiana na wanawake, wasichana na UWAKI na udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono;
    - Kuwafahamisha kuhusu Barometa, mipango yako na madhumuni ya mipango hiyo;
    - Kuwashauri kuhusu taarifa mpya ambayo Barometa inaweza kuibua;
    - Kufafanua jinsi Barometa inaweza kusaidia kazi yao;
    - Kujadili njia za kuwahusisha na kushirikiana nao wakati wote wa utekelezaji wa Barometa; na
    - Kukubalini jinsi maendeleo ya utekelezaji na matokeo na mapendekezo yatashirikiwa wakati wa hatua ya utetezi na usambazaji.

**Wahusika, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake katika eneo husika**:

- Unapaswa kushirikisha kundi hili pana la wadau ili kupata usaidizi wao katika:
    - Ushauri kuhusu muktadha na kuendeleza mpango wako wa utekelezaji;
    - Kupitia matokeo ya data na uthibitisho baada ya ukusanyaji wa data kukamilika;
    - Kuandaa mapendekezo; na
    - Kushiriki katika utetezi wa pamoja, kutoa ushawishi katika ngazi ya kitaifa na kuleta mapendekezo yako ya utetezi kwa serikali (ikiwa ni salama kufanya hivyo) na wadau wengine pamoja na watoa maamuzi (kama vile mashirika ya Umoja wa Mataifa, wafadhili).

**Viongozi na wanajumuiya ya wanawake wenyeji, waliohamishwa na wakimbizi:**

- Unapaswa kushirikisha kundi hili ili kupata usaidizi wao katika:
    - Kushauri kuhusu muktadha wa mpango wako wa utekelezaji ikiwa jumuiya zao zitajumuishwa katika sehemu moja au zaidi ya utekelezaji wa Barometa, na kutambua washiriki;
    - Kuthibitisha data baada ya ukusanyaji wa data kukamilika; na
    - Kuchambua matokeo ya Barometa na hatua zilizochukuliwa.

# Kupanga ratiba

**Barometa inakusudiwa kuwa tathmini ya "haraka" ya muktadha wa kibinadamu na haipaswi kuchukua zaidi ya wiki mbili kwa ukusanyaji wa data ikijumuisha mkutano wa kuanza**. Inaweza kujumuisha siku chache za ziada za maandalizi, kuweka alama, uchambuzi na uandaaji wa mapendekezo.

Muhtasari wa mfano wa ratiba hii ya utekelezaji:

| Hatua ya barometa | Siku | Shughuli | Kwa maelezo zaidi |
|---|---|---|---|
| **Mipango na maandalizi** | siku 5 | Mkutano na wadau, kukusanya hati, kuchagua maeneo na wahojiwa, upangaji wa bajeti, ratiba, n.k. | Hati hii, *Sehemu ya 1* |
| **Mkutano wa kuanza na timu ya Barometa** | siku 2 | Mkutano wa lazima wa kutoa mafunzo kwa timu kuhusu Barometa na ukusanyaji wa data.<br><br>Ikihitajika, ongeza muda katika kipindi ili kujikumbusha mafunzo kuhusu UWAKI na/au dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. | Angalia *Mkutano wa Kuanza Kukusanya Data* |
| **Ukusanyaji wa data** | siku 12 | Kufanya Majadiliano ya Vikundi Lengwa, Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu, Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Tafiti za Mitazamo ya Wafanyakazi. | Angalia *Sehemu ya 2* |
| **Uchambuzi wa data, uthibitisho na mapendekezo** | siku 3 | Kuchambua data, kuyakinisha data kwa wadau wakuu na kuandaa mapendekezo. | Angalia *Sehemu ya 3* |
| **Utetezi na usambazaji** | Muktadha utaamua | Kuamuliwa kulingana na muktadha (Kumbuka: Lenga kuanza hili punde tu unapokamilisha kuandaa mapendekezo na utetezi wako). | Angalia *Sehemu ya 4* |

Ili kuandaa na kukamilisha ratiba yako, pitia hatua mbili zinazofuata: kupanga bajeti na kuchagua maeneo unayotaka pamoja na washiriki. Hatua hizi zitakuwezesha kukamilisha maelezo na kubainisha mawanda ya shughuli zako za kukusanya data.

- *Angalia Ratiba ya Utekelezaji ili upate mfano wa kina ya ratiba ya utekelezaji wa Barometa unaozingatia timu yenye idadi ya chini ya washiriki wanne.*

# Kupanga bajeti

**Utekelezaji wa Barometa utahitaji bajeti na rasilimali.** Kiasi cha fedha na rasilimali unazohitaji zitategemea kile ambacho tayari unacho na kile utahitaji ili kutekeleza Barometa kikamilifu.

Ili kukusaidia kufikiria ni ufadhili gani na/au rasilimali nyingine zipi utakazohitaji, haya hapa ni maswali elekezi na mambo ya kuzingatia:

- **Timu ya Barometa:**
  - o Je, utahitaji wanatimu wangapi ili kutekeleza Barometa (kwa kuzingatia mahitaji ya chini ya watu wanne)?
  - o Ni asilimia ngapi ya muda wa kila mwanatimu itahitajika?
  - o Je, itagharimu nini kwa wanatimu kufanya kazi kwenye Barometa—kwa mfano, kufanya kazi muda wote katika ratiba ya wiki mbili ya kukusanya data?

- **Mkutano wa kuanza barometa:**
  - o Je, utaufanyia mkutano huu wapi?
  - o Je, utahitaji rasilimali au vitu maalum, kama vile chakula na vinywaji?
  - o Ikiwa unaufanyia mtandaoni, ni mambo gani ya ziada, rasilimali, vifaa vya TEHAMA au programu unahitaji?
- **Vifaa vya kukusanya data**:
  - o Ni gharama gani za uchapishaji zinahusishwa na zana za kukusanya data?
  - o Je, unakusanya data kwenye programu au jukwaa gani?
  - o Je, utakuwa ukihifadhi na kutunza taarifa hizo vipi?
- **Ukalimani/ tafsiri:**
  - o Utafanya kazi yako katika lugha gani?
  - o Je, utahitaji usaidizi wa ukalimani au tafsiri? Ikiwa ndiyo, itagharimu kiasi gani?
- **Mawasiliano:**
  - o Je, utahitaji pesa au rasilimali ili kuhakikisha kuwa timu yako inaweza kuwasiliana na kila mmoja na pia na wadau na washirika wote wa Barometa?
- **Usafiri:**
  - o Utahitaji usafiri gani ili kufanya shughuli za Barometa, hasa ukusanyaji wa data?
  - o Je, unaweza kupata usafiri huo?
  - o Je, utahitaji kukodi huduma za usafiri? Je, itagharimu nini? Je, utauhitaji kwa muda gani?
  - o Je, utaweza kumpata dereva anayejulikana na anayeaminika?
- **Ushirikiano:** Iwapo shirika lako ni la kibinadamu linaloshughulikia UWAKI ambalo linashirikiana na kikundi, shirika au mtandao wa haki za wanawake, utahitaji kuzingatia gharama za mshirika, muda wa wafanyakazi na uwezekano wa kusafiri, malazi, fidia ya kila siku na matumizi mengine. Maelezo ya ushirikiano, ikiwa ni pamoja na bajeti, yanafaa kutengenezwa kwa ushirikiano na mshirika wakati mnakubaliana kutekeleza Barometa.

Ili kujibu baadhi ya maswali ya bajeti, pitia sehemu inayofuata, *Kuchagua Maeneo Yako na Washiriki,* ili ikusaidie kuamua bajeti na rasilimali utakazohitaji (kwa mfano, aina ya usafiri, vifaa vya mawasiliano, wanatimu wa ziada, n.k.)

# Kuchagua maeneo yako na washiriki

Huenda haitawezekana kutathmini dharura yote ya kibinadamu wakati wa kutekeleza Barometa. Kwa hivyo ni muhimu kuchagua kwa uangalifu maeneo na sehemu mahususi ambapo Majadiliano ya Vikundi Lengwa, Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu na Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia utafanyiwa katika muktadha wa dharura ya kibinadamu.

Kutathmini eneo au sehemu ya kipekee wakati wa utoaji usaidizi wa kibinadamu bado kunaweza kutoa "muhtasari" wenye thamani wa habari kuhusu utoaji wa usaidizi wa kibinadamu bila kuzamia eneo kwa upana. Itakuwa muhimu kuchagua maeneo **ambayo ni salama na inawezekana** kutekeleza, ambapo inawezekana kukamilisha utekelezaji **ndani ya muda uliopendekezwa wa wiki mbili**, na pale unapoweza kujihusisha na **washiriki anuwai walio muhimu kwa muktadha wako wa dharura** kutoka katika:

- Kila **eneo lililoathiriwa** (k.m., mijini, pembezoni mwa miji, kambi au makazi yasiyo rasmi);
- Kila **kundi lililoathirika** (k.m., mwenyeji, wanaorejea, wakimbizi au waliofurushwa makwao (IDP); na
- Kila **rika la umri** (wanawake na wasichana waliobalehe).

**Muhimu:** Lenga kuchagua **maeneo maalum yasiyozidi manne** ambapo utatekeleza Barometa.

## Mwongozo wa hatua kwa hatua: Hatua 6 za kukusaidia kuchagua maeneo yako na vikundi vya washiriki

Fuata kwa umakini hatua hizi sita ili zikusaidie kuamua maeneo yako maalum na vikundi vya washiriki kwa ajili ya utekelezaji wa Barometa na ukusanyaji wa data.

### 1. Shirikiana na wanawake na wasichana waliobalehe katika utekelezaji wa Barometa

Jihusishe na vikundi vya wanawake na wasichana waliobalehe kama sehemu ya utekelezaji wa Barometa.

### 2. Tambua vikundi vilivyoathiriwa katika dharura yako ya kibinadamu

Chagua vyote ambavyo ni muhimu:

- ☐ Jumuiya ya wenyeji
- ☐ Wanaorejea
- ☐ Wakimbizi
- ☐ Waliofurushwa makwao (IDP)

### 3. Tambua maeneo yaliyoathiriwa katika dharura yako ya kibinadamu

Chagua vyote ambavyo ni muhimu:

- ☐ Miji
- ☐ Pembezoni mwa miji
- ☐ Kambi
- ☐ Makazi yasiyo rasmi

## 4. Orodhesha maeneo yote yanayofaa kwa utekelezaji wa Barometa

Orodhesha maeneo maalum yaliyoathiriwa na janga la kibinadamu na ubainishe ni vikundi gani vinaishi maeneo hayo na kama kuna usaidizi wa kibinadamu ambao tayari unatolewa katika eneo hilo.

Kufanya hivyo kutakusaidia kupunguza maeneo na washiriki wa kuchagua hali itakayokuruhusu kushughulikia vikundi na maeneo mengi iwezekanavyo.

Tumia jedwali hili kuweka taarifa kuhusu sehemu zote tarajiwa katika eneo lako ambazo zimeathiriwa na dharura ya kibinadamu (mifano imetolewa katika maandishi yaliyolazwa):

| Eneo | Sehemu | Usaidizi | Wenyeji | Wanaorejea | Wakimbizi | Waliofurushwa makwao (IDP) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *Miji* | *Mji "A"* | | *X* | | | *X* |
| *Miji* | *Mji "B"* | *X* | *X* | *X* | | |
| *Pembezoni mwa miji* | *Nje mwa mji "B"* | | | | | |
| *Kambi* | *Kambi "A"* | *X* | | | *X* | *X* |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

## 5. Usalama: tathmini ya haraka ya hatari kwa maeneo tarajiwa

Kuzingatia usalama wa sehemu tarajiwa ni hatua muhimu katika mchakato huu na kutakusaidia kuondoa au kuchagua sehemu kulingana na usalama wa jumla *na* usalama wa sehemu hizo kwa wanawake.

Ili kukusaidia kuchuja na kuchagua sehemu unazotaka, tumia zana ya ***Tathmini ya Haraka ya Usalama***. Zana hii itakusaidia kutafakari kuhusu sehemu tarajiwa kwa kuzingatia mtazamo wa usalama unaolenga wanawake. Itakuuliza mfululizo wa maswali ili kukusaidia kuamua kama sehemu hiyo itakuwa salama vya kutosha kwa timu yako. Zana hii imeundwa mahususi kwa kuzingatia usalama wa wanawake. Kwa hivyo itakuwa sehemu muhimu ya kuangazia katika upangaji wako wowote wa usalama na utayarishaji na ufuatiliaji wakati wote wa utekelezaji.

**Muhimu:** Hata kama una wafanyakazi wa usalama na umeanzisha mifumo ya usalama ama katika shirika lako mwenyewe au kupitia unaoshirikiana nao katika Barometa, bado inashauriwa ujumuishe zana hii inayowalenga wanawake—pamoja na taratibu zako za usalama zilizopo—ili kuhakikisha kwamba usalama wa wanawake unazingatiwa.

Kwa taarifa za hivi punde kuhusu usalama katika muktadha wako wa kibinadamu, unaweza kupata taarifa hizo kutoka kwa waratibu na ripoti za hali za Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu masuala ya Kibinadamu (OCHA), taarifa za usalama za Idara ya Usalama na Ulinzi ya Umoja wa Mataifa (UNDSS), pamoja na jumuiya ya kibinadamu na wafanyakazi wenzako wa misaada kwa wanawake na wahusika, makundi na mashirika ya haki za wanawake.

## 6. Chagua maeneo ya utekelezaji wa Barometa

**Kikumbusho:** Lenga kuteua **maeneo yasiyozidi manne ya utekelezaji wa Barometa.** Kumbuka kwamba ratiba ya utekelezaji ya wiki 2 inapendekezwa.

Kwa kutumia taarifa ulizokusanya kutoka hatua ya 2-6, **chagua hadi maeneo manne** ambayo yatakuruhusu kujihusisha, kwa usalama iwezekanavyo, na vikundi vingi vilivyoathiriwa katika maeneo tofauti yaliyoathiriwa, ili kuhakikisha washiriki ni anuwai iwezekanavyo.

**➔ Kwa mfano:**

- Ikiwamuktadhawakowakibinadamu una maeneo yote manneyaliyoathirika—mijini, pembezonimwamiji, kambinamakaziyasiyorasmi—unawezakutekeleza Barometa katika sehemumojandogondaniyakilamojawapoyamaeneohaya.
- Ikiwa muktadhawako una kambinamakaziyasiyorasmi, unawezakutekeleza Barometa katikasehemumoja au mbilindogo katika kilamoja wa poyamaeneohayamawili..
- Kwa kuzingatialengolinalopendekezwa la vikao 6-8 vya FGD kwa utekeleza jimzimawaBarometa, kufanya hivyokutakuruhusukujihusishanavikundi 6-8 tofautivyawanawakena wasichana kutoka vikundianuwai, maeneonasehemutofautikatikamuktadhawakowadharura.

## Upatie kipaumbele uchaguzi wa eneo

Hivi hapa ni vidokezo vichache vya mwisho vya kukusaidia kuweka kipaumbele na kufanya uteuzi wako wa mwisho:

- Jaribu kuchagua angalau sehemu moja kutoka kila eneo lililoathiriwa, ambayo itakuruhusu kujihusisha na kila kikundi kilichoathiriwa angalau mara moja.
- Pale ambapo ni salama kufanya hivyo, jaribu kujumuisha sehemu mahususi zisizo na au zilizo na huduma chache ya usaidizi wa kibinadamu na/au zinachukuliwa kuwa "ngumu kufikia," ili Barometa pia iweze kutathmini maeneo ambayo huenda yana mahitaji zaidi, yametengwa zaidi, au ambapo watu wametengwa zaidi.
- Jaribu kujumuisha sehemu (ambazo ni salama vya kutosha na zinafikika) ambazo zimejumuishwa kwenye ***Mpango wa Nchi wa Usaidizi wa Kibinadamu*** (ikiwa upo). Kwa kawaida maeneo kama hayo yatapatikana kupitia OCHA na Mratibu wa Usaidizi wa Kibinadamu ndani ya nchi,[21] au kupitia tovuti ya Taarifa za Usaidizi wa Kibinadamu.[22]
- Wakati wa kuamua shemu unazotaka, zingatia kuchagua sehemu ambayo inaweza kuchunguzwa (kupitia Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia) kwa siku moja pekee (yaani, chagua kambi au eneo/sehemu ya kambi ambayo unajua unaweza kuangalia au kutembea ndani, kwa siku moja).
- Ukubwa wa timu yako utaathiri ni sehemu ngapi unazoweza kuzishughulikia ndani ya wiki mbili, kwa hivyo unaweza kuzingatia umbali kati ya sehemu husika. Kwa mfano: Ikiwa utakuwa ukifanya kazi na timu ya wanawake wanne, utaweza tu kufanya shughuli moja ya kukusanya data kwa wakati:
    - o Unaweza kukamilisha vikao viwili vya FGD kwa siku (kimoja asubuhi, kimoja alasiri);
    - o Unaweza kukamilisha uchunguzi wa sehemu moja kwa siku.
- **Nafasi salama za kufanyia FGD zako ni jambo kuu la kuzingatia wakati unachagua sehemu zako**. Tambua maeneo ambapo nafasi salama na zinazofaa zinapatikana. Kwa umahususi:
    - o FGD zifanyike katika chumba/sehemu ambapo hakuna shughuli nyingine inayofanyika na hakuna mtu mwingine nje ya majadiliano anayeweza kuivuruga, ili kudumisha usiri. Kunapaswa kuwa na kumbi/nafasi zinazopatikana katika eneo, ambazo zimetambuliwa kuwa salama na ambazo wanawake na wasichana wanaweza kufika (ikiwa huna habari hizi, fanya kipaumbele kujua).
    - o Zaidi ya hayo, wakati wowote inapowezekana, sehemu yenye mahali pa kutunzia watoto inafaa kupendekezwa kwa wanawake walio na watoto wadogo.
- **Muhimu!** Hatimaye, wakati wa kuamua kuhusu maeneo yako, inashauriwa kuwa na **maeneo mbadala** (mbadala B, mbadala C, n.k.) yakiwa tayari na ukiwa umekubaliana na wenyewe iwapo eneo lako la kwanza (mpango wa kwanza) halipatikani kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya usalama au ya kibinadamu.

21 Unaweza kupata mifano ya Mipango ya Usaidizi wa Kibinadamu kwa Nchi hapa: Sudan Kusini - https://reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/south_sudan_humanitarian_response_plan_2019_final.pdf | Syria - https://www.humanitarianresponse.info/en/operations/syria/document/2015-syrian-arab-republic-strategic-response-plan.

22 Taarifa za Usaidizi wa Kibinadamu: https://www.humanitarianresponse.info/.

# Kujiandaa kwa ukusanyaji wa data

## hati muhimu za kukusanya na kukagua

Kwa uchache, inapopatikana kama sehemu ya usaidizi wa kibinadamu, hati muhimu zifuatazo zinapaswa kuchuliwa na kukaguliwa na timu ya Barometa wakati wa hatua ya kupanga:

- **Hati za Kikundi Kinachoshughulikia UWAKI:** Taratibu za Kawaida za Kushughulikia UWAKI au Njia za Rufaa kama zinavyopatikana kwa eneo la utekelezaji; data iliyokusanywa katika Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za UWAKI (GBVIMS); ukaguzi na tathmini za usalama
    - ➔ Tathmini za Mtandao wa Kuzuia Unyanyasaji na Dhuluma za Kingono (PSEA) na itifaki za kuripoti, kama zinavyopatikana
    - ➔ Ripoti na tathmini za ushiriki na uwakilishi wa wanawake, kama zinavyopatikana
    - ➔ Ripoti na tathmini za uchambuzi wa jinsia na nguvu, kama zinavyopatikana
    - ➔ Mipango ya Usaidizi wa Kibinadamu

Hati hizi kwa kawaida hupatikana kutoka kwenye sekta ndogo ya UWAKI (kwa mifano: tembelea kurasa za Afghanistan au Syria zilizosasishwa katika Taarifa za Usaidizi wa Kibinadamu) au kutoka kwenye Mtandao wa Kuzuia Unyanyasaji na Dhuluma za Kingono (PSEA) (kwa mifano: tembelea hati zinazopatikana kutoka Jordan au Bangladesh).

Hati hizi zinapaswa kukaguliwa na timu ya Barometa kabla na wakati wa mkutano wa siku 2 wa kuanza ikiwa kuna wakati (angalia hapa chini).

## Kuelewa njia za rufaa na mawasiliano za UWAKI

Wanawake na wasichana wanaweza kufichua matukio ya ukatili wakati wa utekelezaji wa Barometa. Kwa hivyo, **ni muhimu kwa wanatimu wote wa Barometa wajue jinsi ya kuwaelekeza waathiriwa katika huduma zinazopatikana na zinazofaa za kukabiliana na UWAKI. Hii inajumuisha wanawake wanaofanya kazi katika dharura.**

Hakikisha yafuatayo yanatekelezwa kila wakati:

- **Kwa wanawake na wasichana walio katika jamii zilizoathirika au zinazolengwa**:
    - o Mfanyakazi/Msimamizi wa kike wa masuala ya UWAKI lazima awe katika timu ya kukusanya data;
    - o Wakati wa vikao vya FGD na wanawake na wasichana, Mfanyakazi/Msimamizi wa kike wa masuala ya UWAKI anapaswa kujitambulisha mwanzoni na mwisho wa kikao hicho, na awe tayari kutoa msaada wowote kwa wanawake na wasichana kulingana na kanuni zinazomlenga manusura na njia za rufaa;
    - o Kwa ujumla, wakati wa mchakato mzima wa ukusanyaji wa data, Mfanyakazi/Msimamizi/ Mtoa huduma wa kike wa masuala ya UWAKI anafaa kupatikana, iwapo kutakuwa na ufichuzi au wasiwasi ambao unaweza kutokea katika hatua au sehemu yoyote ya mchakato.
- **Kwa wanawake wanaofanya kazi ya misaada ya kibinadamu:**
    - o Mwanatimu ya ukusanyaji wa data ya Barometa ambaye ni mwanamke anayeendesha Tafiti za Mitazamo ya Wafanyakazi ni sharti afahamu na aweze kuonyesha uelewa wa vitendo na matumizi ya njia na itifaki maalum za rufaa kwa wahudumu wa kike wa kibinadamu pamoja na huduma zinazofaa na/au usaidizi unaopatikana kwao. Maelezo haya ambayo ni mahususi kwa muktadha lazima pia yajumuishwe katika zana ya utafiti mtandaoni na katika usambazaji wowote wa utafiti wa mtandaoni.

# Mkutano wa siku 2 za mwanzo wa timu ya kukusanya data

Ni lazima kwamba baada ya timu ya kukusanya data kuundwa, inafaa kushiriki katika mkutano wa kuanza ili kujiandaa kwa ajili ya ukusanyaji wa data. Mkutano huu unajumuisha taarifa muhimu kuhusu Barometa na vipengele vya mafunzo kuhusu jinsi ya kuitumia na zana za kukusanya data.

Inashauriwa sana kuwa uwe **Mkutano wa siku 2** ili kuwa na muda wa kutosha wa kushughulikia mada zote muhimu. Unaweza kuzingatia kupunguza urefu au kuuongeza kwa siku chache ili kuendana na ratiba zako, lakini hili litategemea mahitaji ya timu, hasa kuhusu kuhakikisha uelewa wa masuala ya kimaadili na usalama na jinsi ya kutumia zana.

Inafaa kufafanuliwa kwamba **haya si mafunzo ya kukabili UWAKI au kuzuia dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono**. Mkutano huu wa kuanza umeundwa mahususi ili kutoa mafunzo kwa timu ya kukusanya data kuhusu jinsi ya *kutekeleza Barometer* pekee.

Ukitathmini kuwa timu ya Barometa inahitaji muda zaidi kuliko uliotolewa katika ajenda ya mfano iliyo hapa chini kuhusu UWAKI na/au dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono, unaweza kuuongeza kama kipengele tofauti cha mafunzo. **Ni muhimu kukumbuka, hata hivyo, kwamba timu ya ukusanyaji wa data lazima iwe tayari ina ujuzi na uzoefu wa awali katika kushughulikia UWAKI na/au dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono, na tayari wawe wamefunzwa kuhusu dhana kuu za UWAKI, kanuni elekezi na huduma inayomzingatia manusura**.

Ili kupunguza idadi ya washiriki, ni timu nzima ya Barometa pekee ndiyo inapaswa kujumuishwa katika mkutano huu.

- *Kwa mada za msingi ambazo lazima zishughulikiwe na mkutano huu, angalia Mkutano wa Kuanza Kukusanya Data ili upate ajenda ya kina ya mkutano wa kuanza wa siku 2 na slaidi za uwasilishaji.*

# Mfano wa Ajenda ya Mkutano wa siku 2 wa Kujiandaa Kukusanya Data

## Kujiandaa Kukusanya Data: Agenda ya Mkutano wa Siku 2

**Mwishoni mwa mkutano, washiriki watakuwa na:**

- Uelewa wa Mradi wa Sikiliza! na Barometa
- Uelewa wa madhumuni na matumizi ya zana zote za ukusanyaji wa data na uelewa uliokubaliwa wa kukusanya data kulingana na kanuni za ufeministi
- Makubaliano ya kikundi juu ya wajibu, majukumu, usalama, ulinzi na mbinu bora

**Kabla ya mkutano, waratibu wanapaswa kuwa:**

- Wamechapisha hati zinazohitajika
- Wamepitia wajibu na majukumu ya uratibu
- Wamekagua na kurekebisha (panapohitajika) wasilisho la PowerPoint

- *Angalia sehemu ya Mkutano wa Kuanza Kukusanya Data, iliyo na mifano ya slaidi za wasilisho za kuambatana na ajenda hii.*

## Siku ya 1

| | |
|---|---|
| **9:00-9:15** | **Kukaribishwa, Kujuana, Kuweka Kanuni za Msingi**<br>▪ Majina, wajibu, umefanya kazi hii kwa muda upi, umefanya kazi kwa muda upi au umeishi katika eneo hili kwa muda upi?<br>▪ Kichocheo - kwa mfano, jina lako linamaanisha nini? Je, unapenda kufanya nini kwa ajili ya kujiburudisha? Au kitu chochote kingine kama inavyohitajika! |
| **9:15-10:00** | **Mradi wa Sikiliza! na Barometa ni nini?**<br>▪ Mradi wa Sikiliza! (tazama slaidi ya Historia katika hati ya wasilisho)<br>▪ Muhtasari wa Barometa (Kwa nini tuko hapa na kwa nini tumekuomba ufanye kazi hii leo?) (Angalia 0a. Utangulizi wa hati ya Barometa ya Sikiliza! kwa maelezo zaidi juu ya vidokezo hivi):<br>Barometa ni nini? Lengo lake ni lipi?<br>o Viwango vya chini vilivyoongoza kubuniwa kwake<br>o Mradi wa Skiliza! ambao umetumiwa katika Barometa<br>o Barometer inalenga nani?<br>o Je, tunapaswa kuitumia lini? Kwa nini tumeamua kutekeleza Barometa sasa?<br>o Je, tunapimaje usaidizi wa kibinadamu kwa kutumia Barometa?<br>▪ **Ajenda ya siku mbili zijazo:**<br>o Ukaguzi wa dhana za msingi za ukatili wa kijinsia (UWAKI), kanuni elekezi na usaidizi unaozingatia manusura<br>o Istilahi na lugha<br>o Misingi ya ukusanyaji wa data ya wanawake<br>o Ukusanyaji wa data: ukaguzi na matumizi ya zana<br>o Mazingatio ya usalama na maadili na ulinzi<br>o Wajibu na majukumu ya kila mwanatimu ya Barometa<br>o Makubaliano ya Kikundi na Kanuni za Maadili<br>o Ukaguzi wa mawasiliano na njia za rufaa za UWAKI<br>o Ukaguzi wa hati muhimu za kibinadamu |
| **10:00-10:30** | **Ukaguzi wa dhana za msingi za UWAKI, kanuni elekezi na usaidizi unaomlenga manusura** |
| **10:30-11:30** | **Istilahi na lugha**<br>▪ Kufafanua na kutafsiri dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono na istilahi nyingine msingi za UWAKI.<br>▪ Kujadili tafsiri na njia za kufasiri ufafanuzi huu kwa usahihi na kwa ubayana katika lugha ya muktadha ambapo Barometa itatekelezwa.<br>▪ Hakikisha timu nzima inakubali na inaelewa lugha inayotumiwa. |
| **11:30-12:30** | **Misingi ya ukusanyaji wa data ya wanawake**<br>▪ Nadharia kuu ya ufeministi na kanuni zinazosimamia uzuiaji na utoaji usaidizi wa UWAKI:<br>▪ Jumuishi na Shirikishi<br>▪ Zinazolenga wanawake, wasichana na manusura<br>▪ Zinalenga kutumia data kufanya utetezi (si kuripoti wafadhili!) |

**12:30-13:30**

**Mapumziko ya chakula cha mchana**

**13:30-17:30**

**Rekebisha wakati kama inavyohitajika ili kujumuisha mapumziko na uhakikishe kuwa timu yako ina muda wa kutosha kuelewa kila zana kikamilifu na jinsi ya kuitumia.**

**Ukaguzi wa zana na mazoezi ya matumizi (saa 4)**

**Kunakili kumbukumbu**

- Wape wanakikundi hati hizi tatu na uwaombe wazipitie
  - Mwongozo wa ukurasa 1 wa Wanaoandika Kumbukumbu
  - Kiolezo cha Kumbukumbu za Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD)
  - Kiolezo cha Kumbukumbu za Mahojiano ya Mtoa Taarifa Muhimu (KII)
- Angalia uelewa wa washiriki. Ni muhimu kila mtu aelewe jinsi ya kuandika kumbukumbu nzuri na bayana. Waambie watumie mwongozo huu na violezo hivi wakati wa kufanya mazoezi. Ikiwa wanatumia kompyuta kuandika kumbukumbu, shiriki nao violezo pepe.
- Wale wanaoandika kumbukumbu wakati wa mazoezi—na hasa wale ambao watakuwa wakiandika kumbukumbu za Barometa—wanapaswa kutumia violezo vya madokezo ama kuandika kwa mkono au kuchapa kumbukumbu zao kwa Kiingereza. Ingekuwa vyema zaidi kuandika kumbukumbu kwa mkono kama watakavyofanya wakati wa vipindi halisi vya FGD na KII. Kwa njia hii wanaweza kufanya mazoezi ya kuandika kumbukumbu nzuri na bayana.

*(Kwa zana zote za kukusanya data, angalia: Kiambatisho cha Zana za Kukusanya Data)*

- **Zana ya FGD**
- Peana zana za FGD.
- Mtu mmoja mmoja au wawili, kagua zana kwa kuzisoma.
- Maswali/Majibu: Tenga muda kujibu maswali yoyote ambayo timu inaweza kuwa nayo kuhusu zana.
- Ni nani atatumia zana hii: Kagua lini na jinsi zana itatumiwa na washiriki mahususi wa timu.
- **Mazoezi na maigizo:** Fanya mazoezi ya kuendesha Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD) kwa kuhakikisha kila mtu amepitia majukumu mbalimbali—mtu 1 au 2 wanaangalia, mtu 1 anaendesha kikao cha FGD, wengine ni washiriki, 1 ndiye anayeandika kumbukumbu. Uliza maswali 2-3 pekee katika mazoezi, lakini kila mtu asome na aelewe utangulizi na umuhimu wake. Hakikisha kila mtu anashiriki, ana jukumu na anahusika. Kama sehemu ya maigizo haya, lazima mpitie kila wakati mchakato wa kupata idhini na mjumuishe taratibu za ufichuzi katika mazoezi hayo. Kwa vipindi hivi vya mazoezi, unaweza kuwaleta wenzako ambao si sehemu ya timu ya Barometa ili wachukue nafasi ya “washiriki wa FGD” na waigize nafasi hizo, kisha uwajumuishe katika mchakato wa kupata maoni hapa chini.
- **Maoni:** Baada ya kila kipindi cha mazoezi, waombe washiriki wajibu maswali yafuatayo:
  - Ni nini kilifanya kazi vizuri katika zana husika?
  - Ni nini hakikufanya kazi vizuri au kilikuwa changamoto katika FGD?
  - Ni lugha/ istilahi zipi, kama zipo, ambazo bado huelewi vizuri au unahitaji maelezo na/au ufafanuzi zaidi? Je, dhana za dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono na UWAKI zinaeleweka na kujadiliwa vipi? Je, makundi yetu yataelewa?
  - Je, tunahitaji kurekebisha lugha yoyote katika zana ili kuambatana na muktadha wetu? Kama ndiyo, jadili na uhakikishe kuwa mnakubaliana kuhusu lugha kama timu. Hatua hii ni muhimu ili kuhakikisha kuwa zana zinafaa na kwamba vikundi vya wanawake na wasichana ambao utashiriki nao watazielewa.
- **Mwongozo wa Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi**
  - Peana zana.
  - Mtu mmoja mmoja au wawili, kagua zana kwa kuzisoma.
  - **Maswali/Majibu:** Tenga muda kujibu maswali yoyote ambayo timu inaweza kuwa nayo kuhusu zana.
  - **Ni nani atatumia zana hii:** Kagua lini na jinsi zana itatumiwa na washiriki mahususi wa timu.

- **Mazoezi na maigizo:** Fanya mazoezi ya kufanya utafiti kwa kuhakikisha kila mtu amepitia majukumu mbalimbali—mtu 1 au 2 wanaangalia, mtu 1 ndiye mhoji, mtu 1 ndiye mhojiwa. Uliza maswali 5 pekee katika mazoezi, lakini kila mtu asome na aelewe utangulizi na umuhimu wake. Hakikisha kila mtu anashiriki. Kama sehemu ya maigizo, lazima mpitie kila wakati mchakato wa kutoa idhini na mjumuishe taratibu za ufichuzi kutoka kwa wafanyakazi wa kibinadamu wa kike katika mazoezi hayo. Kwa vipindi hivi vya mazoezi, unaweza kuwaleta wenzako ambao si sehemu ya timu ya Barometa ili wachukue nafasi ya "wafanyakazi washiriki" na uwajumuishe katika mchakato wa kupata maoni hapa chini.
- **Maoni:** Baada ya kila kipindi cha mazoezi, waombe washiriki wajibu maswali yafuatayo:
  - Ni nini kilifanya kazi vizuri katika zana husika?
  - Ni nini hakikufanya kazi vizuri au kilikuwa changamoto katika utafiti?
  - Ni lugha ipi, kama ipo, ambayo bado huelewi vizuri au unahitaji maelezo na/au ufafanuzi zaidi?
- **Zana ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia**
  - Peana zana.
  - Mtu mmoja mmoja au wawili, kagua zana kwa kuzisoma.
  - Maswali/Majibu: Tenga muda kujibu maswali yoyote ambayo timu inaweza kuwa nayo kuhusu zana.
  - Ni nani atatumia zana hii: Kagua lini na jinsi zana itatumiwa na washiriki mahususi wa timu.
  - Shiriki mifano ya wakati unaweza kutumia sehemu maalum za zana ya kuchunguza kwa kuangalia. Ikiwa walio kwenye timu wanafaa kutoa majibu katika sehemu ambayo utaangazia, mnaweza hata kuanza kujibu baadhi ya maswali au kuonyesha jinsi sehemu ya zana tayari imejazwa kulingana na ukaguzi wa hati.
  - Jadili sehemu ambazo utaangazia.
- **Zana ya KII**
- Peana zana.
- Mtu mmoja mmoja au wawili, kagua zana kwa kuzisoma.
- **Maswali/Majibu:** Tenga muda kujibu maswali yoyote ambayo timu inaweza kuwa nayo kuhusu zana.
- **Ni nani atatumia zana hii:** Kagua lini na jinsi zana itatumiwa na washiriki mahususi wa timu.
- **Mazoezi na maigizo:** Fanya mazoezi ya kufanya mahojiano ya KII kwa kuhakikisha kila mtu amepitia majukumu mbalimbali—mtu 1 au 2 wanaangalia, mtu 1 ndiye mhoji, mtu 1 ndiye mhojiwa. Uliza maswali 5 pekee katika mazoezi, lakini kila mtu asome na aelewe utangulizi na umuhimu wake. Hakikisha kila mtu anashiriki. Kwa vipindi hivi vya mazoezi, unaweza kuwaleta wenzako ambao si sehemu ya timu ya Barometa ili wachukue nafasi ya "wawakilishi kutoka mashirika yanayoshughulikia masuala ya wanawake" na uwajumuishe katika mchakato wa kupata maoni hapa chini.
- **Maoni:** Baada ya kila kipindi cha mazoezi, waombe washiriki wajibu maswali yafuatayo:
  - Ni nini kilifanya kazi vizuri katika zana husika?
  - Ni nini hakikufanya kazi vizuri au kilikuwa changamoto katika KII?
  - Ni lugha ipi, kama ipo, ambayo bado huelewi vizuri au unahitaji maelezo na/au ufafanuzi zaidi?
  - Je, zana inahitaji marekebisho yoyote kabla ya kuitumia?
- **Kagua shughuli ya kunakili kumbukumbu**
  - Baada ya kupitia zana zote nne na michakato iliyoainishwa hapo juu, ni wakati wa kukagua shughuli ya kunakili kumbukumbu ili kuhakikisha timu nzima inaelewa kile kinachohitajika kutokana na kumbukumbu nzuri na bayana, na kuhakikisha kuwa wanaonakili kumbukumbu wanakubaliana na kujiamini katika majukumu yao. Tumia hati za Mwongozo kwa Wanakili Kumbukumbu ili kusaidia mazungumzo haya, pamoja na mwongozo wa kubainisha mada katika kumbukumbu (angalia Sehemu ya 3. Uchambuzi wa Data, kwa maelezo juu ya hili). Ikiwa kuna muda, huenda ukataka kukagua shughuli ya kunakili kumbukumbu baada ya kufanya mazoezi na angalau moja ya zana na kusahihisha makosa yoyote, ili yasiendelezwe kwa kurudiwa rudiwa.

| | |
|---|---|
| **17:30-18:30** | **Ratiba ya Utekelezaji wa Barometa**<br>(Ratiba iliyokamilishwa, maeneo, vikundi lengwa, nyakati, taratibu za usafiri, shughuli za ukusanyaji wa data, n.k.) |
| **Mwisho wa Siku ya 1** | |

## Siku ya 2

| | |
|---|---|
| **09:00-11:00**<br><br>**Iwapo unaweza kufikia wahudumu wa usalama katika shirika lako au lile unaloshirikiana nalo, hakikisha umewajumuisha kwenye kikao cha usalama ili mkiratibu pamoja.** | **Mazingatio ya usalama na maadili na ulinzi**<br>(Angalia Sehemu ya 1. Mipango na Maandalizi na Tathmini ya Usalama ya Haraka kwa mwongozo na maelezo zaidi kuhusu maeneo haya. Tumia maelezo haya kuelekeza kipindi hiki na timu.)<br>▪ Usiri na Faragha<br>▪ Ulinzi wa data<br>▪ Utoaji idhini<br>▪ Hatari, faida na mazingatio ya usalama<br>▪ Tathmini, taratibu na itifaki za usalama<br>o Hii inahusu kuhakikisha timu inayokusanya data ina fursa ya kujadili tathmini za usalama zilizofanywa; kushiriki katika kuamua utekelezaji ambao ni salama kwao binafsi na kwa wote; na kujua taratibu na itifaki za usalama za utekelezaji wa Barometa, cha kufanya nazo na namna ya kuzitumia katika mazoezi.<br>o Jadili itifaki yako ya usalama na uiendeleze zaidi na timu, huku ukihakikisha kuwa kila mtu anaelewa itifaki na hatua za usalama zilizoandikwa na jinsi zitakavyokaa zikitekelezwa. Inapendekezwa mfanye mazoezi ya itifaki hizi kadri mwezavyo, ili kundi lizikumbuke. Pitia itifaki pamoja nao, ukitoa mifano au matukio ya timu kutafakari ili kuonyesha uelewa wao na mikakati inayoweza kuwekwa.<br>▪ Utambulisho salama na rufaa kwa huduma na usaidizi wakati manusura (wanawake na wasichana kutoka jamii au wafanyakazi wa kike wanaotoa misaada ya kibinadamu) wanafichua hali zao wakati wa utekelezaji wa Barometa. |
| **11: 00-12: 30** | **Wajibu na majukumu ya kila mwanatimu ya Barometa**<br>▪ **Onyesha kila wajibu wa timu na majukumu yake:**<br>o Kiongozi wa Timu<br>o Mratibu<br>o Anayeandika kumbukumbu/ Usaidizi<br>o Mkalimani<br>o Mshughulikia / Msimamizi / Mfanyakazi wa masuala ya UWAKI<br>▪ **Weka majina kwa shughuli katika ratiba ya ukusanyaji wa data:**<br>o Rejelea tena zana na shughuli za kukusanya data.<br>o Jadili ni nani atakayefanya shughuli ipi na upatie shughuli katika ratiba ya kukusanya data majina.<br>▪ Alika timu kujadili haya ili kuhakikisha kila mtu anaelewa majukumu na wajibu wa kila mwanatimu, kazi mahususi katika ratiba na jinsi watakavyofanya kazi pamoja kama timu wakati wa kukusanya data. |

| | |
|---|---|
| **12:30-13:30** | **Mapumziko ya chakula cha mchana** |
| **13:30-15:00** | **Makubaliano ya Kikundi na Kanuni za Maadili**<br><br>Inapaswa kuwa wazi ni nini kila mwanatimu anafanya na wakati anafaa kukifanya (kwa mfano, kutakuwa na wakati ambapo wanatimu wanakaa nje ya FGD au wakati baadhi ya watu wanafanya utafiti wa kuchunguza kwa kuangalia au KII wakati wengine wanafanya majadiliano ya FGD (ilimradi tu kuna wakalimani wa kutosha). Itakuwa muhimu kubuni makubaliano ya timu. Maeneo muhimu ya kujadili na kukubaliana ni:<br>o Nani anafanya nini na lini;<br>o Haja ya kukaa na wanatimu mliowekwa pamoja kila wakati;<br>o Kuripoti masuala au wasiwasi wowote kama yanahusiana na ukusanyaji wa data na/au usalama mara moja—jinsi gani na kwa nani;<br>o Vifaa (ikiwa ni pamoja na vifaa vya huduma ya kwanza na maji katika kila gari, simu za setilaiti zinapohitajika, n.k.);<br>o Kuwasiliana na kukagua kila siku wakati data inakusanywa;<br>o Ratiba za kila siku, nyakati za mapumziko ya chakula cha mchana;<br>o Kumbukumbu na tarehe za kukamilisha;<br>o Kuhakikisha kila mtu ana taarifa zote anazohitaji (namba za simu, n.k.); na<br>o Kukubali kwamba kazi hii inaweza kuwa ngumu na kwamba wanaweza kusikia habari ngumu sana kutoka kwa washiriki-na kuhakikisha wanatimu wanajua wapi pa kwenda na nani wa kumwendea ikiwa wanataka kuzungumza kwa faragha kuhusu kile wanachopitia na kusikia kila siku. Hakikisha kwamba washiriki wa timu wanajua hatua za kuchukua ikiwa watafahamishwa kuhusu kisa cha UWAKI wakati wowote katika majadiliano ya FGD au shughuli nyingine ya kukusanya data.<br><br>Ili kufunga kipindi hiki, ipatie timu nafasi ya kuuliza maswali ili kuhakikisha kwamba kila mtu anaelewa na anahisi kuwa yuko tayari na pia anaelewa kile atakachokuwa akifanya na msaada anaoweza kupata. |
| **15:00-16:00** | **Ukaguzi wa mawasiliano na njia za rufaa za UWAKI**<br>▪ Pitia maelezo ya mawasiliano na njia za sasa za rufaa za UWAKI katika eneo, mahali na maeneo ambayo mtakuwa mnatekeleza Barometa.<br>▪ Jadili jinsi njia hizo zinavyofanya kazi.<br>▪ Eleza jinsi ya kuwaelekeza manusura, wakiwemo wanawake wanaofanya kazi katika hali za dharura, kwa huduma zinazopatikana na zinazofaa za kukabiliana na UWAKI.<br>▪ Shughulikia masuala au maswali yoyote yanayojitokeza (kama vile wasiwasi kuhusu habari kutokuwa sahihi au kuwa zimepitwa na wakati).<br>▪ Hakikisha timu inaelewa kikamilifu maelezo ya mawasiliano na njia zinazopatikana na hawana wasiwasi kuzitumia. Mpe kila mwanatimu nakala za njia na maelezo ya mawasiliano. |

| | |
|---|---|
| **16:00-17:00** | **Ukaguzi wa hati muhimu za kibinadamu**<br>Iwapo umeweza kukusanya hati hizi kabla ya mkutano huu na mmesalia na muda kwenye mkutano, zipitieni pamoja kama timu. Hati hizi zinaweza kujumuisha:<br>▪ Hati za Kikundi Kinachoshughulikia UWAKI: Taratibu za Kawaida za Uendeshaji za shughuli za kukabiliana na UWAKI au Njia za Rufaa kama zinavyopatikana katika eneo la utekelezaji; data iliyokusanywa katika Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za UWAKI (GBVIMS); ukaguzi na tathmini za usalama;<br>▪ Itifaki za tathmini na ripoti za Mtandao wa Kuzuia Unyanyasaji na Dhuluma za Kingono (PSEA), kama zinavyopatikana;<br>▪ Ripoti na tathmini za ushiriki na uwakilishi wa wanawake, kama zinavyopatikana;<br>▪ Ripoti na tathmini za uchambuzi wa jinsia na nguvu, kama zinavyopatikana; na<br>▪ Mipango ya Usaidizi wa Kibinadamu. |
| | **Waambie wanakikundi watafakari, waandike na wajadili:**<br>▪ Taarifa yoyote muhimu kuhusu maeneo ambapo watakuwa wakitekeleza Barometa, kama vile:<br>o Ni sekta gani zilizopo au hazipo; ni usaidizi na huduma gani mahususi zinapatikana, na kwa ajili ya nani, na upungufu wowote katika sekta zote; ni wahusika gani wa kibinadamu wanaofanya kazi huko;<br>o Panapopatikana, ukaguzi wa usalama na uchanganuzi au tathmini za jinsia au UWAKI zinasemaje kuhusu hali ya wanawake na wasichana;<br>o Ni mahitaji na vipaumbele vipi vinavyotambuliwa na au kwa ajili ya wanawake na wasichana;<br>o Je, hali ya sasa ya kazi yoyote inayofanywa na jumuiya ya kibinadamu ya kuzuia udhalilishaji na dhuluma ya kingono, au kazi yoyote ya kushughulikia unyanyasaji wa kingono ikoje; na<br>o Taarifa nyingine ambayo timu inaonelea ni muhimu au inafaa kwa utekelezaji wako wa Barometa. |
| **ASANTENI!**<br>**Mwisho wa mkutano wa kuanza** | |

# Timu ya Barometa ya Sikiliza!

## Hadidu za Rejea (Inafaa kukamilishwa kila wakati kabla ya Utekelezaji)

[Tarehe] ____________________

[Eneo: Nchi/eneo] ____________________

[Shirika/mashirika yanayotekeleza Barometa] ____________________

### Usuli wa Barometa ya Sikiliza!

Barometa ya **Sikiliza!** ni zana ya kupanga na kutathmini inayochunguza hali za wanawake na wasichana ili kubaini kama mazingira ya usaidizi wa kibinadamu katika dharura yanaweza kuzuia, kupunguza na kukabiliana na Ukatili wa Kijinsia, ikiwa ni pamoja na udhalilishaji na dhuluma za kingono, pamoja na unyanyasaji wa kingono. Kipimo cha Barometa kimeundwa ili kubuni tathmini ya haraka ya uwezo na udhaifu wa utoaji usaidizi wa kibinadamu kwa wanawake na wasichana-ikiwa ni pamoja na wale wanaofanya kazi katika dharura za kibinadamu na wale walio katika eneo chanzo la usaidizi wa dharura-kwa madhumuni ya kuandaa mapendekezo kwa ajili ya utetezi. Kinatumia zana na shughuli nne za kukusanya data: Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FGD); Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII); Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia; na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi. Hasa, Barometa inaweza kutumika kama zana ya utetezi-kwa wahusika, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake inayofanya kazi ndani ya na kwa ushirikiano na jumuiya zao, na kwa wahusika wanaoshughulikia UWAKI katika miktadha ya kibinadamu-kuwawajibisha wale wanaohusika na utoaji usaidizi wa kibinadamu kwa wanawake na wasichana.

Barometa ya Sikiliza! iliundwa kulingana na **Nadharia ya Mabadiliko** iliyobuniwa na mashirika ya wanawake na mitandao ya haki za wanawake kutoka eneo la Kusini mwa Dunia na Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (IRC). Ni sehemu moja ya Mradi wa Sikiliza! unaofadhiliwa na Wizara ya Marekani ya Mashauri ya Kigeni , unaolenga kukuza sauti na uwezo wa wanawake na wasichana wakimbizi, na wanawake wanaofanya kazi katika hali za dharura. Lengo lake ni kuchochea mageuzi ya kitaasisi, uchukuaji hatua miongoni mwa mashirika husika na kuongeza rasilimali ili kupunguza ukatili wa kijinsia na udhalilishaji na dhuluma ya kingono katika mazingira ya kibinadamu.

### Timu ya Barometa

Timu yako ya Barometa itakayokusanya data inapaswa kujumuisha **wanawake kutoka ndani ya kikundi, shirika au mtandao wako** na, ikiwa unatekeleza Barometa kwa ushirikiano, **wanawake kutoka shirika unaloshirikiana nalo**. Kwa mashirika yanayoshughulikia UWAKI katika muktadha wa kibinadamu yanayotekeleza Barometa, lazima wanawake kutoka kundi, shirika au mtandao unaoshirikiana nao wawe sehemu ya timu kama viongozi au washirikiane katika kuongoza. Timu ya Barometa inaweza pia kujumuisha **wanawake waliopewa mafunzo kutoka miongoni mwa wenyeji au jumuiya ya wakimbizi** wanaoweza kuongoza vikundi vya FGD; kutumika kama wakalimani wa lugha za wenyeji katika majadiliano na wanawake na wasichana walioathiriwa na majanga; au wasaidie katika utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia. Ni lazima wafunzwe kuhusu dhana za msingi za UWAKI na kanuni zinazomlenga manusura na wajumuishwe katika mkutano wa kuanza unaohusisha timu yako yote ya Barometa.

**Timu ya kukusanya data ya barometa** inapaswa kujumuisha **angalau wanawake wanne** katika majukumu yafuatayo: Kiongozi wa Timu, Mratibu, Mnakili wa kumbukumbu, Mkalimani, na/au Mfanyakazi/Msimamizi/mtoa huduma anayeshughulikia masuala ya UWAKI. Tafadhali tazama hapa chini kwa maelezo zaidi.

## Wajibu na Majukumu

## Timu yote

**Mahitaji muhimu**

- **Timu ya wanawake pekee, ya kukusanya data. Ni salama na inafaa zaidi kwa timu kuwa na wanawake watakaotagusana na wanawake na wasichana katika utekelezaji wa Barometa**. Hii ni pamoja na kuwa na wakusanyaji data wa kike watakaoendesha tafiti za ana kwa ana za mitazamo ya wafanyakazi na vikao vya FGD. Sio tu kwamba hii inatoa safu ya ziada ya usalama kwa wanawake na wasichana, kuna uwezekano mkubwa wa wanawake na wasichana kuzungumza na wanawake wengine juu ya maswala yaliyojadiliwa katika zana husika - hasa wanawake ambao wameteuliwa ipasavyo ili kutekeleza jukumu hilo.
- Lazima kila mwanatimu awe:
    - o Angalau amepokea **mafunzo juu ya dhana kuu za UWAKI, kanuni zinazomlenga manusura na namna ya kuzuia udhalilishaji na dhuluma ya kingono**; na
    - o Ana **kiasi fulani cha uzoefu** katika kushughulikia masuala ya UWAKI na/au kuzuia udhalilishaji na dhuluma za kingono.
- Kila mwanatimu lazima awe **amepata mafunzo ya jinsi ya kutekeleza Barometa.**
- Kila mwanatimu anapaswa kufahamu njia na itifaki za rufaa ya UWAKI zinazopatikana katika eneo husika-kwa jumuiya na wafanyakazi wanaotoa usaidizi-na awe na nakala, zinapopatikana, za matoleo ya hivi karibuni na taarifa zake. **Ikiwa kuna nambari za simu za dharura, zinafaa kujaribiwa kabla ya zoezi la kukusanya data.**
- Kila mwanatimu lazima aelewe na atie saini **Kanuni ya Maadili.**
- **Kuingiza na kurekodi data**: Kila mwanatimu anayeendesha shughuli ya kukusanya data ana wajibu wa kuingiza data na kurekodi kumbukumbu zake mwishoni mwa kila siku ya kukusanya data. Anapaswa kutumia violezo na zana zilizotolewa ili kuingiza data na kuhakikisha kuwa data hii imehifadhiwa katika folda zinazolindwa kwa nenosiri. Mara tu data ghafi inaporekodiwa, lazima kumbukumbu zote ziharibiwe siku hiyo. Nenosiri linapaswa kushirikiwa tu na timu ya Barometa, ikiwa ni pamoja na Kiongozi wa Timu, ambaye atawajibikia data hiyo.

## Wanatimu Binafsi

**Mahitaji muhimu**

**KIONGOZI WA TIMU**

- Angalau mwanamke mmoja katika timu yako anafaa kuongoza na kuratibu mchakato mzima wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data.
- **Mratibu**: Ikiwa hakuna mwanamke mwingine wa kuratibu, Kiongozi wa Timu anaweza pia kuwa Mratibu. Ni muhimu Mratibu awe na ujuzi na uzoefu unaohitajika katika kuendesha mazungumzo na wanawake na wasichana kuhusu masuala ya UWAKI na/au udhalilishaji na dhuluma ya kingono. Ataendesha vikao vya FGD, atahudumu kama mhoji wa vipindi vya KII na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi, na anaweza kufanya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.

**MNAKILI KUMBUKUMBU**

- Mnakili Kumbukumbu ataandika kinachojadiliwa wakati wa vikao vya FGD na KII.
- Mnakili Kumbukumbu pia anaweza kufanya utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia ikiwa ana tajriba ya awali katika kufanya ukaguzi wa usalama.

**MKALIMANI**

- Mtu huyu atakalimani wakati wa vikao vya FGD na KII na lazima awe mtu anayezungumza lugha ya wenyeji. Kama sehemu ya mkutano wa kuanza, hakikisha kwamba Mkalimani anaelewa jinsi ya kukalimani/ kutafsiri kwa usahihi na ipasavyo istilahi kuhusu UWAKI na masuala ya udhalilishaji na dhuluma ya kingono.
- Mkalimani pia anaweza kufanya utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia ikiwa ana tajriba ya awali katika kufanya ukaguzi wa usalama.
- Kimsingi, Mkalimani atashiriki katika shughuli nzima ya kutekeleza Barometa ili kuhakikisha mwambatano; kama hili haliwezekani (kwa mfano, ikiwa lugha nyingi zinazungumzwa katika eneo fulani), kila Mkalimani anapaswa kushiriki katika mafunzo ya Barometa.

**MFANYAKAZI/ MSIMAMIZI / MTOA HUDUMA ZA MASUALA YA UWAKI**

- Lazima mtu huyu awe amefunzwa na ana uzoefu wa kusaidia wanawake na wasichana manusura katika unyanyasaji unaotekelezwa na wanaume (aina zote za UWAKI, zikiwemo unyanyasaji unaotekelezwa na mpenzi na unyanyasaji wa kingono). Lazima aweze kuzingatia kanuni ya usiri wakati wote, kulingana na kanuni elekezi.
- Atatoa usaidizi kwa manusura ambao watafichua walichopitia wakati wa utekelezaji wa Barometa na lazima awepo mwanzoni na mwishoni mwa kila kikao cha FGD ili aweze kujitambulisha na kupokea ufichuzi wowote.
- Lazima awe na uwezo wa kutoa utaalamu na ujuzi juu ya uwezo na upatikanaji wa huduma na rufaa za UWAKI.
- **Muhimu!** Ikiwa hakuna mwanamke kama huyo anayepatikana kutoka katika shirika lako au shirika mnaloshirikiana nalo, angalau, Mratibu anafaa kutenga muda mwanzoni mwa kikao cha FGD na ashiriki habari kuhusu huduma na usaidizi ambao washiriki wanaweza kupata. Kwa mfano, ikiwa kuna nambari ya simu za dharura katika eneo hilo, wapatie nambari hiyo na habari muhimu kuihusu, na jinsi ya kuipata. Iwapo kuna maeneo salama karibu, yanayoaminika na yanayojulikana ya wanawake na wasichana, eleza kikundi mahali yalipo, jinsi ya kuyapata na huduma zinazotolewa huko. Kufanya hivi kunaweza kusaidia kujenga imani kati ya Mratibu na washiriki.

## Ratiba

Timu ya Barometa itafanya kazi kuanzia [tarehe] hadi [tarehe] ili kutekeleza na kukamilisha shughuli zote za ukusanyaji wa data ya Barometa.

# Tathmini ya Usalama ya Haraka

**Muhimu: Zana hii inakusudiwa kutumiwa na timu yako ya Barometa. Maamuzi juu ya kile ambacho ni salama au si salama kwa wanawake lazima ufanywe kwa ushirikiano na wanawake wanaofanya kazi hiyo, pamoja na wanaoangalia usalama au wataalamu wengine wote wanaopatikana.**

**Vyanzo vya habari za usalama vinavyoaminika:** Taarifa za hivi punde za kuaminika kuhusu usalama katika muktadha wako wa kibinadamu kwa kawaida zinaweza kupatikana kutoka kwa waratibu na ripoti za hali zinazotoka kwa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), Waratibu wa Misaada ya Kibinadamu, mihutasari ya usalama ya Idara ya Usalama na Ulinzi ya Umoja wa Mataifa (UNDSS), pamoja na jumuiya ya kibinadamu na wafanyakazi wenza wa kike na wahusika, vikundi na mashirika ya haki za wanawake.

| **Eneo** | | | |
|---|---|---|---|
| Je, eneo hilo linachukuliwa kuwa si salama na vyanzo vya kuaminika vya taarifa za usalama (kwa mfano, OCHA, UNDSS, Mashirika ya Kimataifa Yasiyo ya Serikali ya (INGO) na vituo vya usalama vya Mashirika Yasiyo ya Serikali, vikundi, mashirika na mitandao ya wanawake)? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kuna vikundi vilivyojihami vinavyojulikana kwa sasa kuwa katika au karibu na eneo hilo? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kumekuwa na matukio yoyote ya hivi majuzi ya vurugu (k.m., machafuko ya vurugu, migogoro inayohusisha silaha, utekaji nyara, uvamizi, uporaji, unyanyasaji / mashambulizi ya kingono, n.k.)? (Chukulia "hivi majuzi" kama kipindi cha wiki iliyopita, kukiwa na utulivu kiasi katika mwezi uliopita, isipokuwa ushauriwe vinginevyo na vyanzo vya usalama vinavyoaminika). | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kuna ripoti za kuongezeka kwa machafuko na mvutano mkali baada ya kipindi husika cha utulivu? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kuna ripoti za uwezekano wa vurugu au ukosefu wa usalama kutokea sasa au hivi karibuni? | Ndiyo | La | Sijui |
| **Safari na njia** | | | |
| Je, eneo hilo ni ngumu kufika (kwenda pale NA kutokana na sababu za usalama)? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, eneo hilo linachukuliwa kuwa salama lakini ni ngumu sana kufika pale? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kuna njia salama na zinazopatikana za usafiri za kufika pale? (Fikiria: Utafika pale vipi na kwa mbinu ipi ya usafiri) | La | Ndiyo | Sijui |
| Je, mvua/ hali mbaya ya hewa itaathiri uwezo wako wa kufika kwenye eneo lengwa, au mvua/ hali mbaya ya hewa inaweza kusababisha kukwama hapo au barabarani? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, utaweza kusafiri na magari mawili kwenye msafara kwa usalama zaidi? Je, unaweza kusafiri kwa msafara na wahusika wengine wa kibinadamu hadi eneo hilo ili kutoa usalama zaidi? (Hili sio muhimu, lakini linaweza kushauriwa na wahusika wa usalama). | Hapana | La | Sijui |
| Je, njia ya kufika huko na kurudi ni salama? (Fikiria: Je, kuna hatari zozote zinazojulikana kwenye njia hiyo (k.m., wahusika wenye silaha, vikundi vinavyoendeleza vurugu, migodi, vituo tete vya ukaguzi, kuvuka mipaka ya upinzani/ serikali, n.k.?) | La | Ndiyo | Sijui |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ukizingatia wanatimu wenzako, je, kuna madhara yoyote ya kiafya yanayoweza kuwapata kutokana na kusafiri huko, au kuwa huko? (Zingatia barabara au miundombinu mibovu/hatari, kama vile madaraja, milipuko ya magonjwa ambukizi, n.k.) | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, itakuchukua siku moja au zaidi kusafiri huko? (Fikiria: Ingechukua muda gani kusafiri kwenda huko na kurudi? Je, umbali mrefu utaathiri vipi idadi ya maeneo unayoweza kufika katika wiki mbili? Huenda pia ikaongeza wasiwasi wa usalama ikiwa itabidi usafiri mbali kiasi hicho.) | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kuna njia mbadala za kuondoka mahali pale ambazo ni tofauti na ulizotumia kufika pale? (Fikiria: Katika maeneo ambayo huenda kukawa na matatizo ya usalama, kuwa na njia mbadala ni mkakati muhimu wa kujilinda iwapo njia moja itafungwa). | La | Ndiyo | Sijui |
| **Mawasiliano** | | | |
| Je, simu yako itakuwa na mtandao katika eneo hilo? (Fikiria: Je, mawasiliano yatakuwaje mahali hapo? Eneo lisilo na mtandao wa simu linapaswa kuchukuliwa kuwa tatizo la usalama. Fikiria chaguo zingine, kama vile simu za redio au satelaiti.) | La | Ndiyo | Sijui |
| Je, utaweza kupata umeme/stima ya kuchaji vifaa vyako vya mawasiliano, au kupata betri za ziada zenye chaji utakazobeba? | La | Ndiyo | Sijui |
| Je, kuna wahusika wakuu wa usalama na/au uratibu, kama vile UNDSS au OCHA, ambao unaweza kuwaita katika dharura? Ikiwa wapo, unaweza kupata nambari zao? Ikiwa sivyo, kuna wahusika wengine salama na wanaoaminika ambao wanaweza kutoa usaidizi wa usalama katika tukio la dharura? | La | Ndiyo | Sijui |
| **Malazi** | | | |
| Je, utahitaji kulala mahali hapo? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, ni salama kukaa mahali hapo usiku kucha? | La | Ndiyo | Sijui |
| Je, kuna maeneo salama ya wanawake kukaa usiku? | La | Ndiyo | Sijui |
| Je, kuna wahusika wengine wa kibinadamu ambao hulala huko? (Fikiria mahali wanapokaa na kama unaweza kufikia nafasi hizo ikiwa unaziona kuwa salama kwa wanawake (k.m., nyumba ya wageni, hoteli, kambi, kituo cha Umoja wa Mataifa, n.k.) | La | Ndiyo | Sijui |
| **Timu ya Barometa, shirika lako na unaoshirikiana nao** | | | |
| Je, timu yako inajihisi salama na kuridhishwa na chaguo zinazopatikana za mahali pa kulala kwenye eneo hilo? Je, wanaweza kulala usiku kucha, tukizingatia majukumu mengine ambayo wanaweza kuwa nayo nyumbani? | La | Ndiyo | Sijui |
| Je, wanawake katika timu yako wanajihisi salama kusafiri kwenda/kutoka eneo hilo? | La | Ndiyo | Sijui |
| Je, wanawake katika timu yako wanajihisi salama katika eneo hilo? | La | Ndiyo | Sijui |

**Unaweza kutumia zana hii kwa madhumuni yafuatayo:**

- Kutathmini kwa haraka usalama wa maeneo ambapo Barometa inaweza kutekelezwa;
- Kujadiliana na timu zako kuhusu kila mahali na eneo ambapo kipimo cha Barometa kinaweza kutekelezwa ili kuwasaidia katika kufanya maamuzi yao wenyewe kuhusu kama wana wasiwasi wowote kuhusiana na kusafiri wao binafsi na kwa pamoja hadi eneo husika; na
- Ili kukusaidia uendelee kutathmini usalama wa maeneo unayochagua wakati wa utekelezaji.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Je, kuna vikundi fulani (k.m., watu kutoka taifa, kabila, mbari, ukoo, dini fulani, n.k.) ambavyo havitakuwa salama kuwa mahali pale au kusafiri kwenye njia hiyo? (Ikiwa jibu ni "ndiyo" kwa mtu yeyote kwenye timu yako, eneo hilo si salama). | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kutakuwa na athari zozote mbaya au upinzani dhidi yako, timu yako, shirika lako, mashirika mnayoshirikiana nayo, au familia, ukisafiri kwenda au kutoka eneo hilo? | Ndiyo | La | Sijui |
| Je, kutakuwa na athari zozote mbaya au upinzani dhidi yako, timu yako, shirika lako, mashirika unayoshirikiana nayo, au familia, ukitembelea na kukaa katika eneo hilo? | Ndiyo | La | Sijui |

| **Ikiwezekana (hiari): Waulize wafanyakazi wengine wa kike wanaotoa usaidizi wa kibinadamu au wanaharakati wa haki za wanawake ambao wameishi na kufanya kazi kwenye eneo hili karibuni au hivi sasa. (Jitahidi kuuliza wafanyakazi mbalimbali wa kike wa eneo hilo, wa kitaifa na kimataifa, kwani uzoefu na mitazamo yao inaweza kutofautiana).** | | | |
|---|---|---|---|
| Je, ni salama kwa wanawake kukaa usiku kucha/kuishi huko? | La | Ndiyo | |
| Je, ni salama kwa wanawake kuwa huko na kufanya kazi huko wakati wa mchana? | La | Ndiyo | |
| Je, ni salama kwa wanawake kusafiri kwenda au kutoka huko? | La | Ndiyo | |
| Je, maoni yako ya jumla ya eneo hilo ni yapi kukija ni usalama na kusafiri kwenda au kutoka mahali hapo? | | | |

## Mwongozo

Ikiwa umechagua jibu lenye rangi NYEKUNDU katika swali MOJA au ZAIDI, hili linapaswa kuchukuliwa kuwa tatizo kubwa la usalama na unapaswa kuzingatia KUTOFANYA shughuli zako katika eneo hilo.

Ondoa eneo lolote ambalo lina jibu MOJA au ZAIDI lenye rangi NYEKUNDU. Huenda maeneo haya si salama hata kidogo, hayawezi kutabiriki na ni tete kwa utekelezaji wa Barometa.

Ikiwa umechagua jibu lenye rangi ya CHUNGWA katika swali MOJA au ZAIDI, na HUWEZI kupata taarifa zaidi zinazothibitisha eneo hilo ni salama vya kutosha, inashauriwa uegemee upande wa tahadhari na uchague eneo tofauti.

Ikiwa umechagua jibu lenye rangi NYEUSI katika swali MOJA au ZAIDI na HUNA swali lolote lilila na jibu lenye rangi NYEKUNDU, hili halimaanishi kuwa eneo si salama. Lakini utahitaji kufikiria jinsi ya kushughulikia suala ambalo lilipata rangi nyeusi, au ufikirie kile unachoweza kufanya ili kupunguza au kuepuka suala hilo, na uwe huna wasiwasi na una imani na suluhisho lililofikiwa.

Ikiwa umechagua jibu lenye rangi NYEUSI katika swali MOJA au ZAIDI NA una jibu lenye rangi NYEKUNDU katika swali lolote kati ya haya, hili linafaa kuchukuliwa kuwa tatizo kubwa la usalama na unapaswa kuzingatia KUTOFANYA shughuli yako katika eneo hilo.

Rangi ya KIJANI inaonyesha kuwa eneo linaweza kuwa salama vya kutosha kutekeleza utafiti wa Barometa.

MUHIMU: Hii ni tathmini msingi, ya haraka ya usalama na haiwezi kukuhakikishia usalama au kukupa taswira kamili. Wewe na mshirika wako wa Barometa lazima mhakikishe kuwa mna habari za kutosha na za hivi punde zaidi kuhusu hali ya usalama katika eneo hilo kwani hali inaweza kubadilika haraka. Wasiliana na wahusika wanaoratibu misaada ya kibinadamu (OCHA) na wahusika wa usalama (UNDSS, vituo vya usalama vya kibinadamu).

Unapaswa kuweka hatua zote muhimu za usalama kwa safari yako, zikiwemo:

- Kuhakikisha wanatimu yako wanasafiri wakiwa wawili au zaidi (yeyote ASISAFIRI peke yako), wametoa idhini yao ya kusafiri hadi eneo hilo, mmoja mmoja na kwa pamoja wamekubali kwamba wako radhi kwenda na kuelewa hatari zozote zinazoweza kutokea;
- Usafiri wa kutosha, salama na wa kutegemewa, na kusafiri na dereva anayejulikana na anayeaminika (ikiwa unaenda kwa gari/chombo);
- Njia za kutosha za mawasiliano na nambari muhimu za mawasiliano;
- Malazi ya kutosha na salama kwa wanawake (ikiwa wanalala huko);
- Upatikanaji wa taarifa za sasa, za kuaminika za usalama kuhusu eneo kutoka kwa vyanzo vinavyoaminika (OCHA, UNDSS, INGO/NGO, mashirika, vikundi, mitandao ya wanawake); na taarifa za hivi punde siku ya kusafiri na ukiwa katika eneo husika;
- Mipango iwe imewekwa ikiwa unahitaji kuondoka mahali hapo kwa haraka, iwapo kuna mabadiliko/kuzorota kwa usalama. (Hii ni pamoja na kuhakikisha unajua njia za kutumia kuondoka eneo hilo na kuwa umetambua njia tofauti au mbadala); na
- Kuwa umetambua angalau eneo lingine 1 au 2 kama maeneo mbadala ikiwa hutaweza kufikia mojawapo ya maeneo uliyochagua kutokana na mabadiliko ya usalama.

Daima kumbuka kwamba faida za kuchagua eneo mahususi lazima ziwe nyingi kuliko hatari. Ikiwa huna uhakika au bado una wasiwasi kuhusu usalama wa eneo, unaweza kuchagua eneo tofauti.

# Ratiba ya wiki 2 ya Utekelezaji wa Barometa ya Sikiliza! (mfano)

**Kumbuka:** Huu ni mfano wa ratiba ya wiki ya 2 ya utekelezaji wa Barometa kwa ajili ya ukusanyaji data iliyoundwa kwa ajili ya timu ya Barometa isiyopungua watu wanne, ambayo unaweza kurekebisha kulingana na mahitaji yako. Ratiba yako itategemea muktadha wako, vipaumbele, rasilimali, ahadi nyingine, n.k. Ikiwa una timu kubwa zaidi, utaweza kufanya shughuli za ukusanyaji wa data kwa sambamba. Jaribu kukusanya **maoni ya waliojibu** unapoenda au upange kuyakusanya baadaye lakini kabla ya shughuli yako ya kukusanya data kukamilika.

| Tarehe | Saa | Mahali | Shughuli | Wanakikundi/ majukumu) | Maoni / Usafiri |
|---|---|---|---|---|---|
| Siku ya 1 | [Alasiri] | [Mji/ Jiji/ Eneo] | Kukusanya timu yako ya Barometa mahali mnafaa kuanzia | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | [Inaweza kujumuisha mipango ya usafiri] |
| Siku ya 2 | Simu nzima: 9:00 – 17:00 | [Ofisi/ Sehemu ya Mkutano] | Mkutano wa kuanza na timu ya Barometa (Siku ya 1) | Timu yote ya Barometa | [Inaweza kujumuisha rasilimali/vitu mtakavyohitaji, chakula n.k.] |
| Siku ya 3 | Simu nzima: 9:00 – 17:00 | [Ofisi/ Sehemu ya Mkutano] | Mkutano wa kuanza na timu ya Barometa (Siku ya 2) | Timu yote ya Barometa | [Inaweza kujumuisha rasilimali/vitu mtakavyohitaji, chakula n.k.] |
| Siku ya 4 | Asubuhi | “Kambi ya 1” | Ukusanyaji data:<br>Kikao cha FGD na wanawake (wakimbizi) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | [Inaweza kujumuisha maelezo ya usafiri au usafirishaji] |
| | Alasiri | “Kambi ya 1” | Ukusanyaji data:<br>Kikao cha FGD na wasichana (wakimbizi) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | [Inaweza kujumuisha rasilimali/ vitu vyovyote mtakavyohitaji] |
| Siku ya 5 | Asubuhi | “Kambi ya 1” | Ukusanyaji data:<br>Kikao cha FGD na wanawake (wakimbizi wa ndani) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | Alasiri | “Kambi ya 1” | Ukusanyaji data:<br>Kikao cha FGD na wasichana (wakimbizi wa ndani) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 4pm | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 6 | Asubuhi | "Kambi ya 1" | Ukusanyaji data:<br>Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | Alasiri | "Kambi ya 1" | Ukusanyaji data:<br>Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia (kuendelea) | | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 7 | Asubuhi | "Kambi ya 1" | Ukusanyaji data:<br>Utafiti wa Mitazamo ya Wafanyakazi | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | Alasiri | "Kambi ya 1" | Ukusanyaji data:<br>Utafiti wa Mitazamo ya Wafanyakazi | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 8 | Asubuhi | "Kambi ya 2" | Ukusanyaji data:<br>Kikao cha FGD na wanawake (wakimbizi wa ndani) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | Alasiri | "Kambi ya 2" | Ukusanyaji data:<br>Kikao cha FGD na wasichana (wakimbizi wa ndani) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 9 | Asubuhi | "Kambi ya 2" | Ukusanyaji data:<br>Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | Alasiri | "Kambi ya 2" | Ukusanyaji data:<br>Utafiti wa Mitazamo ya Wafanyakazi | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Siku ya 10 | Asubuhi | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: vikao vya KII na "kikundi A cha wanawake" | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | Alasiri | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: vikao vya KII na "kikundi B cha wanawake" | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 11 | Asubuhi | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Kikao cha FGD na wanawake (wenyeji) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | Alasiri | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Kikao cha FGD na wasichana (wenyeji) | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 12 | Asubuhi | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Kikao cha FGD na wanawake (wakimbizi wa ndani) | | |
| | Alasiri | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Kikao cha FGD na wasichana (wakimbizi wa ndani) | | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 13 | Asubuhi | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia | | |
| | Alasiri | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia (kuendelea) | | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Siku ya 14 | Asubuhi | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Utafiti wa Mitazamo ya Wafanyakazi | | |
| | Alasiri | "Mji wa 1" | Ukusanyaji data: Utafiti wa Mitazamo ya Wafanyakazi | | |
| | | Makao makuu | Kusafisha na kurekodi data; kikao cha kuhoji; kujitayarisha kwa ajili ya siku inayofuata | [Majina, nyadhifa/ majukumu] | |
| Siku ya 15 | Siku nzima: 9:00 – 17:00 | [Ofisi/ Sehemu ya Mkutano] | Kikao cha kuhoji kuhusu ukusanyaji data, kuhakikisha hati zote kutoka kwenye zana ziko sawa (FGD, KII, Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia, Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi, Maoni ya Waliohojiwa) | Timu yote ya Barometa | [Inaweza kujumuisha rasilimali/ vitu vyovyote mtakavyohitaji] |
| Siku ya 16 | Siku nzima | [Mji/ Jiji/ Eneo] | Timu kuondoka | | [Inaweza kujumuisha mipango ya usafiri] |

Sehemu ya 2

# Utekelezaji



Picha na A Brenner, IRC

# Mazingatio ya kimaadili na usalama kwa ukusanyaji wa data nyeti

**Mazingatio ya maadili na usalama** yaliyojadiliwa katika mwongozo huu yanalingana na viwango vya kimataifa na lazima yafuatwe kikamilifu katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa data na zaidi. Kufuata viwango hivi ni muhimu sana wakati wa kuzungumza na wanawake na wasichana kuhusu UWAKI, unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono.

Mazingatio haya yanafafanuliwa na:

- Kanuni ya msingi ya **Usidhuru**, na kanuni muhimu za **usalama, usiri na utu,** ambazo lazima zifuatwe wakati wote wa kukusanya data juu ya UWAKI, unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono. Mambo muhimu ya kuzingatia ni pamoja na:
    - **Usiri na Faragha**
    - **Ulinzi wa data**
    - **Utoaji idhini**
    - **Hatari, faida na mazingatio ya usalama**

Katika utekelezaji, lazima yafuatayo yazingatiwe:

## Usiri na Faragha

**Usiri na faragha ya wote waliojibu na walioshiriki katika ukusanyaji wa data lazima iheshimiwe na ilindwe kila wakati.** Mambo yafuatayo hayawezi kufanyika katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa data:

- Picha, rekodi za sauti au video za yeyote kati ya waliohojiwa au walioshiriki hazipaswi kunaswa. **Utafiti huu wa Barometa hauhitaji rekodi za picha, sauti au video za data yoyote.** Kumbukumbu zote za Mahojiano ya Kikundi Lengwa (FGD) na Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII) lazima zinakiliwe kwa maandishi tu na anayeziandika/wakusanyaji wa data, na baada ya kupata **idhini wazi** kutoka kwa washiriki wa FGD na KII (angalia sehemu ya *Utoaji Idhini baada ya Kufahamishwa* hapa chini).
- **Data yote—iwe kutoka kwa uchunguzi kwa kutazama, vikao vya FGD, KII au Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi—lazima ikusanywe bila kuwatambulisha washiriki. Majina au taarifa yoyote inayoweza kuwatambulisha wahojiwa na washiriki haifai kamwe kukusanywa kama sehemu ya Barometa.** Taarifa hii haihitajiki ili kufikia malengo ya Barometa.

## Ulinzi wa data

Data yote iliyokusanywa kama sehemu ya Barometa lazima ilindwe. Lazima data yote iliyokusanywa katika vikao vya FGD, KII, Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi na Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia ilindwe kila mwisho wa siku inapokusanywa:

- Kila siku, mshiriki mmoja au wawili pekee wa timu ya Barometa wanapaswa kuteuliwa washikilie na walinde data siku nzima.
- Mwishoni mwa kila siku, wanatimu hao lazima waingize data kwenye laha ya Excel inayolindwa kwa nenosiri.
- Pindi data inapowekwa kwenye faili iliyolindwa kwa nenosiri, **lazima ufute na uharibu kumbukumbu na laha**

**zote za data za karatasi kabla ya kumaliza kila siku**.

- Hifadhi faili ya Excel kwenye folda au hifadhi iliyolindwa kwa nenosiri.
- Hakuna data (ikiwemo ile ambayo haimtambulishi mhojiwa) inayopaswa kushirikiwa na yeyote nje ya wanatimu walioteuliwa wa Barometa.

# Utoaji idhini baada ya Kufahamishwa

**Idhini ni makubaliano ya hiari ya mtu binafsi** ambaye ana ukomavu na uwezo unaokubalika kisheria (miaka 18 na zaidi) wa kujitoa idhini. Kwa vijana/wale walio chini ya umri wa miaka 18, tafadhali fuata utaratibu wa kupata idhini au kibali kama ilivyoainishwa katika miongozo ya kimataifa.[23] Mtu yeyote anayetumia Barometa ana **wajibu wa kimaadili wa kuhakikisha kuwa idhini imepatikana *nyakati* zote**. Ili washiriki wanaotarajiwa waweze kufanya uamuzi wakiwa na maelezo ya kutosha na kwa busara kuhusu kama wanataka au hawataki kushiriki, ni lazima wapokee taarifa nyingi iwezekanavyo, kwa njia iliyo wazi na wanayoielewa, kuhusu maelezo ya kushiriki (yaani FGD, KII, Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi).

**Lazima utoaji idhini baada ya kufahamishwa utazamwe kama mchakato, wala sio kama shughuli ya mara moja pekee.** Lazima idhini itolewe kabla ya kuanza shughuli zozote na washiriki za kukusanya data. Hakikisha kuwa washiriki waliotoa idhini wanaelewa kila mara kuwa wana chaguo la kujiondoa wakati wowote katika mchakato wote bila athari wala maswali yoyote. Ni muhimu kwamba washiriki wajue wana haki ya kushiriki au kutoshiriki, njia ya kushiriki, na kwa muda gani, na wanaweza kuacha au kubatilisha ushiriki wao wakati wowote. Kamwe mtu anayeweza kushiriki asishinikizwe kukubali au kuendelea kushiriki. Sambamba na kanuni elekezi za UWAKI, utoaji idhini ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa utafiti wa Barometa katika kutambua haki, wakala na matakwa ya kimsingi ya washiriki katika kujiamulia matendo yao wenyewe kulingana na mahitaji yao, matakwa na vipaumbele vyao.

**Kwa vikao vya FGD na KII:** Idhini inayotolewa kwa mdomo (au mchakato wa idhini/kibali kwa walio chini ya umri wa miaka 18)[24] lazima itolewe na washiriki wote kabla ya kukusanya data katika vikao vya FGD na KII. Washiriki wote wanaotarajiwa lazima wafahamishwe:

- Kuhusu wewe ni nani na unafanya kazi na shirika lipi;
- Kuhusu madhumuni ya FGD/KII, aina ya maswali yatakayoulizwa, sababu za kuyauliza na utakayofanya na taarifa ambayo watashiriki;
- Kuhusu kitakachotokea wakati na baada ya vikao vya FGD/KII;
- Kuhusu hatari na faida za kushiriki zinazoweza kutokea;
- Kuhusu jukumu la wanakili kumbukumbu, kwa nini kumbukumbu zinanakiliwa na zitafanyiwa nini baada ya vikao vya FGD/KII;
- Kwamba kushiriki ni kwa hiari na uamuzi wao wa kushiriki au kutoshiriki hautaathiri kwa njia yoyote huduma na usaidizi wanaopokea na ambao wanastahili;
- Kwamba wana haki ya kukataa kujibu maswali yoyote au kuondoka kwenye vikao vya FGD/KII wakati wowote; na
- Kwamba mchakato huo ni wa siri na hautawatambulisha.

Ukishapitia mambo hayo, waulize kama wana maswali yoyote. Hakikisha kuwa maswali yote yamejibiwa kikamilifu na uangalie tena ili uhakikishe kuwa hakuna chochote kitakachoachwa bila kujibiwa.

Ni muhimu sana kwamba hili lifafanuliwe kwa lugha na njia ambayo washiriki wanaielewa. Lazima wanatimu wanaosimamia vikao vya FGD/KII wawaulize tena washiriki ili kuhakikisha wanaelewa na wanapewa fursa ya kuuliza maswali yoyote, kabla ya kukubali. Ikiwa yeyote kati ya washiriki atauliza maswali, hakikisha kuwa maswali haya yamejibiwa na kufafanuliwa vya njia inayoridhisha washiriki.

23 Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, *"Mwongozo wa UNHCR wa Kuamua Maslahi Bora ya Mtoto"* (2008): https://www.unhcr.org/4566b16b2.pdf; IRC, UNICEF, *"Mwongozo wa Kutunza Watoto Walionusurika"* (2012): https://www.unicef.org/documents/caring-child-survivors-sexual-abuse; Kamati ya Kudumu ya Mashirika ya Kimataifa (IASC), *"Mwongozo wa Mashirika Mbalimbali wa Usimamizi wa Visa na Ulinzi wa Watoto"* (2014): http://www.cpcnetwork.org/wp-content/uploads/2014/08/CM_guidelines_ENG_.pdf.

24 Kama hapo juu

- *Tazama sehemu ya Viambatisho  ili uone Karatasi ya Barometa ya Taarifa ya Mshiriki na fomu ya Kutoa Idhini:*

- **Karatasi ya Barometa ya Taarifa ya Mshiriki** kwa ajili ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi ya kuwapatia wafanyakazi ambao huenda wakashiriki ili kuwasaidia katika kufanya uamuzi wenye burasa kuhusu kushiriki au kutoshiriki katika utafiti; na
- Sampuli ya **Fomu ya Kutoa Idhini.**

# Hatari, faida na mazingatio ya usalama

**Lazima manufaa ya kukusanya data kwa kipimo hiki yazidi hatari kwa wahojiwa, jamii zao na timu inayokusanya data ya Barometa** (na wale wanaohusishwa na wanatimu na mashirika yao). Ikiwa madhara yatakuwa makubwa kuliko faida, data haifai kuanza kukusanywa, na unapaswa kufikiria upya mahali ambapo utafiti huu wa Barometa unaweza kufanyika. Usalama na ulinzi wa wale wote wanaohusika katika ukusanyaji wa data lazima upewe kipaumbele.

**Kutathmini usalama na kuzuia au kupunguza hatari si shughuli za mara moja. Usalama lazima ufuatiliwe na kutathminiwa kila wakati** katika kipindi cha ukusanyaji wa data; hakikisha kuwa shughuli na ratiba zote za ukusanyaji wa data zinarekebishwa ili kupatia usalama na ulinzi wa wote wanaohusika kipaumbele kila wakati. **Lazima tathmini, taratibu na itifaki za kutosha za usalama ziwepo** ili kuzuia na kupunguza hatari na kuhakikisha kuwa hakuna hatari zisizo za lazima kwa wote wanaohusika. Pia kuwe na kituo au timu ya usalama iliyoteuliwa na iliyopewa mafunzo, iliyotengewa timu ya kukusanya data ya Barometa.

Kwa maelezo zaidi juu ya kutathmini usalama, rejelea tena *Tathmini ya Usalama ya Haraka* upate zana ya Tathmini ya Usalama ya Haraka inayolenga wanawake na vigezo vya usalama vya kuzingatia wakati wa kuchagua eneo na washiriki katika *Sehemu ya 1. Mipango na Maandalizi*.

# Muhtasari wa zana za kukusanya data na jinsi ya kuzitumia

Utafiti wa Barometa unajumuisha zana nne za kukusanya data, ambazo zinaweza kupatikana katika *Viambatisho : Zana za Kukusanya Data.*

## Zana za Kukusanya Data

**1. Majadiliano ya Vikundi (FGD)**

Wanawake na wasichana

**2. Kuchunguza kwa Kuangalia**

Wanawake na wasichana

Wafanya kazi wakibinadamu (wanawake na wana ume)

**3. Utafiti wa Mitazamoya Wafanya kazi**

Wafanya kazi wakib-inadamu (wanawake na wanaume)

**4. Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII)**

Wahusika, makundi, mashirika na mitanda oyakibinadamu inayo fanyakazi katika na pamoja na jamii

### Majadiliano ya Kikundi Lengwa

- Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Dokezo la Mwongozo
- Zana ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Wasichana walio balehe
- Zana ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Wanawake
- Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD): Kiolezo cha Kumbukumbu
- Mwongozo kwa Wanaonakili kumbukumbu

Majadiliano ya Kikundi Lengwa ni njia muhimu ya kukusanya taarifa tele na za kina ambazo huenda zisipatikane kwa urahisi kwa kutumia zana za kawaida za kukusanya zinazozingatia kiasi na idadi. Matokeo ya vikao vya FGD yanaweza kutumiwa kuunga mkono au kurekebisha alama za zana ya uchunguzi kulingana na yale wahojiwa wanayosema. Tazama mwongozo zaidi katika *Sehemu ya 3. Mwongozo* wa Uchambuzi wa Data kuhusu jinsi ya kutumia uchanganuzi wa FGD katika ripoti ya jumla ya Barometa.

**Mfano mmoja:** Ikiwa Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia unasema kuwa wanawake wanaweza kupata huduma, lakini wanawake katika vikao vya FGD wanasema kwamba hawataenda kupata huduma hiyo kwa sababu hawaiamini, suala hili linaongeza maelezo muhimu kwenye matokeo ya uchunguzi.

Ni muhimu kujaribu kushirikisha wanawake na wasichana mbalimbali katika vikao vya FGD ambao wanaweza kuzungumza kuhusu masuala tofauti yanayoathiri wanawake na wasichana katika muktadha wa kibinadamu. Si lazima kila mmoja awe "amewakilishwa" na kuna uwezekano mkubwa kwamba jambo hili haliwezekani kwa kuwa matokeo hayatachanganuliwa rasmi kitakwimu.

Hata hivyo, **kuwa na kikundi kinachowakilisha sauti anuai za wanawake na wasichana kutaruhusu ukusanyaji wa taarifa bora na uelewa wa kina zaidi wa hali, uzoefu wa maisha na wasiwasi wa usalama wa wanawake na wasichana**. Uanuai unaweza kujumuisha umri, ulemavu, kabila, dini, eneo ndani ya muktadha unaotathminiwa, na kadhalika. Ambapo wahusika wa LGBTQI (wasagaji, mashoga, wanaoshiriki ngono na watu wa jinsia zote mbili, waliobadili jinsia, watu wa jinsia tofauti) wanahamasisha wanawake na washichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia mara kwa mara na kwa usalama, majadiliano ya kikundi (FGD) yanaweza kufanywa na watu wa kundi hili.

Kila kikundi cha FGD kinapaswa kujumuisha **washiriki wasiozidi wanane wa umri na asili sawa**-kwa mfano: kundi moja la wanawake wakimbizi, kundi moja la wasichana kutoka miongoni mwa wenyeji.

**Kumbuka:** Baadhi ya vijisehemu vidogo na maswali huenda yasitumike katika baadhi ya miktadha kulingana na kiwango na mawanda wa usaidizi uliopo wa kibinadamu. Kwa mfano, katika baadhi ya miktadha, ugawaji wa vifaa vya heshima unaweza kuwa haujafanywa, jambo ambalo ni kigezo cha utetezi.

- *Angalia Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Dokezo la Mwongozo kwa taarifa zaidi.*

# Mahojiano ya watoa taarifa muhimu

- Zana za Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu
- Kiolezo cha Kumbukumbu za Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII)
- Mwongozo kwa Wanaonakili kumbukumbu

Zana ya KII imeundwa ili kuongoza mahojiano ya watoa taarifa muhimu yatakayofanywa na wahusika wa vikundi na mitandao ya haki za wanawake inayofanya kazi katika, na pamoja na, jumuiya zao kama sehemu ya ukusanyaji wa data wa Barometa. Madhumuni ya mahojiano ni kuelewa, kwa kuzingatia mitazamo ya wanawake hawa mambo yafuatayo:

- Iwapo wamehusika na/au kushiriki katika utoaji usaidizi wa kibinadamu katika eneo walimo;
- Kama usaidizi wa kibinadamu unakidhi mahitaji ya wanawake na wasichana; na
- Ni mabadiliko gani wangependa kuona katika mfumo wa kibinadamu katika siku zijazo.

Inapendekezwa ufanye hivi na **mtu mmoja au kikundi kidogo cha hadi wanawake watatu** kutoka kwa kikundi, shirika au mtandao sawa; kuwa na zaidi ya watatu kunaweza kusababisha mazungumzo yasiyo na kina au umakini.

# Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia

- Zana ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia

**Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia** unachambua kwa kina maeneo yanayoonekana ya usaidizi wa kibinadamu. Kila swali kwenye orodha linaweza kujibiwa kwa kuchunguza na kukagua hati zinazopatikana na/au kuangalia maeneo hayo mwenyewe. Zana hii haishughulikii viashirio vinavyohitaji uthibitisho kupitia mawasiliano ya moja kwa moja na wadau, isipokuwa maswali kadhaa ambayo yanahitaji kuulizwa mtoa huduma ili kubainisha—ikiwa anapatikana na ako tayari kujibu.

**Muhimu:** Ukaguzi huu wa hati HAUHITAJI kutazama hati za ndani za shirika. Hati pekee za kukaguliwa ni zile zinazokusudiwa kutolewa nje na zipatikane hadharani kwa manufaa ya jumuiya nzima ya kibinadamu.

Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia unalenga kuchunguza maeneo mawili makuu ya usaidizi wa kibinadamu yenye maeneo maalum ya kutathmini:

- **Ukaguzi wa hati: Mbinu za Kuzuia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono na Sera za Usalama**
    - Ahadi za jumuiya ya kibinadamu katika kushughulikia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono
    - Mitandao ya Kuzuia Unyanyasaji na Dhuluma za Kingono (PSEA)
    - Mbinu na Utaratibu wa Malalamiko ya Kijamii (CBCM)
    - Ufikiaji wa CBCM
    - Maeneo salama kwa wanawake na wasichana
    - Rufaa zinazopatikana kwa jamii
    - Ukaguzi wa usalama
- **Uchunguzi wa eneo: Mazingira ya Usaidizi wa Kibinadamu**
    - Kuzuia na kupunguza UWAKI
    - Maeneo salama kwa wanawake na wasichana
    - Huduma ya afya
    - Huduma za lishe

**Ili kukamilisha sehemu ya ukaguzi wa hati ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia**, timu ya Barometa inapaswa kupata na kukagua hati zifuatazo, ikiwa zipo:

1. Hati za Timu ya PSEA (zinazopatikana kupitia Timu ya PSEA au mtandao/ wakala anayeongoza)
    a. Masharti ya Marejeleo
    b. Taratibu za Kawaida za Uendeshaji
    c. Kumbukumbu za mkutano mitatu ya hivi karibuni ya Timu ya PSEA
2. Mpango wa hivi majuzi zaidi wa Usaidizi wa Kibinadamu
3. Utaratibu wa Kuripoti wa Mashirika mbalimbali (unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono)
4. Orodha ya Viini vya Unyanyasaji wa Ngono kwa kila wakala/eneo
5. Orodha ya Viini vya Udhalilishaji na Dhuluma ya Kingono kwa kila wakala/eneo
6. Njia ya Rufaa (katika maeneo lengwa, sio tu njia za rufaa za kitaifa)
7. Taratibu za Kawaida za Uendeshaji za CBCM
8. Taratibu za Kawaida za Uendeshaji za UWAKI (zinapatikana kupitia nguzo ndogo ya UWAKI)
9. Ripoti za ukaguzi wa usalama au hati nyingine zinazohusiana (zinapatikana kupitia nguzo ndogo ya UWAKI)

**Ili kukamilisha sehemu ya uchunguzi wa eneo ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia**, tembelea mahali na maeneo uliyochagua, na uangalie usaidizi wa kibinadamu hapo.

# Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi

- **Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi:** Dokezo la Mwongozo
- **Zana ya Uchunguzi wa Mtazamo wa Wafanyakazi:** Kwa tafiti za ana kwa ana (Hati ya Word)
- **Zana ya Uchunguzi wa Mtazamo wa Wafanyakazi:** Kwa tafiti za mtandaoni (hati ya Excel)
- **Mwongozo wa Hatua kwa Hatua wa KoBo:** Kuanzisha utafiti wa mtandaoni

**Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi** unakusudia kukusanya data kulingana na hali halisi ambazo wafanyakazi wa kike wamepitia wanapotoa huduma katika majanga ya kibinadamu.

### Utafiti unaweza kukamilishwa kwa njia mbili:

- Mtandaoni, unajifanyia
- Ana kwa ana, na mwanatimu ya kukusanya data

Utafiti huu ni dodoso la kina linalotumiwa kukusanya taarifa juu ya kuelewa jinsi wafanyakazi wa kike walio salama na wanaopata usaidizi wanavyohisi, kiwango cha umakini wa shirika katika masuala kama vile dhuluma na udhalilishaji wa kingono pamoja na unyanyasaji wa kingono, na jinsi usaidizi wa kibinadamu ulivyoandaliwa kushughulikia changamoto hizo na kupatia mahitaji ya wafanyakazi wa kike, wanawake na wasichana kipaumbele. Madhumuni ya utafiti huu ni kunasa mtazamo wa pamoja, kutoka kwa sampuli ya kikundi cha wafanyakazi wa kike na wa kiume, juu ya ahadi za kitaasisi, ufanisi wa taratibu za malalamiko, na viwango vinavyotambulika vya hatari, usalama na usaidizi.

**Important ! Efforcez-vous d'atteindre et d'inclure des répondant(e)s de toutes les catégories de personnel au sein des organisations, comme les chauffeurs, les agent(e) s d'entretien, les cuisinières/ers, les gardiens, les assistant(e)s, les agent(e)s, les responsables, les coordinatrices/eurs, etc.**

**Travaillez avec les membres du personnel qui souhaitent répondre à l'enquête mais qui ont des compétences limitées en matière d'alphabétisation/d'informatique. Aidez-les à accéder discrètement et confidentiellement à l'enquête et à y répondre de la manière qui leur convient le mieux.**

**Utafiti huu unauliza maswali kadhaa katika kategoria zifuatazo:**

- Kujitolea na Uwajibikaji
- Utaratibu wa Kuwasilisha Malalamiko: Urahisi, Usiri na Hatari
- Hatua Zinazochukuliwa na Shirika
- Utambuzi wa Hatari
- Kushirikishwa kwa Wanawake katika Kutunga na Kutekeleza Sera

# Maoni ya Washiriki

## Zana ya Maoni ya Washiriki

Mbali na zana kuu nne za kukusanya data, **Zana ya Maoni ya Washiriki** pia hupewa timu za Barometa ili kukusanya maoni kutoka kwa idadi ndogo ya nasibu inayochaguliwa miongoni mwa wale walioshiriki katika shughuli za Barometa na ukusanyaji wa data (FGD, KII, Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi na Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia).

Utafiti huu wa maoni unaweza kufanywa kwa njia ya kuwauliza wahojiwa kwa mdomo, au wahojiwa wanaweza kuukamilisha wao wenyewe na kuurudisha kwa timu ya Barometa. Wahojiwa wataulizwa watoe maoni baada ya wao kushiriki ama siku hiyo hiyo au wakati ambapo timu ya Barometer itapanga na mhojiwa arejee mahali pale.

Zana hii ya maoni ni mchanganyiko wa maswali ya kuteua jibu na yale ya kueleza. Maswali mengi ya kuteua jibu huwa na swali la kufuatilia linalolenga kupata maelezo ya ziada na ya kina kutoka kwa mhojiwa, ama kwa kujieleza au kwa kuandika. Wanaojibu wanaweza kutoa maoni mengi au machache kadri wanavyotaka. Hakikisha kuwa wahojiwa wenye uwezo na ujuzi wowote wa kusoma na kuandika wana njia za siri na za busara za kutoa maoni yao.

Madhumuni ya maoni haya ni kuboresha utekelezaji wa utafiti wa baadaye wa Barometa kwa kuweka kumbukumbu za: 1) Jinsi wahojiwa walielewa kuhusika kwao na madhumuni ya shughuli na ushiriki wao, 2) Hali yao ilivyokuwa kama washiriki, na 3) Wanachofikiri kingeweza kuboreshwa wakati ujao.

# Kuendesha Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Dokezo la Mwongozo

## Kabla ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD)

- Hakikisha kuwa ni wanawake pekee wanaoendesha vikao vya FGD huku wanawake na wasichana pia wakihudumu katika majukumu ya Mratibu, Mnakili Kumbukumbu na Mkalimani, ikihitajika.
- Hakikisha kuwa mtaalamu wa masuala ya ukatili wa kijinsia (UWAKI) (Anayeshughulikia visa hivi, Msimamizi au Mhudumu) yuko tayari na yuko katika eneo la FGD ili kutoa mwongozo na usaidizi zaidi kwa timu inayoendesha vikao (ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na washiriki watarajiwa na kusaidia timu kutafuta nafasi za kuandaa vikao vya FGD na wanawake na wasichana).
- Hakikisha kuwa timu nzima imepata na inaelewa maelezo kuhusu rufaa, usaidizi na huduma zinazopatikana.
- Hakikisha kwamba kila mtu anaelewa kikamilifu kuwa kanuni ya usiri lazima idumishwe kila wakati, kulingana na kanuni elekezi.
- Hakikisha timu inaelewa kuwa haifai katika hali yoyote kukusanya taarifa zinazotambulika kutoka kwa mshiriki yeyote. (yaani, majina ya watu, anwani, maelezo ya visa maalum, n.k.). Taarifa hii HAIHITAJIKI kamwe na inahatarisha usalama na faragha ya wale wanaohusika.

## Wakati wa Majadiliano ya Kikundi Lengwa

- Vikao vya FGD havifai kuendelea kwa zaidi ya saa moja; huenda washiriki wakaanza kupoteza umakini baada ya saa moja.
- Tambulisha kanuni muhimu:
  - o Hakikisha washiriki wanafahamu usiri wa majadiliano; na
  - o Hakikisha umepata idhini kutoka kwa washiriki mwanzoni kwa kueleza madhumuni ya shughuli na kwamba wanashiriki kwa hiari.
- Endesha na uhimize mazungumzo yawe katika nafsi ya tatu, ili wanawake na wasichana wazungumzie hali za wanawake na wasichana katika jamii zao kwa upana zaidi.
- Kushughulikia ufichuzi: Kwa sababu za kimaadili, usiwauliwe wasichana au wanawake kuhusu hali zao binafsi za UWAKI. Jambo hili linaweza kusababisha kiwewe na au unyanyapaa. Hata hivyo, ikiwa mshiriki atachagua kufichua kisa cha UWAKI alichopitia yeye binafsi, uwe tayari kushughulikia ufichuzi huo kwa njia ifaayo, ukiheshimu mbinu inayomlenga manusura.

## Kushughulikia Ufichuzi

| Ya Kufanya | Ya Kuepuka |
|---|---|
| Kusikiliza, BILA KUHUKUMU. | Usimlazimu manusura aripoti kama hataki. |
| Toa KWA FARAGHA taarifa sahihi kuhusu huduma zinazopatikana. | Usiulize MAELEZO ya tukio. |
| Mwombe manusura RUHUSA kabla ya kumwelekeza kwa mtu mwingine yeyote. | Usitilie shaka unachoambiwa. |
| Tumia mbinu INAYOMLENGA MANUSURA. | Usitoe USHAURI au MAONI yako kuhusu kile manusura anachopaswa kufanya. |
| Hakikisha USIRI, ukizingatia sheria za eneo lako kuhusu kuripoti kwa lazima katika baadhi ya matukio. | Usitoe AHADI ambazo huwezi kutimiza au kumfanya awe na MATARAJIO. |

## Baada ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa

- Hakikisha kwamba data yote uliyokusanya haiwatambulishi washiriki na haiwezi kuhusishwa tena na kikundi chochote au mtu binafsi, wakiwemo waathiriwa wa UWAKI. Ondoa taarifa zozote zinazoweza kumtambulisha mtu mara moja na ukumbushe timu kwamba hakuna mtu anayepaswa kukusanya taarifa yoyote tambulishi.
- USISHIRIKI data na mtu yeyote nje ya wanatimu ya Barometa ambao wameteuliwa kushughulikia data.
- Kila mwanatimu anayeendesha shughuli ya kukusanya data anawajibu wa kuweka data na kurekodi kumbukumbu zao mwishoni mwa kila siku ya kukusanya data. Anapaswa kutumia violezo na zana zilizotolewa ili kuweka data na kuhakikisha kuwa data hii imehifadhiwa katika folda zinazolindwa kwa nenosiri. Mara tu data ghafi inaporekodiwa, lazima kumbukumbu zote ziharibiwe siku hiyo. Manenosiri yanapaswa kushirikiwa tu na timu ya Barometa, ikiwa ni pamoja na Kiongozi wa Timu, ambaye atawajibikia data hiyo.
- Mambo maalum ya kuzingatia kwa watoto walionusurika:
    - o Katika hali ambapo msichana manusura atafichua tukio la UWAKI, wanaoendesha kikao wanapaswa kuzingatia kanuni ya maslahi bora kwa mtoto;[25] Katika miktadha mingi, katika visa vya watoto manusura, hatua ya kuripoti ni ya lazima. Omba mwongozo kutoka kwa mtaalamu wa UWAKI.

# Mwongozo kwa Wanakili kumbukumbu

## Utangulizi

Kuandika kumbukumbu za Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD) au Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII) kunaweza kuwa jambo ngumu sana hasa wakati kuna mambo mengi yanayojadiliwa. Unaweza kuhisi kuwa unahitaji kuandika kila kitu kinachojadiliwa. Hata hivyo, huhitaji kuandika kila neno linalosemwa—hili linaweza kuwa jambo gumu sana na huenda ukakosa taarifa muhimu. Badala yake, jaribu kurekodi mifano mingi thabiti iwezekanavyo ya kile kinachojadiliwa kulingana na mwongozo ulio hapa chini.

Kwa FGD, itakuwa muhimu kuonyesha katika kumbukumbu zako ni washiriki wangapi wanashiriki mitazamo, wanakubaliana au kutokubaliana na hoja zinazotolewa (kama hoja inatoka kwa mtu mmoja, au watu wengi au kundi zima). Jaribu kuandika data hii inaambatana na maoni ya washiriki wangapi.

Kwa FGD na KII, usiandike maelezo yoyote yanayoweza kumtambulisha mtu (k.m., ya watu au matukio mahususi ya ukatili wa kijinsia (UWAKI), ikiwa ni pamoja na udhalilishaji na dhuluma ya kingono).

25 Kwa habari zaidi juu ya uamuzi bora wa maslahi, angalia Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) "Mwongozo wa Kuamua Maslahi Bora ya Mtoto" (2008): https://www.unhcr.org/4566b16b2.pdf.

### Katika vikao vya FGD/KII:

- Sikiliza ili upate hadithi fupi au mifano madhubuti ambayo imetolewa katika mjadala na uinakili. Itaongeza maelezo muhimu kwenye data.
- Kukija ni hadithi fupi au mifano halisi, jaribu kuandika maneno halisi ya anayeyasema kadiri uwezavyo. Kufanya hivi kutahakikisha kuwa tunarekodi sauti za wanawake na wasichana kwa karibu iwezekanavyo na kukuza sauti zao katika data.
- Jaribu kutazama tabia, jibu na hisia za washiriki katika kikundi, na uandike jinsi mambo yanavyoshirikiwa (k.m., kwa mfadhaiko, hasira, furaha, n.k.).
- Pale ambapo wengi katika kikundi wanakubaliana kuhusu mambo fulani, nakili hili. Makubaliano ya aina hii ni muhimu kwani yana uzito mkubwa wakati kundi nzima (au wengi wao) linakubaliana kuhusu suala fulani.
- Ukianza kusikia mada au masuala yanayoibuliwa, unaweza kuyaandika au kuyachora kwenye daftari lako na uanze kuyaweka pamoja ili uweze kupata taswira na mpangilio bayana zaidi wa kumbukumbu zako. Mbinu hii inaweza pia kusaidia ukija kwenye uchanganuzi wa mada katika *Sehemu ya 3. Uchambuzi wa Data*.
- Tafuta njia yako mwenyewe ya kuandika, kwa kutumia alama au vifupisho kurekodi kile unachosikia na kuona.
- Weka alama za kuuliza karibu na vidokezo au pointi ambazo huna uhakika nazo.

### Baada ya vikao vya FGD/KII:

- Kagua kumbukumbu zako ili uone kama una maswali au kuna sehemu ambazo huna uhakika.
- Tafuta nafasi ya faragha ili ujadili kumbukumbu zako na mratibu na mkalimani (kama alikuwepo) ikiwa una maswali au kuna sehemu ambazo huna uhakika kuhusu pointi au kumbukumbu ulizoandika. Waulize walichosikia na uulize kama wanaweza kusaidia kufafanua au kuongeza chochote.
- Taja manukuu yoyote ya moja kwa moja na mambo muhimu ambayo yanaonekana wazi.
- Angazia mada zozote zinazoanza kujitokeza.

# Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Dokezo la Mwongozo

### Kuna njia mbili za kufanya Tafiti za Mtazamo wa Wafanyakazi:

- **Utafiti wa ana kwa ana:** Ili kupata idhini ya wafanyakazi wanaoweza kushiriki katika Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi, lazima ***Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa*** itolewe kwa washiriki ili kuwasaidia katika kuamua kama wanataka kushiriki au la.
- **Utafiti wa mtandaoni:** Wakati wa kutuma barua pepe yenye kiungo cha kukamilisha Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi mtandaoni, lazima pia *Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa* iambatishwe. Utahitaji kurekebisha karatasi ili kuendana na muktadha wako. Tafiti zitakazofanywa mtandaoni zitakusanywa bila kuwatambulisha watakaoshiriki, kwa kuwa hakuna taarifa zozote zinazoweza kuwatambulisha zitakazohitajika kama sehemu ya utafiti. Wafanyakazi wanaoukamilisha wataamua kwa wakati wao, kwa kutumia maelezo waliyopewa pamoja na kiungo cha utafiti, ikiwa wanataka kushiriki au la.

● *Tazama Kiambatisho: Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa na Idhini baada ya Kufahamishwa ili upate hati ya Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa.*

## Mwongozo wa kuanzisha na kutekeleza utafiti wa mtandaoni

KoBo ndilo jukwaa la mtandaoni linalopendekezwa la kufanya utafiti huu wa wafanyakazi. Tumia hati zifuatazo kukusaidia kuanzisha utafiti wako mtandaoni:

- **Zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Kwa tafiti za mtandaoni (laha ya Excel)** - Utatumia lahajedwali hii kupakia utafiti wako kwenye KoBo.
- **Mwongozo wa Hatua kwa Hatua wa kutumia KoBo: Kuanzisha utafiti wa mtandaoni** - Mwongozo huu utakusaidia kufungua akaunti ya KoBo na kutumia KoBo kwa utafiti wako wa mtandaoni. Hati inajumuisha maagizo juu ya:
    - o Jinsi ya kufungua akaunti ya KoBo na kuwa na akaunti ya kipekee inayolindwa kwa nenosiri;
    - o Jinsi ya kupakia laha iliyotolewa ya Excel kwenye KoBo na kuhakikisha kwamba haina maelezo yanayoweza kuwatambulisha wanaoshiriki (na haikusanyi maelezo yoyote ya kibinafsi, ikiwa ni pamoja na anwani za IP za wanaojibu);
    - o Mahali pa kupata kiungo cha utafiti ili kukishiriki na kukisambaza (tazama hapa chini); na
    - o Jinsi ya kupata na kupakua majibu ya utafiti.

## Usambazaji wa utafiti:

- Katika kusambaza utafiti, jitahidi kushirikisha mashirika mengi tofauti ya kibinadamu yanayotoa usaidizi kadri iwezekanavyo. Njia inayopendekezwa ya kufanya hivi itakuwa kupitia uratibu wa vikundi/sekta ya ukatili wa kijinsia (UWAKI) na vikundi vingine vya uratibu wa sekta. Kupitia msaada wao, unaweza kutuma barua pepe kwa vikundi tofauti vya mashirika ya kibinadamu kupitia orodha zao za barua pepe.
- Unapotuma barua pepe yenye kiungo cha kukamilisha Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi mtandaoni, hakikisha pia kuwa umeambatisha ***Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa***. Utahitaji kurekebisha karatasi ili kuendana na muktadha wako. Taja katika barua pepe yako kwamba Tafiti za Mtazamo wa Wafanyakazi zilizofanywa mtandaoni zitakusanywa bila kuwatambulisha washiriki na kwamba uamuzi wao wa kushiriki ni wa hiari. *Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa* pia ina sehemu mwishoni ambayo unafaa kujaza taarifa kuhusu huduma na usaidizi unaopatikana kwa wafanyakazi wanaotoa misaada ambao wamepitia unyanyasaji wa kingono au aina nyingine za UWAKI.
- Kukusanya majibu ya utafiti mtandaoni: Mfumo wa KoBo utakutolea lahajedwali ya Excel kiotomatiki ili uichanganue. Kisha unaweza kupakua majibu (kama ilivyoelezwa hapo juu) ili uyatumie katika hatua ya uchanganuzi wa data.

## Mwongozo wa kutekeleza utafiti wa ana kwa ana na mmoja wa wanaokusanya data

- Usambazaji wa utafiti: Fuata utaratibu sawa na uliofafanuliwa kwenye utafiti wa mtandaoni. Hakikisha umejumuisha toleo la Word (***Zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Kwa tafiti za ana kwa ana*** ) la utafiti katika barua pepe yako na uangazie kuwa chaguo zote mbili—ana kwa ana au mtandaoni—zinapatikana.
- Ili upate idhini kutoka kwa wafanyakazi wanaoweza kushiriki katika Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi, lazima *Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa* itolewe kwa washiriki watarajiwa ili kuwasaidia katika kuamua kama wanataka kushiriki au la, na kuhakikisha wanapata muda na nafasi wanayohitaji kujifanyia uamuzi. Hakikisha umerekebisha laha hii na uongeze taarifa muhimu kwa muktadha wako.
- Ikiwa washiriki watatoa idhini yao, panga kukutana nao katika eneo salama, lililojificha na la siri ili kufanya utafiti.
- Muhimu: Washiriki wa timu ya Barometa wanaoendesha utafiti wa ana kwa ana WASIWE wametoka shirika moja na mhojiwa.

# Mwongozo wa Hatua kwa Hatua wa Kufungua Akaunti na Kutumia KoBo

**Mwongozo wa hatua kwa hatua** wa kutumia akaunti ya KoBo kwa utafiti wako wa mtandaoni. Hati inajumuisha maagizo juu ya:

- o Jinsi ya kufungua akaunti ya KoBo na kuwa na akaunti ya kipekee inayolindwa kwa nenosiri;
- o Jinsi ya kupakia karatasi iliyotolewa ya Excel kwenye KoBo;
- o Mahali pa kupata kiungo cha utafiti ili kukishiriki na kukisambaza; na
- o Jinsi ya kupata na kupakua majibu ya utafiti.

### Hatua ya 1 Kufungua akaunti yako isiyolipishwa ya KoBo

- **Nenda kwenye ukurasa wa wavuti**: **https://kobo.humanitarianresponse.info/accounts/register/#/**
  - o Kwenye ukurasa wa "Fungua akaunti mpya (Create an account)", jaza maelezo yako na ubofye kitufe cha kijani "FUNGUA AKAUNTI (CREATE ACCOUNT)" chini mwa ukurasa.
  - o Fungua barua pepe yako na "UWEZESHE (ACTIVATE)" akaunti yako ya KoBo Toolbox kwa kubofya kiungo kilichotolewa kwenye barua pepe.
  - o Mara tu utakapobofya kiungo, utarudishwa kwenye kivinjari chako ambapo utaona dashibodi yako ya mradi wa KoBo.
  - o Sasa uko tayari kutumia KoBo!

### Hatua ya 2. Kuanzisha mradi "mpya": kupakia faili ya zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi ndani ya KoBo

- Kwenye dashibodi ya mradi wa KoBo, bofya "MPYA (NEW)" upande wa juu wa kushoto na skrini ya Anzisha mradi: Chagua chanzo (Create project: Choose a source) itatokea. Kisha ubofye "PAKIA fomu ya XLSForm (UPLOAD an XLSForm)."
  - o **Tafuta Zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi (Hati ya Excel) Faili hii inaitwa:** "Zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi.XLS"[26]
    . Muhimu: Usibadili data au taarifa yoyote katika laha hii ya Excel.
  - o **Baada ya kupata faili, ipakie kwenye KoBo:** Ichague AU "buruta na udondoshe" faili ya Excel moja kwa moja kwenye skrini ibukizi.
  - o Pindi faili ya "Zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi.XLS" itakapopakiwa, andika "JINA LA MRADI (PROJECT NAME)" Wako: Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi. Unaweza pia kuongeza "MAELEZO (DESCRIPTION)." Ili kukamilisha mchakato huu, bofya "ANZISHA MRADI (CREATE PROJECT)" na zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi sasa itapakiwa.

### Hatua ya 3. Kupata kiungo cha Utafiti wako wa Mtazamo wa Wafanyakazi kinachoweza kushirikiwa

- ☐ Kwa kuwa sasa utafiti umepakiwa, unaweza "KUANGALIA (PREVIEW)" utafiti kwa kubofya aikoni ya "jicho" kwenye kona ya juu kulia. Hatua hii itafungua skrini ya "kuangalia" inayokuonyesha kile mshiriki ataona atakapokuwa akikamilisha utafiti.
- ☐ Baada ya kuamua kuwa utafiti uko tayari kutumika, **bofya "SAMBAZA (DEPLOY)" ili kufanya utafiti wako UPATIKANE MOJA KWA MOJA**.
- ☐ Ili kushiriki kiungo chako cha utafiti, nenda chini hadi sehemu ya Kukusanya Data na ubofye "NAKILI" ili unakili kiungo cha utafiti. Sasa unaweza kushiriki kiungo hiki na mtu yeyote ambaye atakamilisha utafiti huu.

26 Zana ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi.XLS ya kuweka utafiti wa KOBO inaweza kupatikana katika https://gbvresponders.org/womens-movement-building/listen-up/

- Utaweza kubandika kiungo hiki kwenye Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa (inapatikana katika Kiambatisho Karatai ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometa na Fomu ya Idhinibaada ya kufahamishwa) au mawasiliano mengine unayotumia kusambaza kiungo cha utafiti.

  - ☐ Unaweza pia kufungua utafiti kwa kubofya “FUNGUA” na dirisha tofauti litaonekana likiwa na zana yako.

### Hatua ya 4. Kupakua data ya Utafiti wa Maoni ya Wafanyakazi

- ☐ Ukishakusanya angalau tafiti MOJA au ZAIDI kutoka kwa washiriki wako mtandaoni, ukurasa mpya unaoitwa “DATA” utapatikana kwenye ukurasa wa mradi wa KoBo. Bofya kwenye ukurasa huu na utakuleta kwenye ukurasa wa ripoti ya muhtasari.
- ☐ Katika upande wa kushoto, bofya “VIPAKULIWA (DOWNLOADS)” ili kwenda kwenye ukurasa wa Kupakua Data. Ukiwa tayari kupakua data yako, bofya kitufe cha “HAMISHA (EXPORT)”.
- ☐ Sogeza chini hadi “FAILI ZILIZOHAMISHWA (EXPORTS),” na faili ambayo umehamisha sasa iko tayari kupakuliwa. Ili kupakua, bofya kwenye aikoni ya kishale inayoelekeza chini, na faili ya Excel iliyo na data yako ya utafiti itapakuliwa kiotomatiki.
- ☐ Tafuta mahali faili imepakuliwa, na sasa data yako ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi iko tayari kuingizwa kwenye ***Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data*** (Excel)[27]

27 Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data (Excel) inaweza kupatikana katika https://gbvresponders.org/womens-movement-building/listen-up/

# Sehemu ya 3

# Uchambuzi wa Data



Picha na N Todres, IRC

# Muhtasari: Maeneo manne ya matokeo ambayo Barometa hupima

Barometa hupima maeneo manne muhimu ya matokeo:

1. Les femmes et les filles ont confiance en et ont accès à des services de soutien sûrs, confidentiels et redevables lorsqu'elles sont confrontées à la VBG, y compris au harcèlement, à l'exploitation et aux abus sexuels.
2. Les femmes et les filles accèdent aux services et ressources humanitaires et les contrôlent de manière égale.
3. Les travailleuses/eurs humanitaires utilisent leur pouvoir de manière positive et respectent et valorisent les femmes et les filles ainsi que les communautés affectées.
4. Les organisations humanitaires rendent leur personnel redevable pour lutter contre le harcèlement, l'exploitation et les abus sexuels.

Barometa hutumia zana nne za kukusanya data kukusanya taarifa katika maeneo yote manne ya matokeo:

1. Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD)
2. Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII)
3. Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia
4. Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi

Aidha, kuna zana nne zinazotumiwa kunasa data kutoka kwa shughuli tatu kati ya hizo:

- Kiolezo cha Madokezo ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa
- Kiolezo cha Madokezo ya Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu
- Kiolezo cha Majibu ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi (kwa tafiti za ana kwa ana)
- Majibu ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi Mtandaoni kupitia KoBo (kwa tafiti za mtandaoni)

Zana hizi zinaweza kupatikana katika sehemu ya *Viambatisho Zana za Kukusanya Data*.

# Kutoka kurekodi data hadi uchanganuzi wa data: hatua 3

Kuna hatua tatu kuu za kuchukua baada ya kukusanya data yote:

1. **Kurekodi na kuchanganua data ya kiasi (idadi)**
2. **Kukagua na kuchambua data kulingana na mada kwa misingi ya ubora (simulizi)**
3. **Kuchanganua matokeo yako ya jumla ya Barometa**

Sehemu tatu zinazofuata zitakuongoza kupitia hatua hizi kwa undani zaidi, ikijumuisha jinsi data inavyohesabiwa, jinsi ya kurekodi data na jinsi ya kuelewa na kuchanganua data yako.

## Hatua ya 1: Kurekodi na kuchanganua data ya kiasi - tafiti za kuchunguza kwa kuangalia na mtazamo wa wafanyakazi

Utatumia zana zako mbili za kukusanya data ili kupata alama ya Barometa:

- Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia
- Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi (majibu ya ana kwa ana na ya mtandaoni)

### Zana ya Excel ya Kurekodi na Kuchambua Data

Ili kurekodi data yote ya nambari kutoka kwa zana hizi mbili za kukusanya data, utaingiza alama kutoka kwa kila moja ya zana hizi hadi kwenye zana kuu ya Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data (Excel). Hati hii inaweza kupatikana katika Sehemu ya 3  Zana za Kurekodi na Kuchambua Data. Maagizo ya hatua kwa hatua kuhusu jinsi ya kutumia hati hii na kurekodi/kuongeza data yako yanaweza kupatikana katika sehemu iyo hiyo. Kwa Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi uliokamilishwa ana kwa ana, utaweza kuongeza data hiyo moja kwa moja kutoka kwa fomu ulizotumia kukusanya data. Kwa Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi uliokamilishwa mtandaoni, kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya 2. Utekelezaji, utahitaji kupakua majibu kutoka kwa zana ya KoBo na kuyaingiza kwenye Excel.

### Kuhesabu alama

Baada ya kuongeza data yote kutoka kwa zana hizi mbili za kukusanya data, hati ya Excel itakokotoa kiotomatiki alama zako za jumla za Barometa. Inakuruhusu uone alama ya kila moja ya matokeo manne na ya vipengele tofauti vinavyopimwa. Hili linakupa wepesi wa kuchagua pointi na uchanganuzi wa data ambao ungependa kujumuisha katika mapendekezo na utetezi wako (angalia Sehemu ya 4. Utetezi na Usambazaji kwa maelezo zaidi).

### Je, kipimo cha Barometa kinatoa alama vipi?

**Barometa hutumia “mfumo wa taa za barabarani”** (Rangi Nyekundu, ya Chungwa, ya Manjano na ya Kijani) ili kutoa alama kwa hali ya usaidizi wa kibinadamu katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia (UWAKI) na unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono katika maeneo manne ya matokeo.

Katika kila mojawapo ya maeneo haya manne, kuna vigezo tofauti ambavyo vinatathminiwa kando kando. Kila kigezo kina mfululizo wa vipengele ambavyo vitapewa alama kati ya 1-4 (Nyekundu hadi Kijani), kulingana na taarifa iliyokusanywa kutokana na zana nne za kukusanya data: Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia, Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FGD), Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi na Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII).[28]

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Rouge** 1 point | **Orange** 2 points | **Jaune** 3 points | **Vert** 4 points |

Kutoka kwenye alama hizi, Barometa itatoa majibu mawili: ukadiriaji wa binafsi wa kila mojawapo ya maeneo hayo manne ya matokeo kutoka nyekundu hadi kijani; na, kwa kujumlisha alama kutoka maeneo yote manne, alama ya jumla ya usaidizi wa kibinadamu unaotathminiwa.

| | |
|---|---|
| 91-100% | Bonne réalisation de tous les critères ; représente une bonne pratique et une forte capacité de l'environnement de l'aide humanitaire à prévenir et à répondre à la VBG, y compris l'exploitation et les abus sexuels et le harcèlement sexuel ; dépasse les normes minimales. |
| 67-90% | Réalisation satisfaisante de la plupart des critères ; démontre la capacité de prévenir et de répondre à la VBG, y compris l'exploitation et les abus sexuels et le harcèlement sexuel ; atteint les normes minimales. |
| 51-66% | Réalisation limitée de la plupart des critères ; démontre une certaine capacité à prévenir et à répondre à la VBG, y compris l'exploitation et les abus sexuels et le harcèlement sexuel ; des améliorations sont nécessaires pour garantir le respect des normes minimales. |
| 0-50% | Réalisation insuffisante de l'ensemble des critères ; l'environnement de l'aide humanitaire ne prévient pas et ne répond pas de manière adéquate à la VBG, y compris l'exploitation et les abus sexuels et le harcèlement sexuel ; une planification stratégique claire est nécessaire pour améliorer les politiques et les pratiques ; inférieur aux normes minimales. |

Ili kupata alama hii ya jumla, utahitaji kwanza kupata matokeo kutoka kwa zana hizi mbili za kukusanya data.

28 Tazama Sehemu ya 2: *Utekelezaji.*

# Mwongozo wa kuhesabu data ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi

Sehemu mbili zifuatazo zinatoa mwongozo wa jinsi ya kupatia matokeo yako ya zana za Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi alama, kwa kuongeza zana hizi kwenye Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data (Excel).

## Kuhesabu data ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia

**Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia** unajumuisha maswali 66 ambayo yanatathmini maeneo mawili makuu ya usaidizi wa kibinadamu: 1) Mbinu za Kuzuia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono na Sera za Usalama, na 2) Mazingira ya Usaidizi wa Kibinadamu. Maeneo haya yanagawanywa katika mada 16 za tathmini, kila moja ikihesabiwa chini ya eneo moja au zaidi la matokeo.

**Ukaguzi wa hati: Mbinu za Kuzuia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono na Sera za Usalama**

Sehemu hii inahusisha ukaguzi wa hati zilizopo ambazo zinapatikana kwa umma.

- ☐ Ahadi za jumuiya ya kibinadamu katika kushughulikia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono
- ☐ Mitandao ya Kuzuia Udhalilishaji na Dhuluma za Kingono (PSEA)
- ☐ Mbinu na Utaratibu wa Malalamiko ya Kijamii (CBCM)
- ☐ Ufikiaji wa CBCM
- ☐ Maeneo salama kwa wanawake na wasichana
- ☐ Rufaa zinazopatikana kwa jamii
- ☐ Ukaguzi wa usalama

**Uchunguzi katika eneo halisi: Mazingira ya Usaidizi wa Kibinadamu**

Sehemu hii inahusisha kutembea mwenyewe na kujionea mazingira ambapo usaidizi wa kibinadamu unatolewa.

- ☐ Kuzuia na kupunguza UWAKI
- ☐ Maeneo salama kwa wanawake na wasichana
- ☐ Huduma ya afya
- ☐ Huduma za lishe

Zana ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia (*Kiambatisho: Zana za Kukusanya Data*) ina safu wima ya kulia kabisa, "Alama," ambapo utapata alama za kila swali. Maswali yote katika zana hii yana uzito sawa, na alama huanzia:

- pointi 1
- pointi 0.75
- pointi 0.50
- pointi 0.25
- pointi 0
- Majibu ya Sijui au Sina Jibu (NA) hayajumuishwi kwenye alama

Alama ya "1" inawakilisha jibu chanya zaidi kwa swali. Alama ya "0" inawakilisha jibu hasi zaidi kwa swali. Alama hizi zitaongezwa na kukokotolewa dhidi ya jumla ya alama za juu zaidi zinazowezekana za Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.

Majibu yoyote ya "Sijui" au "Sina Jibu (NA)" hayatahesabiwa katika alama ya mwisho kama chanya au hasi. Utaratibu huu pia utatumiwa kwa maswali yote ambayo YAMERUKWA. Maswali hayo yataondolewa kiotomatiki kwenye alama, na alama ya juu kabisa inayowezekana itapunguzwa ipasavyo.

- **Kwa mfano:** Ikiwa ulitia alama ya "NA" kwenye maswali 5, alama ya juu zaidi unayoweza kupata kwa muktadha na eneo lako itakuwa ***61*** (66 kutoa 5 = 61). Kwa hivyo, muktadha na eneo lako linaweza kupata jumla ya alama **34** kati ya jumla ya upeo mpya unaowezekana wa alama ***61*** ambazo zinaweza kufikiwa katika Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.

**Hutahitaji kufanya hesabu hizi au kufanya mabadiliko wewe mwenyewe**-- Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data (Excel) itakufanyia kazi hiyo, kulingana na data utakayoingiza. Utakapoingiza alama binafsi, zitatoa alama ya jumla ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia ya maeneo yaliyotathminiwa; pia zitachangia katika alama ya jumla ya Barometa, ambayo inajumuisha matokeo ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi. Angalia sehemu inayofuata.

## Kuhesabu alama za Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi

Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi unajumuisha maswali 43 yanayolenga mada tano za tathmini, kila moja ikihesabiwa chini ya eneo moja au zaidi la matokeo:

- ☐ Kujitolea na Uwajibikaji (Matokeo ya 3 na 4)
- ☐ Utaratibu wa kuwasilisha Malalamiko: Urahisi, Usiri na Hatari (Matokeo ya 2, 3 na 4)
- ☐ Hatua Zinazochukuliwa na Shirika (Matokeo ya 1 na 3)
- ☐ Kushirikishwa kwa Wanawake katika Kutunga na Kutekeleza Sera (Matokeo ya 2 na 3)
- ☐ Utambuzi wa Hatari (Matokeo ya 2 na 3)

Katika hati ya Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Jinsi ya Kuhesabu Alama za Utafiti Huu (Sehemu ya 3: Kurekodi na Kuchambua Data) utaona utafiti, pamoja na safu wima ya ziada upande wa kulia yenye alama kwa kila swali. Alama hizi zinaanzia:

- pointi 1
- pointi 0.75
- pointi 0.50
- pointi 0.25
- pointi 0
- Majibu ya Sijui au Sina Jibu (NA) hayajumuishwi kwenye alama

Alama ya "1" inawakilisha jibu chanya zaidi kwa swali. Alama ya "0" inawakilisha jibu hasi zaidi kwa swali. Alama hizi zitaongezwa na kukokotolewa dhidi ya alama za jumla za juu zaidi zinazowezekana kwa Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi.

Majibu yoyote ya "Sijui" au "Sina Jibu (NA)" hayatahesabiwa katika alama ya mwisho kama chanya au hasi. Utaratibu huu pia utatumiwa kwa maswali yote ambayo YAMERUKWA. Maswali hayo yataondolewa kiotomatiki kwenye alama, na alama ya juu kabisa inayowezekana itapunguzwa ipasavyo.

Hutahitaji kufanya hesabu hizi au kufanya mabadiliko wewe mwenyewe-- Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data (Excel) itakufanyia kazi hiyo, kulingana na data utakayoingiza. Utakapoingiza alama binafsi, zitatoa alama ya jumla kwa Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi; pia zitachangia alama ya jumla ya Barometa, ambayo inajumuisha matokeo ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.

**Dokezo kuhusu uzani na umuhimu tofauti unaowekewa baadhi ya maswali**

Maswali yote katika Utafiti wa Maoni ya Wafanyakazi yana uzito sawa, isipokuwa maswali mawili ya kwanza (Swali la 1, Swali la 2) na Swali la 24 na Swali la 25. Maswali haya yamepewa uzito maradufu, kumaanisha kwamba alama zake zitakuwa na athari kubwa kwa jumla. Utakapoingiza alama kwenye Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data (Excel), majibu ya maswali haya yatarekodiwa moja kwa moja na uzani maradufu.

## Swali la 1 na Swali la 2 yanachukuliwa kuwa maswali muhimu ambayo mengine yote yanaegemezwa:

**Swali la 1.** Kwa kipimo cha 1 (Ni muhimu sana) hadi 5 (Sio muhimu hata kidogo), suala la unyanyasaji wa kingono lina umuhimu kiasi gani katika shirika lako?

**Swali la 2.** Kwa kipimo cha 1 (Ni muhimu sana) hadi 5 (Si muhimu hata kidogo), suala la udhalilishaji na dhuluma ya kingono lina umuhimu kiasi gani katika shirika lako?

Haya yanauliza maswali mawili ya msingi: ikiwa masuala ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono ni muhimu kwa mashirika haya. Ikiwa masuala haya hayaonekani kuwa muhimu, huenda hayatapewa kipaumbele na yataathiri jinsi shirika linavyochukua hatua, kupanga na kukabiliana na masuala hayo na usalama na ulinzi wa wanawake kwa jumla. Swali la 24 na Swali la 25 yanafuata ruwaza sawa.

**Swali la 24.** Kwa maoni yako, masuala ya usalama na ulinzi wa wanawake yanashughulikiwa kikamilifu na sera na desturi za usalama na ulinzi zilizopo katika shirika lako?

**Swali la 25.** Kwa maoni yako, kukija ni masuala ya usalama na ulinzi, uhalisia na hali za wanawake zinazingatiwa kikamilifu katika sera na desturi za rasilimali watu zilizopo katika shirika lako?

Haya yanauliza kama uhalisia, hali na masuala ya usalama na ulinzi wa wanawake yanazingatiwa katika sera na taratibu za usalama na rasilimali watu, mambo ambayo yanaathiri vipengele vikuu vya hali ya wanawake kazini, ikiwa ni pamoja na usafiri, malazi, vifaa vya ofisi na maeneo ya kazi, faida, vyakula, nk. Ikiwa wanawake hawazingatiwi na hawaonekani katika sera hizo, usalama wa wanawake unadhoofishwa, kutoshughulikiwa na kutothaminiwi sana. Suala hili linaweza kuathiri maswali mengine yote yanayotathmini jinsi mashirika yanavyoshughulikia usalama wa wanawake kupitia sera na desturi zake. Ndiyo maana maswali haya yana uzito zaidi kuliko mengine.

## Hatua ya 2: Kukagua na kuchambua data kulingana na mada kwa misingi ya ubora - majadiliano ya vikundi na mahojiano ya watoa taarifa muhimu

Hatua hii inayofuata inashughulikia jinsi ya kukagua na kuchambua zana za Majadiliano ya Vikundi Lengwa na Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu.

**Majadiliano ya Vikundi Lengwa** ya wanawake na wasichana yanajumuisha hatua nane, kila moja ikiwa na mfululizo wa maswali elekezi. Kupitia njia ya kushirikisha jamii katika kutambua rasilimali, zana hii inashughulikia mada zifuatazo saba: mashauriano na wanawake na wasichana; wasiwasi na maeneo yasiyo salama kwa wanawake na wasichana; vifaa vya hadhi; vitu visivyo vya kula (NFI) na usambazaji wa chakula; maeneo salama; mifumo ya kuwasilisha malalamiko katika jamii; na ushauri wa kujenga mazingira salama zaidi. Mada hizi zote pia zinazingatiwa katika Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.

**Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu** ya wanaharakati, vikundi na mashirika ya haki za wanawake yanajumuisha maeneo tano makuu, kila moja likiwa na msururu wa maswali.

Tumia ***Kidokezo cha Mwongozo wa Uchambuzi wa Data kutoka kwa Matini*** (ona *Sehemu ya 3 Zana za Kurekodi na Kuchambua Data* kwa mwongozo wa uchambuzi kwa misingi ya mada) ili kukusaidia katika kuchanganua data yako ya simulizi kutoka vikao vya FGD na KII (kwa kutumia maelezo yako ya KII na FGD na ramani za jumuiya kutoka vikao vya FGD). Hii itakusaidia kutambua mada muhimu zaidi zinazotokana na mazungumzo hayo na kutambua vipande vya habari na madondoo muhimu. Kisha utatumia uchanganuzi huu ili kukamilisha na kuongeza maelezo, ukwasi na utofauti wa simulizi kwenye alama za Barometa zilizopatikana hapo juu.

Mara tu unapomaliza uchanganuzi wako wa data ya simulizi, nenda kwenye hatua inayofuata ambapo utaongozwa katika namna ya kuchanganya alama yako ya Barometer na matokeo yako ya data ya simulizi kutoka kwa zana hizi.

# Hatua ya 3: Uchanganuzi wa matokeo yako ya jumla ya Barometa

Katika hatua hii ya tatu, leta pamoja alama za nambari zilizokokotolewa na kuchanganuliwa kiotomatiki kutoka kwa zana ya Excel na uchanganuzi wako wa matini. Hatua hii itakuongoza kujadili, kuhakiki, kuchambua na kuunganisha matokeo na kuyakamilisha (kwa maandalizi ya uthibitishaji wa data katika Sehemu ya 4. Utetezi na Usambazaji). Unaweza kupata kwamba unapoanza kwenye maswali ya kwanza, kikundi kinaweza kujadili maswali mengi ya baadaye kabla ya kuyafikia. Tumia mbinu zilizo hapa chini kama mwongozo wa jumla ili kukusaidia kuleta uelewaji, maana na muunganisho katika seti yako yote ya data, pamoja na tofauti ndogo ndogo zilizo ndani yake.

- ☐ Tafuta njia ya kuonyesha kwa ubayana seti zote mbili za data mbele ya timu yako. Anza kwa kujadili kwa mapana kile unachokiona kwenye seti za data, ukitumia maswali haya kama mwongozo. Utaratibu huu unakusudiwa kupata maoni na majibu ya mwanzo na ya haraka kutoka kwa timu:
    - o Unaona nini kuhusu data hii?
    - o Ni nini kinachoshangaza? Ni nini ambacho si cha kushangaza?
    - o Ni nini kipya kwako? Ni nini ambacho tayari ulikuwa unajua?
- ▪ Kwa maswali elekezi yanayofuata, zingatia zaidi kila seti ya data, na uanze kuandika madokezo au michoro ya majadiliano:
    - o Je, kuna mfanano na uhusiano wowote kati ya seti za data (za idadi na ubora)? Ikiwa upo, ni nini kinachofanana au kinachoshirikiwa? Je, jambo hili linasema nini kuhusu matokeo na uchambuzi? Ni yapi kati ya matokeo yanayoungana mkono kati ya seti zote mbili? Uhusiano uliopo ni upi?
    - o Je, kuna tofauti zozote? Je, matokeo yoyote kutoka kwa seti moja yanahitilafiana na matokeo kutoka seti nyingine? Je, seti hizi zinaonyesha matokeo tofauti? Ikiwa ndiyo, ni nini tofauti, ni nini kinachohitilafiana? Je, jambo hili linasema nini kuhusu matokeo na uchambuzi? Je, mambo haya yanaweza kushughulikiwa au kutatuliwa au la?
- ▪ Kisha, zingatia data iliyounganishwa na mjadili maswali yafuatayo elekezi ili kukusaidia kuzingatia zaidi vipengele thabiti, vya kina na mahususi vya kile data inakuambia:
    - o Je, hali ya sasa ikoje kwa wanawake na wasichana na wafanyakazi wa kike wanaotoa misaada, kulingana na yake ambayo uchambuzi unaonyesha? (Zingatia maeneo yote manne ya Barometa.)
    - o Ni nini kimebadilika? Kimekuwa bora au kibaya zaidi? Au hakijabadilika hata kidogo?
    - o Je, kuna nini cha kujifunza?
    - o Ni mapendekezo gani yanayojitokeza?
    - o Ni hatua au mabadiliko gani yanayohitajika ambayo yanajitokeza kama muhimu au ya kupewa kipaumbele? Na mahitaji haya yanahitaji kuelekezwa kwa nani?

Pindi unapopitia mchakato huu wa kutafakari, andika kumbukumbu za kina (pamoja na madondoo makuu ambayo tayari ulichagua) ili kunasa kwa usahihi uchambuzi na mijadala yako kwa jumla. Utapeleka uchanganuzi huu mbele katika sehemu inayofuata ya kuthibitisha data na Sehemu ya 4. Utetezi na Usambazaji, ambapo utathibitisha alama zako na kuandaa mapendekezo na utetezi wako.

# Maagizo ya Hatua kwa Hatua ya Kutumia *Hati ya Kurekodi na Kuhesabu Data*(Excel)

Tumia hatua nne zifuatazo kukuelekeza jinsi ya kutumia hati ya ***Kurekodi na Kuhesabu Data*** : jinsi ya kutayarisha zana yako kwa matumizi; jinsi ya kuvinjari zana hii; jinsi ya kuingiza data iliyokusanywa kutoka kwa Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na Tafiti za Mtazamo wa Wafanyakazi; na jinsi ya kuona alama za mwisho.

- *Kwa maagizo ya kina kuhusu jinsi ya kufanya marekebisho au mabadiliko kwenye zana yenyewe, tafadhali angalia kichupo cha "Maelekezo" kwenye zana. Tahadhari: Zana hii inategemea pakubwa makro, fomula za Excel, majedwali badilifu na zana za wasanidi kama vile vitufe vya redio. Fanya marekebisho au mabadiliko yoyote kwa uangalifu, kwani yanaweza kuzuia zana kufanya kazi vizuri.*

### 1. Kufungua, kuhifadhi na kulinda zana yako kwa nenosiri

- Unapofungua hati ya Excel, utaona ujumbe: ***"Hati hii ina macros (This workbook contains macros)…"***. Bofya kitufe cha **"Washa macros (Enable macros)"** ili kufungua hati ili iwe zana inayoweza kufanya kazi kikamilifu.
- Unapohifadhi zana yako na jina la faili ulilochagua, hakikisha kwamba:
  - o Umechagua **"Chaguo…, (Options…,)"** ambayo itakupa chaguo la kulinda faili yako kwa nenosiri. Chagua nenosiri ambalo litatumika kufungua na kurekebisha faili; na
  - o Hifadhi faili kama aina ya faili: ***"Excel Macro-enabled Workbook.xlsm"***.

### 2. Kutumia zana

☐ Utaona "vichupo" nane tofauti katika sehemu ya chini ya hati. Vichupo hivi ni:

- o **Kichupo cha 1. Mwanzo** - Hutoa maelezo juu ya yaliyomo kwenye zana hii;
- o **Kichupo cha 2. Maagizo** - Hutoa maelezo na maelekezo ya kina zaidi ya jinsi ya kufanya marekebisho au mabadiliko ya zana (tafadhali rejea tahadhari iliyotajwa hapo juu);
- o **Kichupo cha 3. Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia** - Tumia zana hii **kuweka data** kutoka kwa Utafiti wote wa Kuchunguza kwa Kuangalia;
- o **Kichupo cha 4. Utafiti wa Wafanyakazi** - Tumia zana hii **kuweka data** kutoka kwa Tafiti za Mtazamo wa Wafanyakazi zilizofanywa ana kwa ana na/au mtandaoni;
- o **Kichupo cha 5. Aina za utoaji alama** - Hutoa maelezo kuhusu jinsi majibu tofauti ya maswali yanavyopatiwa alama katika zana hii;
- o **Kichupo cha 6. Barometa** - Hutoa maelezo kuhusu alama ya jumla ya Barometa ya muktadha wako, pamoja na alama mahususi kwa kila moja ya maeneo manne ya matokeo;
- o **Kichupo cha 7. Barometa kwa Mada** - Hutoa maelezo kuhusu alama za kina katika maeneo ya kibinafsi ndani ya kila zana ya kukusanya data; na

- o **Kichupo cha 8. Data** - Hutoa maelezo kuhusu data ghafi uliyorekodi/kuongeza katika Vichupo vya 3 na 4. Utaweza kuona kitambulisho kilichotolewa kwa kila utafiti (ama wa kuchunguza kwa Kuangalia au wa Maoni ya Wafanyakazi), pamoja na data yake kwa kila jibu na uzani uliopewa kila jibu. Data kutoka kwa muktadha wako ikishaongezwa hapa kiotomatiki baada ya kuwasilisha tafiti zako, unaweza kwenda kwenye kichupo hiki na ufute maandishi, ***"Safu mlalo ya kishikilia nafasi ambayo inaweza kufutwa baada ya data kuongezwa hapa chini."***

### 3. Kurekodi/kuongeza data yako kutoka kwa zana mbili za kukusanya data

- ☐ **Kichupo cha 3. Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia**: Tumia kichupo hiki **kuingiza data yako yote** kutoka kwa Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia:

  a. Kuna vitufe 5 katika sehemu ya juu ya Kichupo:
     - **WEKA UPYA FOMU (NYEKUNDU)** - Bonyeza sehemu hii ikiwa unataka kufuta data iliyo kwenye fomu na uanze tena.
     - ANGALIA MAJIBU - Hii ndiyo fomu kuu ambapo utarekodi/kuongeza data yako kutoka kwa Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.
     - ANGALIA MATOKEO - Kwa taarifa yako: Bofya sehemu hii ili uone ni swali gani katika utafiti linalorejelea eneo fulani la matokeo.
     - ANGALIA UZANI - Kwa taarifa yako: Bofya sehemu hii ili uone jinsi kila swali linavyopata alama na uzani.
     - **TUMA (BLUU)** - Bonyeza sehemu hii ili utume data yako pindi unapokamilisha fomu ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia.

  b. Bonyeza "ANGALIA MAJIBU" ili ufungue fomu kwa ajili ya kuanza kurekodi/kuongeza data yako. Fomu moja inawakilisha Utafiti mmoja wa Kuchunguza kwa Kuangalia. Kwa mfano: Ikiwa ulikamilisha tafiti mbili za Kuchunguza kwa Kuangalia katika muktadha wako, utahitaji kujaza fomu mara mbili.

  c. Ingiza data kutoka kwa Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia katika fomu iliyotolewa;
     - Weka tarehe ya utafiti ukitumia mojawapo ya miundo ifuatayo, "SIKU/MWEZI/MWAKA" au "MWEZI/SIKU/MWAKA".
     - Kwa mfano: Ikiwa utafiti ulifanywa tarehe 29 Juni 2020, unaweza kuandika ama: 29/06/2020 au 06/29/2020.
     - Iwapo hukujibu swali lolote kati ya hayo, chagua "NA (Not Applicable)" kwa swali hilo. Kufanya hivi moja kwa moja kutatenga jibu, kuondoa swali hili ili lisihesabiwe na hakutaathiri alama yako ya jumla. Ikiwa ulichagua "Sijui" katika mojawapo ya maswali hayo, chagua "Sijui" (au "NA" ikiwa hilo ndilo chaguo jingine pekee lililopo).

  d. Baada ya kuongeza data yako yote ya Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia, bonyeza kitufe cha bluu cha **"TUMA"** kilicho sehemu ya juu. Ukifanya hivi, utaona kisanduku cha ujumbe: ***"Una uhakika uko tayari kutuma? Ukituma, hatua hii itaondoa majibu yote katika fomu na kuiweka tayari kutumiwa kuweka seti mpya ya data."*** Iwapo umekagua data yako, unakubali kuwa ni sahihi na kamili, na uko tayari kutuma fomu hii, bonyeza "Ndiyo." Hata hivyo, ikiwa ungependa kuiangalia tena, bonyeza "Hapana" na ukague data uliyoweka, kabla ya kubonyeza "Tuma" na "Ndiyo." *Muhimu: Pindi unapobonyeza "Ndiyo" ili kutuma data yako, huwezi kupata fomu tena ili uibadilishe. Utahitaji kuanza tena na kufuta data ghafi isiyo sahihi kutoka kwenye kichupo cha DATA.*

  e. Baada ya kutuma data yako ya utafiti, utapewa kitambulisho cha utafiti, ambacho unaweza kutumia kutambua utafiti katika michoro ya Barometa (Vichupo vya 3 na 4).

- ☐ **Kichupo cha 4. Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi**: Tumia kichupo hiki **kuingiza data yote** iliyotoka kwa Tafiti za Mtazamo wa Wafanyakazi:

  a. Kuna vitufe 5 katika sehemu ya juu ya Kichupo:

- **WEKA UPYA FOMU (NYEKUNDU)** - Bonyeza sehemu hii ikiwa unataka kufuta data iliyo kwenye fomu na uanze tena.
- ANGALIA MAJIBU - Hii ndiyo fomu kuu ambapo utarekodi/kuongeza data yako yote kutoka kwa Tafiti zako za Mtazamo wa Wafanyakazi.
- *ANGALIA MATOKEO - Kwa taarifa yako: Bofya sehemu hii ili uone ni swali gani katika utafiti linalorejelea eneo fulani la matokeo.*
- *ANGALIA UZANI - Kwa taarifa yako: Bofya hii ili kuona jinsi kila swali linavyopata alama na uzani.*
- **TUMA (BLUU)** - Bonyeza sehemu hii ili utume data yako pindi unapokamilisha fomu.

b. Bonyeza "ANGALIA MAJIBU" ili ufungue fomu kwa ajili ya kuanza kurekodi/kuongeza data yako. Fomu moja inawakilisha Utafiti wa Maoni ya Mfanyakazi mmoja. Kwa mfano: Ikiwa kulikuwa na Tafiti nane za Mtazamo wa Wafanyakazi zilizokamilishwa katika muktadha wako, utahitaji kujaza fomu hii mara nane.

c. Ingiza data yako kutoka kwa Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi kwenye fomu iliyotolewa:

- **Weka tarehe ya utafiti ukitumia mojawapo ya miundo ifuatayo:** "SIKU/MWEZI/MWAKA" au "MWEZI/SIKU/MWAKA".
- **Kwa mfano:** Ikiwa utafiti ulifanywa tarehe 29 Juni 2020, unaweza kuandika ama: 29/06/2020 au 06/29/2020.
- Iwapo hukujibu swali lolote kati ya hayo, chagua "NA (Not Applicable)" kwa swali hilo. Kufanya hivi moja kwa moja kutatenga jibu, kuondoa swali hili ili lisihesabiwe na hakutaathiri alama yako ya jumla. Ikiwa hukujua/hujui jibu la swali lolote kati ya hayo, chagua "Sijui" (au "NA" ikiwa hilo ndilo chaguo jingine pekee lililopo).
- Iwapo kuna maswali yoyote ambayo "YALIRUKWA," hakikisha umefanya vivyo hivyo kwenye fomu. Kufanya hivi moja kwa moja kutatenga jibu, kuondoa swali hili ili lisihesabiwe na hakutaathiri alama yako ya jumla.

d. Mara tu unapoongeza data yako yote ya Utafiti huo wa Mtazamo wa Wafanyakazi, bonyeza kitufe cha bluu cha **"TUMA"** kilicho hapo. Ukifanya hivi sanduku la ujumbe litaonekana: ***"Una uhakika uko tayari kutuma? Ukituma, hatua hii itaondoa majibu yote katika fomu na kuiweka tayari kutumiwa kuweka seti mpya ya data."*** Iwapo umekagua data yako, unakubali kuwa ni sahihi na kamili, na uko tayari kutuma fomu hii, bonyeza "Ndiyo." Hata hivyo, ikiwa ungependa kuangalia tena, bonyeza "Hapana" na ukague data uliyoweka, kabla ya kubonyeza "Tuma" na "Ndiyo." *Muhimu: Pindi unapobonyeza "Ndiyo" ili kutuma data yako, huwezi kupata fomu tena ili uibadilishe. Utahitaji kuanza tena, na kufuta data ghafi isiyo sahihi kutoka kwenye kichupo cha DATA.*

e. Baada ya kutuma data yako ya utafiti, utapewa kitambulisho cha utafiti, ambacho unaweza kutumia kutambua utafiti katika michoro ya Barometa (Vichupo vya 3 na 4).

**4. Kuangalia alama zako za Barometa**

☐ **Kichupo cha 6. Barometa, na Kichupo cha 7. Barometa kwa Mada:** Vichupo hivi viwili hukuruhusu kuikagua data kikamilifu.

- o **Kichupo cha 6.** hukuonyesha alama ya jumla ya Barometa kwa maudhui yako na kila alama kwa maeneo manne ya matokeo.
- o **Kichupo cha 7.** hukuonyesha alama binafsi za mada 18 mahususi ndani ya zana zote mbili za kukusanya data ili kukupa alama za kina kwa uchanganuzi wa kina zaidi.
    - Kwa vichupo vyote viwili, unaweza kutumia visanduku vya chaguo vilivyo upande wa kulia ili kuchagua nchi au kitambulisho mahususi cha utafiti ili uone alama hizo mahususi. Unaweza pia kutumia kisanduku cha chaguo cha "Mahali" cha Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia ili uone alama za maeneo tofauti. Kwa Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi, chagua "Jinsia" ili uone alama za wanaume au wanawake.

# Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi: Jinsi ya Kuweka Alama

Tumia mwongozo huu ukusaidie kuweka alama katika kila utafiti utakaofanya

| # | Swali | Alama |
|---|---|---|
| **Kujitolea na Uwajibikaji** | | |
| 1 | Kwa kipimo cha 1 (Ni muhimu sana) hadi 5 (Si muhimu hata kidogo), suala la unyanyasaji wa kingono lina umuhimu kiasi gani katika shirika lako?<br>[1. Ni muhimu sana] [2. Ni muhimu kiasi] [3. Sina maoni yoyote] [4. Si muhimu sana] [5. Si muhimu hata kidogo] | 1 = alama 2<br>2 = alama 1.50<br>3 = alama 1<br>4 = alama 0.50<br>5 = alama 0<br>***UZITO MARADUFU** |
| 2 | Kwa kipimo cha 1 (Ni muhimu sana) hadi 5 (Si muhimu hata kidogo), suala la udhalilishaji na dhuluma ya kingono lina umuhimu kiasi gani katika shirika lako?<br>[1. Ni muhimu sana] [2. Ni muhimu kiasi] [3. Sina maoni yoyote] [4. Si muhimu sana] [5. Si muhimu hata kidogo] | 1 = alama 2<br>2 = alama 1.50<br>3 = alama 1<br>4 = alama 0.50<br>5 = alama 0<br>***UZITO MARADUFU** |
| 3 | Ikiwa mtu fulani atashtakiwa au atatekeleza tendo la unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, shirika langu litachukua wajibu wa kuhakikisha kuwa mwathiriwa/manusura aliyeripoti tukio hilo amelindwa.<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Singependa kujibu (NA) | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>NA = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 4 | Ikiwa mtu fulani atashtakiwa au atatekeleza tendo a unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, shirika langu litachukua wajibu wa kuhakikisha kuwa mtu huyo amewajibikia kitendo hicho.<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Singependa kujibu (NA) | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>NA = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| **Utaratibu wa Kuwasilisha Malalamiko: Urahisi, Usiri na Hatari** | | |
| 5. | Kwa kipimo cha 1 (ninahimizwa sana) hadi 5 (sihimizwi hata kidogo), shirika lako limekuhimiza kwa kiasi gani kuripoti madai ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, iwapo yatatokea na wakati yanatokea?<br>[1. Ninahimizwa sana] [2. Ninahimizwa kiasi] [3. Sina maoni yoyote] [4. Sihimizwi sana] [5. Sihimizwi hata kidogo] | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Kwa kipimo cha 1 (nina imani sana) hadi 5 (sina imani hata kidogo), una imani kwa kiasi gani kuwa taratibu za kuripoti visa vya unyanyasaji wa kingono katika shirika lako zinaweza kuwa na matokeo ya haki?<br>1. Nina imani sana \| 2.Nina imani kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Sina imani sana \| 5. Sina imani hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 7. | Kwa kipimo cha 1 (nina imani sana) hadi 5 (sina imani hata kidogo), iwapo utaripoti kisa cha unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, una imani kwa kiasi gani kuwa malalamiko yako yatasalia siri?<br>1. Nina imani sana \| 2.Nina imani kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Sina imani sana \| 5. Sina imani hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 8. | Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), utakuwa na wasiwasi kiasi gani kujumuisha jina lako iwapo utawasilisha malalamiko kuhusu unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?<br>1. Sina wasi-wasi wowote \| 2.Sina wasi-wasi sana \| 3. Sina ma-oni yoyote \| 4. Nina wasiwasi kiasi \| 5. Nina wasiwasi sana | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 9. | Je, ushawahi kuwasilisha malalamiko rasmi kuhusu unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana (Ruka hadi swali la 11) | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 10. | Ikiwa jibu lako la swali ya 9 ni Ndiyo, kwa kipimo cha 1 (niliridhika kabisa) hadi 5 (sikuridhika hata kidogo), uliridhika kwa kiasi gani na jinsi shirika lilivyoshughulikia malalamiko yako?<br>1. Niliridhika kabisa \| 2.Niliridhika kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Sikuridhika sana \| 5. Sikuridhika hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 11. | Je, ushawahi kuwa shahidi katika malalamiko rasmi ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 12. | Je, wewe au mfanyakazi mwenzako mshawahi kutuma malalamiko yasiyo rasmi kuhusu unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono? (Yasiyo rasmi inamaanisha kupitia njia nyingine kando na zile zilizobainishwa kama rasmi)<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana (Ruka hadi swali la 14) | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 13. | Ikiwa jibu lako la swali la 12 ni Ndiyo, kwa kipimo cha 1 (nilihimizwa sana) hadi 5 (sikuhimizwa hata kidogo), shirika lako lilikuhimiza kwa kiasi gani uwasilishe malalamiko rasmi?<br>1. Nilihimizwa sana \| 2. Nilihimizwa kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Sikuhimizwa sana \| 5. Sikuhimizwa hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 14. | Kwa kipimo cha 1 (inawezekana sana) hadi 5 (haiwezekani hata kidogo), kwa maoni yako inawezekana kwa kiasi gani kwa mtu kufutwa kazi ikiwa malalamiko ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono yatawasilishwa dhidi yake?<br>1. Inawezekana sana \| 2. Inawezekana kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Haiwezekani sana \| 5. Haiwezekani hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |

15. Kwa kipimo cha 1 (unaweza kuathiri sana) hadi 5 (hauwezi kuathiri hata kidogo), uwezekano wa unyanyapaa ndani ya shirika lako unaweza kuathiri kwa kiasi gani uamuzi wako wa kuripoti (au kutoripoti) kisa cha unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Unaweza kuathiri sana | 2. Unaweza kuathiri kiasi | 3. Sina maoni yoyote | 4. Hauwezi kuathiri sana | 5. Hauwezi kuathiri hata kidogo |

1 = alama 0
2 = alama 0.25
3 = alama 0.50
4 = alama 0.75
5 = alama 1

16. Kwa kipimo cha 1 (unaweza kuathiri sana na siwezi kuripoti) hadi 5 (hauwezi kuathiri hata kidogo na ninaweza kuripoti), uwezekano wa ulipizaji kisasi ndani ya shirika lako unaweza kuathiri kwa kiasi gani uamuzi wako wa kuripoti (au kutoripoti) kisa cha unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Unaweza kuathiri sana na siwezi kuripoti | 2. Unaweza kuathiri kiasi na sina uhakika ka ninaweza kuripoti | 3. Sina maoni yoyote | 4. Hauwezi kuathiri na labda ninaweza kuripoti | 5. Hauwezi kuathiri hata kidogo na ninaweza kuripoti |

1 = alama 0
2 = alama 0.25
3 = alama 0.50
4 = alama 0.75
5 = alama 1

17. Kulingana na uliyoona, kwa kipimo cha 1 (wamechukua hatua) hadi 5 (wameficha kimakusudi), usimamizi wa shirika lako umeshughulikia vipi uvumi wa kuwepo kwa unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono? Ikiwa HUJUI jibu, RUKA hadi swali la 18.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mipango yenye utaratibu imewekwa | 2. Mipango fulani imewekwa, lakini kulingana na tukio | 3. Sina maoni yoyote | 4. Hakuna hatua zinazochukuliwa | 5. Kumekuwa na juhudi za kimakusudi za kuficha tukio |

1 = alama 1
2 = alama 0.75
3 = alama 0.50
4 = alama 0.25
5 = alama 0

Sijui = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa

18. Je, unahisi kuwa una mwongozo wa kutosha kuhusu taratibu na njia za kuripoti madai ya unyanyasaji au dhuluma ya kingono?

☐ Ndiyo

☐ Hapana

☐ Sijui

Ndiyo = 1
Hapana = 0
Sijui = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa

19. Je, shirika lako lina sera zozote za kuwalinda wapiga ripoti? (Mpiga ripoti: sera ya kuwalinda watu, wakiwemo wafanyakazi, ambao wataripoti visa vya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono dhidi ya kisasi)

☐ Ndiyo, zipo na ninazifahamu

☐ Hapana, sijui kama zipo (Ruka hadi swali la 21)

Ndiyo = 1
Hapana = 0

20. Ikiwa jibu lako la swali la 19 ni NDIYO, kwa kipimo cha 1 (nimelindwa sana) hadi 5 (sijalindwa hata kidogo), unajihisi kwa kiasi gani kuwa umelindwa na sera za shirika lako za wapiga ripoti, ikiwa utaripoti madai ya kunyanyaswa au kudhulumiwa kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Nimelindwa sana | 2. Nimelindwa kiasi | 3. Sina maoni yoyote | 4. Sijalindwa sana | 5. Sijalindwa hata kidogo |

1 = alama 1
2 = alama 0.75
3 = alama 0.50
4 = alama 0.25
5 = alama 0

**Hatua Zinazochukuliwa na Shirika**

| | | |
|---|---|---|
| 21. | Je, unajua mwathiriwa/manusura yeyote wa unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono ambaye alipata huduma za kushughulikia ukatili wa kijinsia kama vile ushauri nasaha au matibabu?<br>☐ Ndiyo, walipewa huduma hizi<br>☐ Hapana, hawakupewa huduma hizi (Ruka hadi swali la 24)<br>☐ Sijui/sina uhakika (Ruka hadi swali la 24) | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>Sijui/sina uhakika = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 22. | Ikiwa jibu lako la swali la 21 ni NDIYO, mwathiriwa/manusura alipewa huduma hizo za kushughulikia ukatili wa kijinsia papo hapo (kama sehemu ya mazungumzo ya kufichua)?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui/sina uhakika | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>Sijui/sina uhakika = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 23. | Ikiwa jibu lako la swali la 21 ni NDIYO, je, mwathiriwa/manusura wa unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono alisaidiwa katika kujifanyia uamuzi kuhusu huduma na usaidizi aliouhitaji?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui/sina uhakika | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0<br>Sijui/sina uhakika = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |

## Kushirikishwa kwa Wanawake katika Kutunga na Kutekeleza Sera

**24.** Kwa maoni yako, kwa kipimo cha 1 (hushughulikiwa sana) hadi 5 (hayashughulikiwi kamwe), masuala ya usalama na ulinzi wa wanawake yanashughulikiwa kwa kiasi gani na sera na desturi za usalama na ulinzi zilizopo katika shirika lako? Ikiwa HUJUI jibu lake, RUKA hadi swali ya 25.

| 1. Hushughulikiwa sana | 2. Hushughulikiwa kiasi, japo kuna sehemu zinazohitaji kuboreshwa | 3. Sina maoni yoyote | 4. Hayashughulikiwi sana; kuna mapengo mengi | 5. Hayashughulikiwi kamwe |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

1 = alama 2
2 = alama 1.50
3 = alama 1
4 = alama 0.50
5 = alama 0
Sijui = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa
***UZITO MARADUFU**

**25.** Kwa maoni yako, kwa kipimo cha 1 (hushughulikiwa sana) hadi 5 (hayashughulikiwi kamwe), kukija ni masuala ya usalama na ulinzi, ni kwa kiasi gani ukweli na hali wanazopitia wanawake huzingatiwa katika sera na desturi zilizopo katika shirika lako? Ikiwa HUJUI jibu lake, RUKA hadi swali ya 26.

| 1. Hushughulikiwa sana | 2. Hushughulikiwa kiasi, japo kuna sehemu zinazohitaji kuboreshwa | 3. Sina maoni yoyote | 4. Hayashughulikiwi sana; kuna mapengo mengi | 5. Hayashughulikiwi kamwe |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

1 = alama 2
2 = alama 1.50
3 = alama 1
4 = alama 0.50
5 = alama 0
Sijui = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa
***UZITO MARADUFU**

**26.** Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), ni mara ngapi ambazo viongozi/ wasimamizi/walinda usalama hukuuliza maoni yako kuhusu mahitaji ya usalama na ulinzi ya wafanyakazi wa kike?

| 1. Kila wakati | 2. Mara kwa mara | 3. Sina maoni yoyote | 4. Nadra | 5. Kamwe |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

1 = alama 1
2 = alama 0.75
3 = alama 0.50
4 = alama 0.25
5 = alama 0

| | | |
|---|---|---|
| 27. | Je, usimamizi wa shirika lako ushawahi kukuuliza maoni yako kuhusu wasiwasi wa wanawake kuhusu ulinzi wakati wanasafiri au kutembea, wakati wa kubuni sera za kutembea na kusafiri?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0 |
| 28. | Je, usimamizi wa shirika lako ushawahi kukuuliza maoni yako kuhusu wasiwasi na mahitaji ya wanawake wakati wa kubuni sera za malazi?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0 |
| 29. | Je, usimamizi wa shirika lako ushawahi kukuuliza maoni yako kuhusu wasiwasi wowote wanawake walio nao kuhusiana na ulinzi na faragha wakati wa kubuni sera za ofisini?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0 |
| 30. | Ikiwa umejibu NDIYO katika mojawapo ya maswali kati ya swali la 27 hadi la 29, je, kuna yoyote kati ya maoni au mapendekezo ambayo umetoa ambayo yamejumuishwa katika desturi na sera za usalama na ulinzi? Ikiwa HUKUJIBU NDIYO katika mojawapo ya maswali hayo, RUKA hadi swali la 31.<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0 |
| **Utambuzi wa Hatari** | | |
| 31. | Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), unahisi kwa kiasi gani kuwa shirika lako linachukua hatua za kushughulikia usalama na ulinzi wa wafanyakazi wenzako wa kike?<br>1. Kila wakati \| 2. Mara kwa mara \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Nadra \| 5. Kamwe | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 32. | Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), unahisi kwa kiasi gani kuwa shirika lako linaweka wafanyakazi wenzako wa kike katika hatari yoyote ya kunyanyaswa kingono?<br>1. Kila wakati \| 2. Mara kwa mara \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Nadra \| 5. Kamwe | 1 = alama 0<br>2 = alama 0.25<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.75<br>5 = alama 1 |
| 33. | Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), unahisi kwa kiasi gani kuwa shirika lako linazuia au kupunguza hatari za wanawake wanaonufaika na kazi yenu kunyanyaswa, kudhalilishwa na kudhulumiwa kingono?<br>1. Kila wakati \| 2. Mara kwa mara \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Nadra \| 5. Kamwe | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 34. | Je, ushawahi kujihisi mwenye woga au unatishwa na wafanyakazi wanaolinda usalama?<br>☐ Ndiyo<br>☐ hapana | Ndiyo = 1<br>hapana = 0 |

| | | |
|---|---|---|
| 35. | Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), una wasiwasi kiasi gani kuhusu uchunguzi wa kuthibitisha ambao shirika lako linafanyia wafanyakazi wanaolinda usalama? Uwapo HUNA HABARI kuhusu uchunguzi wowote wa kuthibitisha, RUKA hadi swali la 36.<br><br>1. Sina wasiwasi wowote \| 2.Sina wasiwasi sana \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Nina wasiwasi kiasi \| 5. Nina wasiwasi sana | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0<br>Huna habari = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 36. | Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), una wasiwasi wowote kuhusu uchunguzi wa kuthibitisha ambao shirika lako linafanyia madereva na wafanyakazi wengine? Uwapo HUNA HABARI kuhusu uchunguzi wowote wa kuthibitisha, tafadhali chagua NA.<br><br>1. Sina wasiwasi wowote \| 2.Sina wasiwasi sana \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Nina wasiwasi kiasi \| 5. Nina wasiwasi sana | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0<br>Huna habari = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 37. | Je, shirika lako hukupatia mbinu ya usafiri kama sehemu ya kazi yako?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana (Ruka hadi Swali la 39) | Ndiyo = RUKA hadi Swali la 38<br>Hapana = RUKA hadi Swali la 39 |
| 38. | Ikiwa umejibu NDIYO katika Swali la 37, kwa kipimo cha 1 (nina wasiwasi sana) hadi 5 (sina wasiwasi wowote), una wasiwasi kiasi gani kuhusu uwezekano wa kunyanyaswa kingono unapotumia mbinu ya usafiri uliyopewa na shirika lako? (Ruka hadi Swali la 40)<br><br>1. Nina wasiwasi sana \| 2. Nina wasiwasi kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4.Sina wasiwasi sana \| 5. Sina wasiwasi wowote | 1 = alama 0<br>2 = alama 0.25<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.75<br>5 = alama 1 |
| 39. | Ikiwa umejibu HAPANA katika Swali la 37, iwapo utahitaji shirika lako likupatie mbinu ya usafiri ili ujihisi salama zaidi, unaonelea kama watakupatia ikiwa utawaomba?<br>☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | Ndiyo = 1<br>Hapana = 0 |
| 40. | Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), una wasiwasi wowote wa kusafiri na wafanyakazi wenza wa kiume? Ikiwa HUSAFIRI na wafanyakazi wenza wa kiume, RUKA hasi swali la 41.<br><br>1. Sina wasiwasi wowote \| 2.Sina wasiwasi sana \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Nina wasiwasi kiasi \| 5. Nina wasiwasi sana | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0<br>Huwa husafiri na wafanyakazi wenza wa kiume = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |

| | | |
|---|---|---|
| 41. | Kwa kipimo cha 1 (nina uhakika kabisa) hadi 5 (sina uhakika hata kidogo), iwapo utahitaji kuomba aina fulani ya malazi (k.m., hoteli au malazi tofauti) ili kupunguza hatari ya kunyanyaswa au kudhulumiwa kingono, una uhakika kiasi gani kuwa shirika lako litakubali ombi lako? Ikiwa hutumii au HUHITAJI malazi kama sehemu ya kazi yako, RUKA hasi swali la 42.<br><br>1. Nina uhakika kabisa \| 2.Nina uhakika kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Sina uhakika sana \| 5. Sina uhakika hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0<br>Huhitaji malazi. = RUKA swali halitahesabiwa/ halitajumuishwa |
| 42. | Kwa kipimo cha 1 (salama kabisa) hadi 5 (siko salama hata kidogo), uhajihisi salama kwa kiasi gani ukiwa mahali unapofanyia kazi (ofisini, eneo la kazini, katika jengo) kukija ni suala la kunyanyaswa, kudhalilishwa na kudhulumiwa kingono?<br><br>1. Salama kabisa \| 2. Salama kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Siko salama sana \| 5. Siko salama hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |
| 43. | Kwa kipimo cha 1 (salama kabisa) hadi 5 (siko salama hata kidogo), uhajihisi salama kwa kiasi gani unapotembea katika eneo la dharura kukija ni suala la kunyanyaswa kingono?<br><br>1. Salama kabisa \| 2. Salama kiasi \| 3. Sina maoni yoyote \| 4. Siko salama sana \| 5. Siko salama hata kidogo | 1 = alama 1<br>2 = alama 0.75<br>3 = alama 0.50<br>4 = alama 0.25<br>5 = alama 0 |

# Dokezo la Mwongozo wa Uchanganuzi wa Data ya Matini la Majadiliano ya Kikundi na Mahojiano ya Watoa Taarifa muhimu

Kuna hatua saba za kufuata ili utoe uchanganuzi wa data yako ya matini ya ubora ya kisimulizi. Unaweza kupitia hatua zote saba kwa mpangilio, au unaweza kuchagua kurudi kwenye hatua 1-5 wakati wa mchakato ili urudie au ukague hatua zenyewe. Fanya kile kinachokufaa zaidi unapopitia hatua ya mwisho.

**1. Kusanya data yako**

- ☐ Ili kuchanganua Majadiliano yako ya Kikundi Lengwa (FGD), utahitaji kumbukumbu zako za FGD na ramani za jamii ambazo zilichorwa wakati wa majadiliano.
- ☐ Ili kuchanganua Mahojiano yako ya Watoa Taarifa Muhimu (KII), utahitaji kumbukumbu zako za KII na hati nyingine zozote ulizotoa wakati wa mahojiano haya.

**2. Ijue data yako**

- ☐ Wewe na timu yako mnapaswa kusoma madokezo yenu yote kwa makini, kwa lengo la kuizamia data.
- ☐ Soma na usome tena madokezo, pamoja na ramani za jamii ikiwa unazo. Jisikie huru kuandika dhana au mawazo yoyote ya mwanzo kuhusu data unaposoma. Unaweza kuchukua karatasi ya chati ya kupindua ili uanze kunakili pointi hizi za mwanzo kutoka kwa timu.
- ☐ Unaposoma, anza kuchagua dondoo fupi kutoka kwa washiriki ambazo zinaelezea vyema jambo na ambazo zitakuwa nyongeza muhimu kwa mapendekezo na utetezi wako (angalia *Sehemu ya 4. Utetezi na Usambazaji*). Unaweza kuchagua kutozitumia baadaye lakini ni muhimu kuwa na dondoo hizo kwa sasa.

**3. Teulia data yako misimbo**

Katika hatua hii inayofuata, utaandalia data yako msimbo wa rangi au kitambulishi:

- ☐ Kuweka misimbo kunamaanisha kuangazia sehemu za data yako (kutoka kwenye FGD au KII) ambazo zinakuvutia zaidi au zenye maana kulingana na zinavyohusiana na matokeo na mada za Barometa.
- ☐ Sehemu hizi za data mara nyingi huwa kauli au sentensi fupi. Kisha, amua vitambulishi ("misimbo") vya kuifafanua, huku ukiweka rangi ili kuvifanya vionekane vizuri (tumia kalamu ya kutia alama kupigia mstari au kuweka nukta kando ya maandishi).
- ☐ Huu hapa mfano mfupi kutokana na mfano wa FGD. Katika mfano huu, unaweza kuona jinsi tungo tofauti zimeangaziwa (safu wima ya kushoto). Zimebainishwa kwa vitambulishi rahisi (safu wima ya kulia), pamoja na misimbo ya rangi inayozishirikisha. Kila kitambulishi kinaelezea wazo, hisia, hali na maoni yaliyotolewa katika sehemu hiyo ya maelezo ya FGD:

| Dokezo la FGD (mfano pekee) | Kitambulishi na msimbo wa rangi |
|---|---|
| "…Kwa kawaida wanaume huwahadaa wasichana wakisema watawapa zawadi, pesa lakini hizi ni ahadi tupu. Wanaume hawa ni wanaojitolea kufanyia kazi NGO katika jamii. Waliwadanganya wasichana wakisema kwamba wangewapa vitu wanavyohitaji kama vile chakula au vocha za kupata bidhaa. Wanajua wasichana wanahitaji vitu hivi. Wanawafanya wafanye ngono nao na baada ya hapo hawawapi chochote. Hili kawaida hufanyika usiku, nyuma ya soko. Wasichana pia wanasumbuliwa ili washiriki kingono wakati mwingine. Wanaume hujilazimisha kwao karibu na vyoo. Wasichana wakitaka kutoka, milango haifanyi kazi vizuri na hakuna taa, kuna giza. Tunaogopa kuripoti kwa kuchelea kulaumiwa…" | **Udhalilishaji wa kingono**<br>**Wahusika kutoka NGO**<br>**Kutokuwa na imani katika kutoa taarifa**<br>**Jamii si salama wakati wa usiku**<br>**Dhuluma ya kingono**<br>**Maeneo ya usafi hayafanyi kazi**<br>**Hakuna maeneo ya umma kwa ajili ya usalama** |

- ☐ Ikihitajika, zingatia maswali haya elekezi unapokagua madokezo yako ili kukusaidia kunakili vipande muhimu vya habari:
  - o Kipi kinasemwa?
  - o Je, kinawakilisha nini? Kinawakilisha nani?
  - o Ni maoni gani au hali zipi zinawasilishwa?
  - o Je, zinatoa mfano wa nini?
  - o Kipi kinaendelea? Ni matukio au mambo gani yanayotokea? Ni nini kinaendelea kwa wanawake na wasichana?
  - o Je, ni kitu gani kinaendelea?
  - o Je, kuna maeneo mahususi au makundi ya usaidizi wa kibinadamu yanayojadiliwa?

Usisahau pia kuangalia ramani za jamii zilizochorwa na wanawake na wasichana. Zitakupa maelezo mengi kuhusu uhalisia wanaoupitia.

Baada ya kupitia madokezo yako na kuweka vitambulishi ("misimbo") na rangi, nenda kwenye hatua inayofuata.

### 4. Andaa mada (huku ukiweka misimbo yako ya rangi pamoja)

Katika hatua hii, utaweka vitambulishi vyako ("misimbo") katika vikundi na mada tofauti.

- ☐ Kagua vitambulishi vyako vyote na uanze kuviweka katika vikundi kulingana na mada zinazofanana au kushirikiwa. Utapata majina ya kuzipa mada hizi unapoanza kuangazia vitambulishi vyako. Katika kila mada unaweza kujumuisha vitambulishi rudufu au vinavyofanana.
- ☐ Unaweza kuwa na karatasi au chati za kupindua zisizo na maandishi ili kuwakilisha mada ambazo chini yake utaweka vitambulishi vyako.
- ☐ Lenga kuwa na kati ya mada 6-8 ili kuepuka kuishia na data nyingi.
- ☐ Unaweza kuzingatia maeneo manne ya matokeo ya Barometa na Nadharia ya Mabadiliko ili yakusaide kubainisha mada husika kutoka kwenye data.
- ☐ Unapotengeneza mada kwa vitambulisho vyako, unaweza pia kuanza kuweka manukuu kwenye mada husika.
- ☐ Kulingana na mfano ulio hapa juu, hivi ndivyo mada kadhaa za mwanzo zinavyoweza kuwa:

| Vitambulishi na misimbo ya rangi | Mada zinazojitokeza |
|---|---|
| Jamii si salama wakati wa usiku<br>Hakuna vistawishi<br>Vistawishi muhimu havifanyi kazi | Mazingira ya kibinadamu |
| Udhalilishaji wa kingono<br>Dhuluma za kingono<br>Wahusika kutoka NGO | Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana |

Baada ya kupitia vitambulishi vyako vyote ("misimbo") na kuziweka pamoja katika mada, nenda kwenye hatua inayofuata.

### 5. Kagua mada zako

Katika hatua hii, "rudi nyuma" na uhakiki mada zako.

- ☐ Fikiria kama unataka **kubadilisha, kuchanganya, kugawanya, kusafisha** au **kutupa** mada zozote.
- ☐ Rudi kwenye ramani zako za jamii:
- o Je, mada zako zinaonyesha kile ambacho wanawake na wasichana walishiriki kupitia ramani hizi?
- ☐ Jiulize:
- o Je, tunakosa chochote?
- o Je, mada hizi zipo katika data yetu inayotokana na FGD/KII? Je, ni sahihi?
- o Je, tunaweza kubadilisha nini ili kufanya mada hizi ziafiki vizuri zaidi?
- o Je, tunahakikisha kuwa sauti za wanawake na wasichana zinapazwa na ni wazi vya kutosha?

Baada ya kukagua mada zako na kufanya marekebisho au mabadiliko yoyote, nenda kwenye hatua inayofuata.

### 6. Bainisha mada zako

Hatua hii inahusisha kuboresha na kufafanua mada zako.

- ☐ Angalia mada zako zote na ujadili jinsi zinavyohusiana katika kubuni simulizi moja ya matokeo yako. Je, mada zinasimulia hadithi gani unapozichukulia kwa pamoja? Ikiwa kuna mapungufu yoyote, kutofautiana au sehemu ambazo haziambatani, endelea kuboresha mada mahususi (au hata kupitia upya hatua ya 2 na 3).
- ☐ Kisha, kwa kila mada, buni ufafanuzi rahisi na wazi wa kutumia unaoelezea maana na yaliyo kwenye mada husika. Fikiria hasa maana ya kila mada na jinsi inavyokusaidia kuelewa data (na jinsi mada hizi zitakuwa sehemu muhimu zaidi katika utetezi wako).
- ☐ Ikiwa bado huna, buni jina fupi, linalojieleza, linaloeleweka kwa kila mada.

Mara tu unaporidhika na hadithi ya pamoja inayojitokeza kwenye mada; jinsi mada zinazoingiliana; kila mada binafsi; na yaliyomo katika kila mojawapo (vitambulishi na nukuu zozote za moja kwa moja kutoka kwa washiriki), nenda kwenye hatua ya mwisho.

### 7. Kujumlisha uchambuzi

Hatimaye, jumlisha uchanganuzi huu wote katika uandishi unaojumuisha uchanganuzi wako wa mada kutoka katika matokeo ya FGD na KII.

- Kwa vile utakuwa ukitumia matokeo haya kukamilisha na kuongeza maelezo ya simulizi, kina na vidokezo kwenye alama za Barometa, unaweza kutumia kiolezo kilicho hapa chini katika uandishi wako. Kiolezo hiki kimeundwa kwa kuzingatia maeneo manne ya matokeo kutokana na Nadharia ya Mabadiliko ambayo

Barometa inatumia kupata alama. Kitakuwezesha kuweka uchanganuzi huu wa mada kwa haraka zaidi na alama zako za upimaji kwenye maeneo hayo manne ya matokeo; pia kuna sehemu tofauti ya mada ambazo unahisi ni mtambuka, zinajitegemea au za kipekee.

- Kwa uandishi wako, amua ni mada zipi zinafaa, wapi na vipi. Fikiria kuhusu:
  - Jinsi inavyohusiana na eneo la matokeo au kwa nini ni ya kipekee/inajitegemea au mtambuka;
  - Tulichofahamu kutokana na uchambuzi na FGD/KII;
  - Ni mapungufu, changamoto, mianya na kutofanikiwa kupi unafahamu kutokana na uchambuzi wa mfumo wa kibinadamu kwa wanawake na wasichana;
  - Tuko mbali kiasi gani kufikia matokeo hayo na ni vikwazo vipi vinazuia kuvifikia;
  - Inatoa picha gani kuhusu kile kinachofanya kazi au kilichoboreshwa kwa wanawake na wasichana?
  - Kitu gani kinahitaji kubadilishwa? Ni nini wanawake na wasichana wanatuambia kinahitaji kubadilika?
  - Je, ni nini cha kipekee na nini kitakuwa cha thamani sana katika utetezi wetu?

### Mfano wa kiolezo cha kuandika

| | |
|---|---|
| **Matokeo ya 1.** Wanawake na wasichana waamini na kupata huduma za usaidizi salama, kwa siri na kwa uwajibikaji wanapopatwa na ukatili wa kijinsia (UWAKI), ikiwa ni pamoja na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. | **Matokeo ya 2.** Wanawake na wasichana kutoka katika jamii zilizoathiriwa waweze kufikia na wawe na udhibiti sawa wa huduma na rasilimali za kibinadamu. |
| **Matokeo ya 3.** Wahudumu wa usaidizi wa kibinadamu watumie mamlaka vyema na waheshimu na kuthamini wanawake na wasichana na jamii zilizoathirika. | **Matokeo ya 4.** Mashirika ya kibinadamu yawawajibishe wafanyakazi ili kukabili dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. |

## Sehemu ya 4

# Utetezi na Usambazaji



Picha na A Oberstadt, IRC

# Muhtasari: Kutoa alama

**Barometa hutumia "mfumo wa taa za barabarani"** (Rangi Nyekundu, ya Chungwa, ya Manjano na ya Kijani) ili kuashiria hali ya usaidizi wa kibinadamu katika ukatili wa kijinsia (UWAKI) na dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono katika maeneo manne ya matokeo.

Katika kila mojawapo ya maeneo haya manne, kuna vigezo tofauti ambavyo vinatathminiwa kimoja kimoja. Kila kigezo kina mfululizo wa vipengele ambavyo vitapatiwa alama kutoka 1-4 (Nyekundu hadi Kijani), kulingana na taarifa iliyokusanywa kutokana na zana nne za kukusanya data: Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia, Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD), Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi na Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII).




Kutoka kwenye alama hizi, Barometa itatoa majibu mawili: ukadiriaji wa binafsi wa kila mojawapo ya maeneo hayo manne ya matokeo kutoka nyekundu hadi kijani; na, kujumlisha alama kutoka maeneo yote manne, alama ya jumla ya usaidizi wa kibinadamu unaotathminiwa.

- *Zana za Kutoa Alama zinaweza kupatikana katika Sehemu ya 4: Zana za Utetezi.*

# Kuanzia Kuweka Alama hadi Utetezi: Hatua 4

Kuna hatua nne kuu za kufanyia alama zako pindi ukishazichanganua:

1. Kuthibitisha Alama
2. Kutayarisha Mapendekezo ya Utetezi
3. Kuandika Ripoti
4. Kufanya Mabadiliko

Sehemu hizi nne zinazofuata zitakuongoza katika hatua hizi kwa undani zaidi, ikiwa ni pamoja baadhi ya dhana za kimsingi za utetezi na vidokezo vya usambazaji, mapendekezo na ujumbe wa utetezi. Utahisi kwamba baadhi ya mazingatio na maswali yaliyo hapa chini yanarudia yale uliyofikiria hapo awali; hili ni jambo zuri na husaidia kuboresha na kuongeza umaalum kwa mapendekezo ambayo yatatokana na alama, kudadisi mawazo yoyote yaliyotolewa, na kukupa muda wa kuchakata matokeo na, hatimaye, kutoa ripoti bora zaidi na mpango wa utetezi.

## Hatua ya 1: Kuthibitisha Alama

Utatumia alama ya Barometa na uchanganuzi/madokezo uliyoandaa wakati wa Hatua ya 3 (Kuchambua Matokeo Yako ya Jumla ya Barometa) ya Sehemu ya 3. Uchambuzi wa Data ili kuthibitisha alama na matokeo ya mwanzo na washirika wakuu (kama ilivyojadiliwa pia katika Sehemu ya 1. Mipango na Maandalizi, ushirikishaji wa wadau).

Mchakato huu wa uthibitishaji husaidia kurekebisha na kuimarisha uchanganuzi wako wa data katika maandalizi ya kuibadilisha kuwa utetezi unaofaa na wa maana. Kuthibitisha alama na uchambuzi/madokezo kutoka Sehemu ya 3. Hatua ya 3 ni muhimu ili kuhakikisha kuwa washirika wote muhimu wanapokea na kukubali matokeo kabla ya kwenda mbele na utetezi na usambazaji wa pamoja. Utaratibu huu hauhusu kubadilisha alama, lakini kuhakikisha kwamba alama zinaeleweka kwa wale ambao wana ufahamu zaidi kuhusu muktadha—hasa, wahusika, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake, na wanawake na wasichana kutoka jamii ambazo Barometa ilitekelezwa.

- ☐ Haitawezekana kumhusisha kila mtu aliyeshiriki katika KII na FGD katika uthibitishaji wa alama na maelezo kutoka Sehemu ya 3. Hatua ya 3. Hata hivyo, unapaswa ama kuwaita wadau wakuu wachache kwa mkutano halisi au wa mtandaoni wa uthibitisho au ufanye vikao/mikutano midogo ya mtandaoni na vikundi tofauti vya wadau, kutegemea muktadha wako na kile kinachowezekana. Vikundi vya wadau wa kushiriki katika uthibitishaji wa alama kimsingi vitajumuisha:
- ☐ Wahusika, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake inayofanya kazi ndani na pamoja na jamii zao; na
- ☐ Viongozi na wanajamii ya wanawake wenyeji, waliohamishwa makwao na wakimbizi.
- ☐ Unaweza pia kutaka kushirikisha wahusika, mashirika na taasisi za kibinadamu (hasa za eneo husika na za kitaifa, lakini pia ya kimataifa). Unaweza pia kuzingatia kujumuisha, ikiwa ni salama kufanya hivyo na ni muhimu katika muktadha wako, wahusika na wawakilishi wa serikali, kama vile wawakilishi wa Wizara ya Masuala ya Wanawake/ Usawa wa Jinsia au idara ya serikali inayoongoza haki za wanawake.
- ☐ Wakati wa mikutano ya **uthibitisho** unaohusisha wadau, hakikisha kwamba waliohudhuria wana Alama ya Jumla (iliyo na "taa za barabarani"pamoja na maelezo ya maana ya alama hii), alama za kila eneo la Matokeo, na Vidokezo kutoka *Sehemu ya 3. Hatua ya 3* (ikiwa ni pamoja na dondoo zozote za moja kwa moja kutoka kwa washiriki wa Barometa ambazo umekusanya kutoka kwenye uchanganuzi wako).

Itakuwa muhimu **kuandika maelezo ya kina** katika mchakato wote wa uthibitishaji.

- ☐ Wakati wa vikao/mikutano ya mtandaoni na wadau wakuu, uliza mfululizo wa maswali ili kuhimiza majadiliano.

**Maswali ya mwongozo kwa mchakato wa uthibitishaji:**

- ☐ Kagua matokeo na uchanganuzi wako na utoe maoni na mchango shirikishi kuhusu:

- o Ni nini kinachoakisi na kuendana na hali halisi au kisichoendana na uchanganuzi wa alama na mada, na hali zote zikiwa zimejumuishwa?
- o Je, matokeo na uchambuzi yanaelezeaje masuala yanayowakabili wanawake, wasichana na wafanyakazi wa misaada wa kike?
- o Nini kipya? Kujifunza ni nini? Nini kinaunga mkono kile kinachojulikana tayari? Kuna migogoro gani?
- o Je, kuna matokeo ambayo ni muhimu zaidi kuliko mengine, kwa maoni ya wadau waliopo?
- o Je, kuna matokeo ambayo yanaweza kutumika katika miktadha nje ya eneo lililotathminiwa na Barometa?
- o Je, wadau wowote wana mawazo kuhusu njia za kuboresha usaidizi kwa wanawake na wasichana wanaoishi na kufanya kazi katika mazingira haya?

- ☐ Kagua uwezo wa kueleweka na uwazi wa matokeo na uchambuzi, haswa katika lugha, ufafanuzi na mawasilisho.

Kuthibitisha matokeo na alama ni hatua muhimu katika mchakato kwa sababu kunawaleta wadau wakuu na utaalamu, maarifa na uzoefu wao. Andika maelezo ya kina ya majibu yao kwa maswali yaliyo hapo juu na ujaribu kufafanua maswali na/au mapendekezo yoyote yanayojitokeza yanayotokana na mijadala.

Kupitia mchakato huu, kuna uwezekano wa kuanza kuandaa **mapendekezo** na ikiwezekana, hata ujumbe wa utetezi. Majadiliano yanapogeukia mapendekezo, hakikisha kwamba unaandika mapendekezo mahususi yanayotokea na uendelee kuuliza maswali ya ufafanuzi na uchunguzi, kama yaliyo hapa chini:

- ☐ Je, pendekezo hili linatatua wasiwasi/tatizo gani ambalo lililetwa na alama? Je, ni matokeo gani yataimarishwa kupitia utekelezaji wa pendekezo hili?
- ☐ Mapendekezo haya ni ya nani? Je, tunahitaji kumfikia nani na utetezi wetu ili kufikia mabadiliko haya?
- ☐ Je, pendekezo hili litafanya kazi katika muktadha huu? Kwa nini ndiyo au kwa nini hapana? Nani anafaa kujumuishwa ili pendekezo hili litekelezwe?
- ☐ Je, matokeo na mapendekezo haya yanatumika nje ya muktadha mahususi ambapo Barometa ilichanganua?

**Muhimu:** Kumbuka kwamba maswali haya kuhusu mapendekezo, hasa kuhusu wale ambao mapendekezo yanawahusu na wale wanaopaswa kulengwa kwa utetezi, yanaweza kuwa nyeti sana. Uliza tu maswali haya kwa washirika unaowaamini na uwasiliane na washirika unaowaamini na timu ya Barometa kabla ya mikutano halisi/ mikutano ya mtandaoni ya uthibitishaji ili kujadili kama mapendekezo yanapaswa kuwa sehemu ya kila majadiliano. Ikiwa kwa sababu yoyote unahisi kuwa haitakuwa salama au itakuwa hatari kubwa sana kuuliza maswali kama haya kwa wadau fulani, usiwaulize.

# Hatua ya 2: Kuandaa Mapendekezo ya Utetezi

Katika hatua hii ya pili, leta Alama ya Jumla, Alama ya Matokeo na madokezo kutoka kwenye sehemu zote zilizopita ili kuandaa na kukamilisha mapendekezo yako ya utetezi ili yaakisi matokeo ya Barometa. Utaratibu huu unapaswa kufanywa katika kikundi kidogo kama vile timu ya Barometa, au na Kiongozi wa Timu ya Barometa ili kurahisisha mchakato iwezekanavyo.

Michakato mingi inaweza kutumika kuandaa mapendekezo maalum ambayo ni muhimu katika utetezi.

**Mbinu ya "SMART",** inayoelezwa hapa chini, inaweza kukusaidia kuyapa kipaumbele mapendekezo yako. Inakupa msururu wa maswali ya uchunguzi na kukusaidia kuunda mpango wa "SMART" wa utetezi wako, kwa lengo la kuwafanya watoa maamuzi walengwa na wahusika wakuu wakubali mapendekezo yako.

Unaweza kupendelea kutumia mchakato tofauti, kutegemea na muktadha wako au ikiwa unapendelewa na wataalam wa utetezi ambao wanashughulikia Barometa pamoja na wewe.

## Kukamilisha Mapendekezo

Kwa kuzingatia kazi na tafakari nyingi ambazo tayari zilishafanyika katika Kuweka na Kuthibitisha Alama, ikiwa ni pamoja na mazungumzo na wadau wakuu na timu ya Barometa, mapendekezo kadhaa ya kuboresha mazingira ya wanawake, wasichana na wahudumu wa kike wa kibinadamu yanapaswa kuwa tayari yamepatikana katika hatua hii.

**Je, unapaswa kuwa na mapendekezo mangapi?** Hakuna "idadi mujarabu" ya mapendekezo unayofaa kujitahidi kufikia; mapendekezo yanapaswa kutoa masuluhisho kwa changamoto kuu na muhimu zaidi zilizotambulishwa na alama za Barometa. Kunaweza kuwa na mwelekeo wa kutoa pendekezo kwa kila changamoto iliyotambuliwa wakati wa mchakato wa Barometa, jambo linaloweza kuwa na ugumu. Kupunguza idadi ya mapendekezo kunasaidia ili yaweze kupitishwa. **Kuwa na zaidi ya mapendekezo 5-7 kunaweza kufanya iwe vigumu kuandaa mpango wa utetezi, kwa hivyo zingatia kuweka vipaumbele. Tena, kuzingatia alama za "rangi nyekundu" na "rangi ya chungwa" kunaweza kusaidia katika kuwekea mapendekezo vipaumbele.**

Kuandaa mapendekezo *kutajumuisha na kuonyesha* vipengele muhimu vya yale ambayo tayari yamejadiliwa. Katika hatua hii, unapaswa:

- ☐ **Kuweka vipaumbele:**
  - o Je, ni changamoto zipi kuu zimeangaziwa na alama na matokeo?
  - o Kulingana na mijadala ya kuweka alama na uthibitishaji, ni changamoto gani kati ya hizi muhimu zinazohitaji hatua za haraka?
  - o Njia moja ya kuyapa kipaumbele mapendekezo ni kuangalia yale yanayoshughulikia alama "nyekundu" au "za chungwa".
- ☐ **Kuchunguza:**
  - o Kwa changamoto/hatua za kipaumbele:
    - Je, ni yapi, kama yapo, kati ya mapendekezo yaliyoletwa wakati wa mchakato wa uthibitishaji yanashughulikia changamoto hizi?
    - Je, kuna mapendekezo ya ziada yanayohitajika kushughulikia changamoto kuu?
    - Nani anafaa kuchukua hatua kuhusu mapendekezo ili kuleta mabadiliko?
  - o Je, kuna changamoto/hatua nyingine zinazohitaji kuchukuliwa, lakini zinahitaji juhudi za muda mrefu za utetezi?
  - o Je, changamoto zinafaa kushughulikiwa katika ngazi ipi? (Kwa mfano, je, changamoto ipo katika ngazi ya eneo husika, ambapo usimamizi wa kambi unaweza kulengwa katika utetezi? Je, tatizo la mfumo wa kibinadamu ni pana zaidi, ambapo lengo la utetezi linapaswa kulenga shirika la Umoja wa Mataifa au serikali ya nchi husika?)

- ☐ **Kuibua changamoto:**
  - o Ili kuhakikisha kuwa una mkusanyiko “sahihi” wa mapendekezo, tumia muda fulani kudadisi mawazo na uchanganuzi wako kwa kila pendekezo. Baadhi ya maswali ya kuongoza ni pamoja na:
    - Je, pendekezo hili litafanya kazi katika muktadha huu? Kwa nini ndiyo au kwa nini hapana?
    - Nani anafaa kujumuishwa ili pendekezo hili litekelezwe? Je, kikundi hicho kinaweza kulengwa? Kivipi?
  - o Je, pendekezo hili linaweza kutumika nje ya muktadha ambao Barometa ilichanganua?
  - o Je, pendekezo hili linahusiana vipi na madhumuni na lengo la jumla la Barometa?
- ☐ **Kuthibitisha Upya:**
  - o Kadri inavyowezekana, shiriki na ujadili mkusanyiko wa mapendekezo yanayokaribia kumalizika na timu ya Barometa na idadi ndogo ya washirika wakuu (hasa mashirika ya eneo husika yanayohusika katika mchakato) ili kuhakikisha kwamba kile kilichosemwa katika mikutano halisi/mikutano ya mtandaoni ya uthibitishaji inawakilishwa ipasavyo na kwamba mapendekezo yanaakisi alama).

Baada ya kukamilisha yaliyo hapo juu, unapaswa kuwa na mapendekezo yaliyoandikwa ambayo, kwa kuzingatia alama na majadiliano, lazima yapokelewe ili kuboresha muktadha kwa wanawake, wasichana na wanawake walio katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu.

Hatimaye, kumbuka kwamba ili Barometa iwe na nyongeza na ichukuliwe kwa uzito na watoa maamuzi, mapendekezo yanapaswa kuungwa mkono na alama, data iliyokusanywa na nukuu zozote za moja kwa moja kutoka kwa washiriki (zingatia usiri na faragha) wakati wa utekelezaji wa Barometa.

# Hatua ya 3: Kuandika Ripoti

Hatua hii inayofuata inashughulikia kuandika ripoti ya utekelezaji wa Barometa, matokeo na mapendekezo.

**Muhimu: Kumbuka kwamba ripoti hii inapaswa kutolewa kwa umma ili matokeo yaweze kutumika kwa upana; hii ina maana kwamba unapaswa kuendelea kuchukulia faragha na ulinzi wa data kwa uzito.**

Baada ya Sehemu ya 3 na Sehemu ya 4. Hatua ya 1-2, sehemu kubwa ya ripoti tayari itakuwa imeandikwa. Hatua muhimu inayofuata itakuwa kujumuisha sehemu zote katika hati moja inayooana na inayoweza kusomeka. Ripoti inafaa ijumuishe taarifa kuhusu mazingira ambamo Barometa ilitekelezwa, maelezo mafupi ya Barometa yenyewe, maelezo ya hatua zilizochukuliwa kufikia alama hizo ikiwa ni pamoja na idadi ya KII na FGD, alama zenyewe na mapendekezo yaliyofikiwa katika hatua zilizopita. Ufafanuzi wa jinsi kila pendekezo lilivyotayarishwa unaweza kusaidia kuhakikisha kuwa mapendekezo yanachukuliwa kwa uzito (kumbuka kuwa mkakati wa kupokea mapendekezo umejadiliwa katika Hatua ya 4 hapa chini). Kwa kutumia manukuu kutoka Sehemu ya 3 inaweza pia kusaidia kufanya ripoti iwe mahususi na kuhakikisha kuwa Alama ya Jumla, alama binafsi, pamoja na mapendekezo, vinaungwa mkono na data na hali za watu binafsi na sauti za wanawake, wasichana na wanawake walio katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu.

**Urefu wa ripoti:** Kama ilivyo kwa idadi ya mapendekezo katika Hatua ya 2, kufanya urefu wa ripoti uwe kurasa 2-4 kunaweza kuwa muhimu ili kuhakikisha kwamba watu wanaohitaji taarifa iliyo ndani ya ripoti wanaisoma na kuitumia. Hii ina maana kwamba inakupasa uandike kwa ufupi inapowezekana na utumie taswira za data (kama vile grafu au chati) inaposaidia katika kueleza hoja, wakati wa na hasa unapowasilisha alama.

## Kuhitimisha Ripoti

Hatua ya mwisho katika kuandaa ripoti inahusisha kuidhinishwa na timu ya Barometa/mashirika washirika. Wale wanaohusika katika utekelezaji wa Barometa wanapaswa kutia saini kwenye ripoti baada ya kuwa na angalau fursa moja ya kukagua na kufanya mabadiliko kabla ya usambazaji wowote wa ripoti yenyewe. Kunapaswa kuwa na makubaliano kati ya washirika wa utekelezaji kuhusu utumiaji wa nembo na haki ya uandishi.

Ikihitajika, ripoti inafaa kutafsiriwa katika lugha za wenyeji.

## Mfano wa Muhtasari wa Ripoti

I. Usuli wa Muktadha (usizidi ukurasa ½)

 (a) Urefu wa migogoro/tatizo; muktadha ndani ya muktadha (kwa mfano, "Barometa hii ilichambua hali za wanawake na wasichana katika eneo la Bidibidi, Uganda.")

 (b) Misingi ya idadi ya watu (idadi au asilimia ya wanawake na watoto; wakimbizi wa ndani (IDP)/ wakimbizi; urefu wa wastani wa tangu kuhama; aina ya makazi)

 (c) Uchambuzi mfupi wa hali ya wanawake na wasichana

  (i) Data inayopatikana kuhusu UWAKI, uwezeshaji wa kiuchumi, na ukosefu wa usawa wa kijinsia, kwa mfano

II. Ufafanuzi wa Barometa

 (a) Aya 1 ya maelezo ya Barometa na madhumuni yake (unaweza kurekebisha yaliyomo kwenye hati ya mwongozo: 0a. Utangulizi wa Barometa ya Sikiliza!)

III. Alama za Barometa

 (a) Rangi za Alama (kwa ujumla na kwa maeneo manne ya Matokeo) yenye maelezo (angalia hati ya mwongozo: 0a. Utangulizi wa Barometa ya Sikiliza!)

IV. Maelezo ya jinsi ulivyopata alama (yasizidi thuluthi ya ukurasa)

 (a) Idadi ya KII

 (b) Idadi ya FGD

 (c) Idadi ya Tafiti za Mitazamo wa Wafanyakazi ulizofanya

 (d) Idadi ya Tafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia na wapi zilikofanyika

V. Uchambuzi wa alama na mapendekezo (usizidi ukurasa 1)

 (a) Uchambuzi wa alama kulingana na Matokeo 1-4 huku mapendekezo yanayohusiana nayo yakiwa yamepatikana kupitia mchakato wa uthibitishaji na mapendekezo

VI. Kiambatisho – Unganisha kwenye ufafanuzi wa Barometa

# Hatua ya 4: Kufanya Mabadiliko

Madhumuni ya Barometa ya Sikiliza! ni kutumika kama zana ya utetezi kwa vikundi, mashirika na mitandao ya wanawake pamoja na wahusika wengine wanaokabili UWAKI ili kuwawajibisha wale wanaohusika katika utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa wanawake na wasichana. Utekelezaji wa zana na uandishi wa ripoti unaunga mkono lengo hili kuu la kuboresha mfumo wa kibinadamu na usaidizi mahususi, kwa wanawake na wasichana wanaoishi katika mazingira yanayohitaji usaidizi wa kibinadamu, na wanawake wanaohudumu katika hali za kibinadamu wanaofanya kazi nao.

Sehemu ifuatayo inashughulikia usambazaji wa ripoti kwa wahusika na jinsi ya kuunda mkakati wa utetezi ili matokeo na mapendekezo yawe msingi wa hatua za usaidizi wa kibinadamu za siku zijazo. Mazingatio makuu ya utetezi—kama vile ni nani wa kumlenga na ujumbe wa utetezi—yatajadiliwa.

## Usambazaji na Utekelezaji wa Ripoti

Baada ya kukamilika, ripoti inapaswa kusambazwa na kujadiliwa na wale waliohusika wakati wa utekelezaji wa Barometa. Ni muhimu kuhakikisha kwamba waliochangia wanaelewa ripoti ya mwisho na alama, pamoja na mapendekezo, na jinsi unavyopanga kuendelea na ripoti, mapendekezo na ujumbe wa utetezi. Hii ni pamoja na kujadili (ikiwa faragha na utendaji unaruhusu) matokeo na:

- ☐ Watoa taarifa muhimu
- ☐ Washiriki wa FGD
- ☐ Mashirika ya kutekeleza barometa (pamoja na viongozi wakuu kama inavyofaa)
- ☐ Watu binafsi/ mashirika yanayohusika katika kutafuta uthibitisho

Usambazaji unapaswa kufanyika *baada ya* masuala ya utetezi yaliyo hapa chini kujadiliwa na makubaliano kufikiwa ili kuhakikisha usalama na ulinzi wa taarifa na kwamba wale wanaopokea matokeo wanafahamu hatua za utekelezaji.

## Mbinu ya SMART

Kuandaa mkakati wa utetezi kunapaswa kuanza kwa kufanya mapendekezo ya ripoti kuwa malengo ya utetezi yanayotekelezeka. Njia moja ya kufanya hivyo ni kutumia mbinu ya "SMART", ambayo ni njia inayoweza kukusaidia kupanga mawazo yako na kuunda mpango kulingana na mapendekezo.

**"SMART" ni ufupisho wa Kiingereza wenye maana ya (Specific) Mahususi, (Measurable) Linaloweza Kupimika, (Atttainable) Linaloweza Kufikiwa, (Relevant) Linalofaa na (Time-bound) Linalowekewa Muda**. Zingatia kuandaa lengo Mahususi, Linaloweza Kupimika, Linaloweza Kufikiwa, Linalofaa na Lenye Muda kwa kila pendekezo ili uwe na mpango wa jinsi ya kufikia mapendekezo.

- ☐ **Maswali ya kujibu ili upate lengo "SMART":**
  - o **M**ahususi – "Kipi kitatokea ikiwa utetezi utafaulu?"
  - o **L**inaloweze kupimika – "Tutajuaje kama utetezi umefaulu?"
  - o **L**inaloweza kufikiwa – "Je, matokeo yanayotarajiwa yanaweza kufikiwa, ikiwa ni pamoja na kama rasilimali zinazohitajika, muda uliopangwa, na msukumo vipo ili kufikia matokeo?"
  - o **L**inalofaa – "Je, lengo hili linaleta hatua ya maana kuelekea pendekezo?"
  - o **L**enye muda – "Ni lini tunafaa kutekeleza hili na ni muda gani wa muafaka kwa washirika?"

Kujibu maswali haya na kuunda mpango wa SMART kwa kila moja ya mapendekezo uliyochagua kutasaidia kuweka vigezo vinavyoweza kufikiwa katika mapendekezo yako. Kwa mfano, pendekezo kutoka kwenye Barometa linaweza kuwa *"kuongeza ufadhili wa mafunzo ya kuzuia udhalilishaji na dhuluma za kingono." Mfano wa lengo la SMART linalounga mkono hatua kuhusu pendekezo hilo ni "kuongeza ufadhili kwa 20% kwa ajili ya kuzuia udhalilishaji na dhuluma za kingono kwa mashirika ya eneo husika katika miaka miwili ijayo."*

Kuna mbinu nyingine ambazo watetezi wanaweza kupendekeza ili kuhakikisha kuwa mapendekezo yanatekelezeka. Kwa ujumla, ni muhimu kuzingatia malengo yako maalum (kama yalivyoelezwa na mapendekezo); fikiria kuhusu rasilimali utakazohitaji; na uandike mpango wako wa utetezi ukiwa na muda/makataa yaliyoambatishwa kwa kila pendekezo. Haya yatafanya mipango ya utetezi kuwa thabiti zaidi na kuwa na uwezekano wa kutekelezwa.

## Mazingatio

Ripoti ni mojawapo ya bidhaa zako kuu za utetezi, lakini usambazaji wa ripoti pekee hautahakikisha kuwa mabadiliko yaliyopendekezwa yatatokea. Hilo huenda likahitaji mkakati wa utetezi na juhudi za pamoja za utetezi.

Ili kuboresha zaidi mkakati wa utetezi, kuna mambo kadhaa ya kuzingatia. Ingawa mambo na maswali yaliyo hapa chini ni sehemu muhimu ya kuanzia, kila muktadha utakuwa tofauti.

- ☐ **Hatari ni zipi na tunaweza kuzipunguza vipi?**

  Wahusika wa kibinadamu, ikiwa ni pamoja na mashirika ambayo yanatekeleza Barometa, mara nyingi hufanya kazi katika mazingira hatari, si tu kimwili lakini pia kisiasa na kifedha. Ni muhimu kwa wanaofanya utetezi na mapendekezo ya Barometa kuzingatia hatari ambazo utetezi wao unaweza kuwa nao, wafahamu bayana kuhusu hatari hizi au zinaweza kuwa nini, na wawe na mipango na mikakati ya kuzipunguza (angalia pia Sehemu ya 2. Utekelezaji, kuhusu hatari, faida na mazingatio ya usalama).

Mashirika yanaweza kuwa katika hatari ya kupoteza ufadhili au ufikiaji ikiwa/yanapodai mabadiliko kutoka kwa mashirika ya kimataifa au mashirika ya serikali. Kutarajia msukosuko unaoweza kutokea wa kisiasa au wa kifedha—na athari zake kwa uwezo wa mashirika kufanya kazi na kupata ufadhili—ni muhimu katika hatua hii ili hatari hizi, kama zipo au zinawezekana, ziweze kupunguzwa. Kupunguza hatari kunaweza kutokea kwa kuhusisha mashirika yanayofaa, kutunga ujumbe wa utetezi ipasavyo kulingana na muktadha, na kuchagua wajumbe sahihi (ambao watawasilisha ujumbe na jinsi watakavyofanya hivyo, na kwa nani) na pia kuzingatia wakati.

Inaweza kusaidia kupata uungwaji mkono wa wazi kutoka mashirika ya kimataifa, kama vile Shirikala la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) au serikali (ambapo ni salama kufanya hivyo) kabla ya kufanya utetezi ili kusaidia kupunguza hatari kwa mashirika yanayotekeleza Barometa. Kwa kweli, kupata uungwaji mkono wa wahusika wakuu kunaweza kuwa mojawapo ya hatua za kwanza katika mpango wako wa utetezi.

☐ **Nani wa Kuhusisha?**

Wahusika tofauti watakuwa na mazingatio tofauti linapokuja suala la mamlaka, sauti na hatari ndani ya mfumo wa kibinadamu. Ni muhimu kutoyaacha mashirika ya ndani ya nchi au sehemu mahususi pekee kubeba mzigo mkubwa wa kutetea mabadiliko katika mfumo wa kibinadamu. Ni kinyume cha maadili kuyauliza mashirika ya ndani kurekebisha mifumo ya kibinadamu ambayo hawakubuni, hasa kwa vile mara nyingi wao ni wahusika wasio na nguvu ndani ya mifumo hiyo, na utetezi wa wazi unaweza kuyaweka hatarini, kisiasa na wakati wa kuzingatia ufadhili. Ni muhimu kukumbuka kuwa kunaweza kuwa na nguvu na usalama katika miungano, na kufanya kazi kwa kuhusisha mashirika ya ndani na ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (NGO) kunaweza kuwa njia moja ya kwenda mbele. Kutafuta ushiriki wa mashirika yaliyo na nia kama yao na yaliyo na maadili kama ya Barometa ni chaguo mojawapo la kuunda muungano wa walio tayari kusukuma ujumbe wa utetezi.

Timu ya Barometa na washirika wake na mashirika husika pia inapaswa kuzingatia kama ni jambo la busara na salama kujumuisha mashirika ya kimataifa na serikali katika mazungumzo kuhusu mkakati wa utetezi, au kuyaweka kuwa walengwa wa utetezi pekee.

Baadhi ya maswali ya kuuliza wakati wa kuamua ni nani wa kumjumuisha katika mijadala ya utetezi ni pamoja na:

- Je, ni washirika gani unaoweza kufanya nao kazi ili kuwasilisha ujumbe wa utetezi?
- Ni wajumbe gani wanaofaa? Ni nani walengwa wa utetezi (yaani, watoa maamuzi) watawasikiliza na wanaweza kushirikishwa katika mkakati wa utetezi?
- Nani anaweza kutoa usalama zaidi na/au uhalali kwa matokeo ya Barometa?
- Nani anaweza kufikia watoa maamuzi katika muktadha huu? Je, kuna uwezekano kuwa wataunga mkono mapendekezo ya Barometa?
- Je, ni washirika gani wanaoweza kukusaidia kutimiza malengo ya SMART au kuunga mkono kupitishwa kwa mapendekezo? Wanaweza kuwa mashirika binafsi, kama vile Mtandao wa Kuzuia Unyanyasaji na Dhuluma za Kingono (PSEA) au Makundi ya Utetezi wa Kijinsia, mashirika, miungano na hata idara ndani ya serikali au mashirika ya kimataifa.

☐ **Je, watoa maamuzi watafikishiwa ujumbe vipi?**

Kuna njia nyingi za kufikia watoa maamuzi wanaoweza kufanya mabadiliko yanayobainishwa na mapendekezo na malengo ya utetezi:

- Mikutano ya ana kwa ana au kwa simu
- Kutumia washawishi/washirika wa hadhi ya juu
- Mitandao ya kijamii
- Vyombo vya habari vya jadi

Haya ni machaguzi ambayo yanafaa kuzingatiwa na kupimwa kwa uangalifu. Vitendo hivi vinaweza kuratibiwa, ili juhudi za mitandao ya kijamii zisaidie mikutano ya ana kwa ana, au unaweza kuamua kutoshiriki kabisa katika mikakati fulani ya utetezi. Kwa mfano, kutumia watetezi wa hadhi ya juu kunaweza kusaidia sana matokeo ya Barometa lakini pia kunaweza kuangazia mapungufu ya mfumo mbele ya hadhira pana, kunaweza kuaibisha uongozi wa masuala ya kibinadamu na kusababisha hatari kwa mashirika yanayotekeleza Barometa kufikia wanawake na wasichana wenye mahitaji, ikiwa kulipiza kisasi kutatokea. Vinginevyo, baada ya kutafakari kwa makini, mikutano ya faragha inaweza kuwa haitatosha kuwashawishi watoa maamuzi kwamba wanahitaji kukubali mapendekezo; badala yake, labda shinikizo la hadharani pekee ndilo linaweza kuleta mabadiliko muhimu. Katika hali hiyo, watetezi wa hadhi ya juu watakuwa muhimu sana katika utetezi.

- [ ] **Ni msaada au rasilimali gani nyingine zinahitajika?**

Ingawa alama ya Barometa na mapendekezo yanaungwa mkono na data na ripoti ni zana muhimu ya utetezi, inaweza kuwa muhimu kuzingatia nyenzo au usaidizi mwingine ambao ni muhimu ili kusaidia kutetea kutelelezwa kwa mapendekezo. Kwa mfano, je, mapendekezo ya Barometa yanaunga mkono kutimizwa kwa Mpango rasmi wa Usaidizi wa Kibinadamu katika mazingira fulani? Hili litahitaji uchambuzi wa Mpango wenyewe wa Usaidizi wa Kibinadamu.

Unaweza kuamini kuwa kampeni ya mitandao ya kijamii ni muhimu, lakini huna utaalamu wa mitandao ya kijamii unaohitajika ili kubuni na kutekeleza kampeni, na hivyo ukahitaji kumshirikisha mtu mahiri katika aina hii ya utetezi. Iwapo itabainika kuwa mapendekezo yanahitaji uungwaji mkono katika ngazi ya juu ya uongozi mkuu wa Umoja wa Mataifa, kusafiri hadi New York au Geneva kunaweza kuhitajika (ikiwezekana). Kuzingatia kama shirika lako lina rasilimali (yaani, muda, fedha) na uwezo (yaani, wafanyakazi wanaweza kupata visa?) kufanya safari kama hiyo ni muhimu. Kuelewa rasilimali zako na ukomo wa rasilimali ni muhimu ili kuunda mpango kazi wa utetezi unaotekelezeka.

## Mpangokazi wa Utetezi

Baada ya mambo yote yaliyo hapa juu kuzingatiwa, tengeneza mpangokazi wa utetezi kama hatua ya mwisho. Mpangokazi unapaswa kuundwa kwa pamoja na wale ambao huenda watakuwa na wakati na rasilimali za kuupeleka mbele. Hapa chini tuna mfano wa mpangokazi ambao unaweza kukusaidia kupanga mawazo yako.

| Malengo | Vitendo | Ratiba | Mtu/ Shirika Linalowajibika | Rasilimali Zinazohitajika | Kiashiria cha Mafanikio |
|---|---|---|---|---|---|
| Lengo la 1 la SMART [Weka lengo lako kwa mojawapo ya mapendekezo uliyochagua] | | | | | |
| Lengo la 2 SMART [Weka lengo lako kwa mojawapo ya mapendekezo uliyochagua] | | | | | |

Baada ya mpango huu kukamilika na makubaliano kuafikiwa, kilichobaki ni kuutekeleza. Kila la heri katika kutumia Barometa ya Sikiliza! kufanya mfumo wa kibinadamu uwe mahali salama penye usawa kwa wanawake na wasichana!

# Viambatisho



Picha na A Ohanesian, IRC

# Zana za Kukusanya Data

## Mwongozo wa Majadiliano ya Kikundi ya Washichana

**MUHIMU:** Hakikisha **umepata idhini/kibali** kutoka **kwa** washiriki wote **kabla ya** kuanza kikao cha Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD). Inashauriwa kuwa usiwe na **zaidi ya washiriki wanane** katika kikao chako cha FGD. Angalia *Sehemu ya 2. Hati ya Mwongozo wa Utekelezaji* wa mchakato wa kupata Idhini na *Kiambatisho cha Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometer na Idhini* ya kutumiwa na Fomu ya Utoaji Idhini.

### Nyenzo zinazohitajika:

- Karatasi ya chati ya kupindua
- Kalamu za kutia alama za rangi tofauti [Ikiwa huna za rangi tofauti, tumia alama tofauti kwenye ramani]

### Kuanza kwa kikao cha FGD

**Wakati washiriki wote wamekusanyika, mratibu wa FGD anafaa kuanza kwa utangulizi huu [tafadhali rekebisha palipoonyeshwa]:**

Habari? Jina langu ni ________ na ninafanya kazi katika _______. Ninaandamana na mwenzangu _____ ambaye anafanya kazi katika [shirika lile lile/lingine] na atakuwa akituandikia kumbukumbu. Mwenzangu ___________ atakuwa akikalimani [ikiwa mkalimani atahitajika].

Tuko hapa leo ili kujadiliana nawe baadhi ya vipengele vya usaidizi wa kibinadamu ambao umepokea. Tutakuwa tukichora ramani pamoja ili kutusaidia kuelewa usaidizi unaopatikana katika jamii yako na masuala yaliyopo ya usalama kwa wanawake na wasichana. Tutatumia taarifa hizi ili kutusaidia kuyauliza mashirika kutoa usaidizi wa kibinadamu ulio salama zaidi, wenye usawa na ambao ni rahisi kwa wanawake na wasichana kuufikia.

Majadiliano na ramani hii itakuwa siri. Mratibu (mimi), mnakili kumbukumbu na mkalimani sote pia tumeahidi kudumisha usiri. Hili linamaanisha kwamba taarifa yoyote mtakayoshiriki nasi leo haitashirikiwa na mtu mwingine yeyote. Huhitaji kutupatia majina yako au taarifa yoyote ya kibinafsi. Huhitaji kutuambia kuhusu hadithi zako mahususi. Ramani na majadiliano yetu hayatatutambulisha kwa hivyo hayawezi kuhusishwa nawe binafsi. Katika ramani na katika kumbukumbu zetu, hakuna utambulisho wa mtu utakaotajwa.

Kushiriki kwako katika mkutano huu ni kwa hiari kabisa. Ikiwa unahisi wasiwasi wakati wowote, uko huru kuondoka, na haitaathiri kwa njia yoyote huduma na usaidizi unaopokea na unaostahili. Majadiliano yatadumu kwa muda usiozidi saa moja.

Tutakuwa tukifanya zoezi hili na makundi mengine ya wanawake na wasichana katika jamii.

Je, kuna kitu chochote ambacho ungehitaji ili uwe salama na ushiriki bila wasiwasi? Je, kuna jambo lingine tunaloweza kufanya ili kukusaidia ujisikie bila wasiwasi? Je, una maswali yoyote ambayo ungependa kuuliza kabla hatujaendelea?

*Hakikisha kuwa maswali yote yamejibiwa kikamilifu na uangalie tena ili uhakikishe kuwa hakuna chochote kitakachoachwa bila kujibiwa.*

# Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Wasichana walio balehe

## 1. Maelezo ya msingi ya kikundi

**Tarehe:**

**Mahali:** ________________________________

**Mratibu:** ________________________________________

**Mnakili kumbukumbu:** ________________________________________

**Je, ukalimani unahitajika? NDIYO HAPANA**

**Ikiwa ndiyo, ni ukalimani kutoka __________________ (lugha) hadi ____ (lugha)**

**Mkalimani:** ________________________________________

**Idadi ya washiriki:** ________

**Umri wa washiriki wa kikundi (chagua aina inayofaa):**

- ☐ Miaka 10-14
- ☐ Miaka 15-19

## 2. Ramani na majadiliano

### Hatua ya 1. Kuchora jamii na huduma

Kipe kikundi kalamu na karatasi ya chati ya kupindua, ambayo inapaswa kuwa imechorwa muhtasari katika KALAMU NYEUSI wa nyumba chache ili kuanza kuwakilisha jamii. Eleza uwakilishi huu kwenye ramani ili kikundi kielewe.

*Hakikisha kila mtu anaweza kuona/kufikia ramani.*

**Kisha waalike washiriki waongeze kwa kutumia KALAMU NYEUSI vipengele vingine vyote muhimu katika maisha na jamii yao, ikijumuisha huduma na vistawishi vinavyopatikana na mahali vilipo**. Pia waongeze nyumba zaidi, barabara, njia, maeneo ya kawaida ndani na nje ya makazi/eneo.

Ikihitajika, wahimize waongeze vitu kama vile: vyoo; mabafu; vituo vya maji; vituo vya usambazaji; vituo vya afya; nafasi za wasichana, wanawake, watoto; vituo vya jamii; viwanja vya kucheza; masoko; shule; na kadhalika.

Washiriki watakapohisi kuwa ramani inawakilisha jamii yao, nenda kwenye hatua inayofuata.

### Hatua ya 2. Mashauriano na wasichana

| | |
|---|---|
| **Vipimo vya Barometa** | Kadirio la idadi ya watu ambayo vistawishi na miundombinu ya WASH (maji, usafi wa mazingira na ustawi) inashughulikia maswala na mahitaji ya usalama ya wanawake na wasichana kupitia usanifu na mpangilio unaofaa na ufikiaji sawa |
| | Kadirio la idadi ya watu ambayo jinsi kambi hiyo imewekwa, jinsi inavyodumishwa na miundombinu iliyopo, inashughulikia maswala na mahitaji ya usalama ya wanawake na wasichana kupitia usanifu, mpangilio na ufikiaji unaofaa |

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| **Soma swali hapa chini. Kwenye ramani, weka alama ya kitone cheusi kwenye huduma na/au vistawishi vyote ambavyo wasichana waliripoti kuwa walishauriwa** wakati wa mchakato wa kuvianzisha au kuvijenga katika jamii. | ● | Nyeusi |

**Tumia maswali haya kukusaidia katika jukumu hili:**

- Wafanyakazi wa misaada walipokuja katika eneo lako, je walizungumza na wasichana katika jamii yako kuhusu mojawapo ya sehemu zifuatazo ulizochora kwenye ramani?

o Kidokezi (ikihitajika): Je, waliuliza maswali kuhusu usalama wa wasichana na kile ambacho wasichana wangependelea?

  - Vistawishi (WASH - vyoo, bafu, vituo vya maji)
  - Mpangilio wa kambi (kwa mfano, taa, barabara/njia, ushikaji doria)
  - Huduma (k.m., aina - nafasi salama, vituo vya afya, n.k.; nafasi/mahali; ufikiaji)
  - Taarifa (k.m., mbinu, lugha, ufikiaji)
  - Usambazaji (vifaa vya hadhi, vitu visivyo vyakula (NFI), chakula)

Kisha, **weka alama ya kitone cheusi kando ya kila kituo ambapo wasichana walishauriwa**.

## Hatua ya 3. Wasiwasi na sehemu na maeneo yasiyo salama kwa wanawake na wasichana

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Ukiangalia ramani, weka alama ya MDUARA kwa kutumia MSTARI THABITI eneo au mahali popote ambapo si salama kwa wasichana wakati wa mchana. |  | **Nyekundu** |
| Ukiangalia ramani, weka alama ya MDUARA kwa kutumia MSTARI WA VITONE eneo au mahali popote ambapo si salama kwa wasichana usiku. |  | **Nyekundu** |

**Vidokezo vinavyoweza kutumiwa (ikihitajika) ili kusaidia kikundi kufikiria ni maeneo gani ambayo si salama katika jamii yao:**

- Wasichana wana wasiwasi zaidi kuhusu nini katika jamii yako? Je, ni mambo gani ambayo huwafanya wasichana kuogopa zaidi? Yaorodheshe na uyatie alama kwenye ramani ikiwa mambo mapya yatatokea.
- Je, maeneo haya pia yana hatari zozote za salama kwa wanawake katika jamii yako?
- Ni nini huwafanya wasichana au wanawake kuhisi wasiwasi au woga wakiwa nyumbani? Katika jamii yao?
- Je, wanawake na wasichana wanaweza kutembea kwa usalama hadi kwenye vituo vya afya/nafasi salama kwa chini ya dakika 20? (*Uliza: Ikiwa hawatembei kwenda kwenye vituo vya afya, uliza jinsi wanavyofika kwenye vituo vya afya, ni vituo vipi wanavyoweza kufikia, inachukua muda gani kufika hapo, wanaandamana na nani, n.k.)*
- Je, wasichana wanajihisi salama wanapoenda kuchota maji? Ikiwa sivyo, kwa nini?
- Wakati wa kuchota maji, je, huwa mara nyingi unasubiri kwa muda mrefu? Ikiwa ndivyo, unasubiri kwa muda gani? (k.m., je, mara nyingi kuna foleni na mitungi ya maji iliyopangwa, na wanawake na wasichana wakisubiri kuchota maji?)
- Je, huwa unachota maji kabla ya macheo au baada ya machweo? (Ruka ikiwa maji ya bomba yanapatikana majumbani).
- Je, muda wa wastani wa kusubiri kutumia choo ni zaidi ya dakika 10? (Ruka ikiwa maji ya bomba yanapatikana majumbani).

## Hatua ya 4. Vifurushi vya hadhi (ruka ikiwa hakuna vifurushi vya hadhi ambavyo vimesambazwa)

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Kadirio la idadi ya wanawake na wasichana ambayo imepokea vifurushi vya hadhi vinavyofaa kulingana na mapendeleo na mahitaji yao |

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Weka alama ya + kwenye ramani katika maeneo ambapo vifurushi vya hadhi vimesambazwa. | + | **Buluu** |
| Weka alama ya X kwenye ramani ikiwa eneo ambapo vilisambazwa lilikuwa si salama kwa wanawake na wasichana. | X | **Nyekundu** |

**Kisha, uliza kikundi maswali haya:**

- Unapowafikiria wanawake na wasichana unaowajua—wanafamilia (mama, dada, binamu, shangazi, n.k.), marafiki, majirani—je, wengi wao wamepokea vifurushi vya hadhi?
- Je, unaweza kutuambia ni nini kilikuwa ndani ya kifurushi cha hadhi ulichopokea?
  - o Uliza: Je, vitu vilivyokuwa kwenye kifurushi hiki vilikusaidia/vilikuwa na manufaa kwako? Kwa nini? *Ongoza majadiliano ndani ya kikundi ili kukubaliana juu ya kiwango cha kuridhika. Ikiwa kikundi hakiwezi kukubaliana, kumbuka sifa tofauti zilizotolewa na idadi ya washiriki.*
- Je, unakumbuka nini kuhusu utaratibu wa kwenda kuchukua vifurushi vyako vya hadhi?
  - o Uliza: Ni nani aliyesambaza vifurushi hivi vya hadhi?
  - o **Uliza**: Je, vifurushi hivi vilisambazwa na wanaume au wanawake?
- Je, usambazaji wa vifurushi hivi umeathiri vipi (ikiwa umeathiri) uhusiano kati ya jamii ya wahamiaji na jamii ya wenyeji?
  - o **Uliza:** Je, jamii iliarifiwa vipi kuhusu vifurushi hivyo?

## Hatua ya 5. Usambazaji wa vyakula na vitu visivyo vyakula (NFI) (ruka ikiwa hakujakuwa na usambazaji)

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Sehemu ya watu wanaoelezea wasiwasi wao kuhusu usalama ndani ya na karibu na maeneo ya usambazaji wa NFI na yale yanayohusiana na Usalama wa Chakula na Kilimo (FSA) |

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| **Weka alama ya ~ kwenye ramani** katika maeneo ambapo ugawaji wa NFI/ chakula umefanywa. | ~ | **Buluu** |
| **Weka alama ya XX kwenye ramani** ikiwa eneo hilo la usambazaji halikuwa salama kwa wanawake na wasichana. | XX | **Nyekundu** |

- Je, wasichana wanaendea vitu vilivyosambazwa? Ikiwa jibu ni ndiyo, endelea. Ikiwa jibu ni hapana, ruka hatua hii na uende kwenye Hatua ya 6 hapa chini.
- Usambazaji wa mwisho ulikuwa lini?
  - o **Uliza:** Je, unajua jinsi jamii iliarifiwa kuhusu mahali, wakati na namna ya kuendea vitu vilivyosambazwa?
  - o **Uliza:** Wakati wa kuendea vitu vilivyosambazwa, kuna nyakati maalum zilizotengewa wanawake/wasichana kukusanya vitu hivyo na/au kuna mambo mengine hasa yanayofanywa kwa ajili ya wanawake wakati wa kwenda kwenye maeneo ya usambazaji?
  - o **Uliza:** Je, usambazaji ulifanya jamii yako kutokuwa salama kwa wasichana?

## Hatua ya 6. Nafasi salama (ruka hatua hii ikiwa hakuna nafasi salama)

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Kadirio la idadi ya watu ambao nafasi salama kwa wanawake na wasichana - pamoja na ushughulikiaji wa visa na usaidizi wa kisaikolojia na kijamii - zimeanzishwa, ni salama kufikiwa na zimewekwa umbali unaofaa.<br><br>Idadi ya wafanyakazi wa kike katika huduma na programu za kukabiliana na ukatili wa kijinsia (UWAKI), huku wanawake wakichukua tu nafasi zote za mstari wa mbele katika kutoa usaidizi na huduma |

**Nenda kwenye nafasi salama ambazo kikundi kilikuwa kimewekea alama kwenye ramani:**

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Chora kitone kikubwa katika sehemu zote ambapo msichana katika jamii yako anaweza kwenda ikiwa anaogopa na anataka usaidizi. (Kumbuka: Hizi zinaweza kuwa sawa au tofauti na nafasi salama ambazo tayari zimetambuliwa). | ● | **Kijani** |
| Chora mstari kwenye ramani kuelekea nafasi zozote za wasichana ambazo si salama kwao kusafiri. | ——— | **Nyekundu** |
| Weka alama ya X kando ya nafasi yoyote kati ya hizo ambazo si salama na kuna wasiwasi kwa wasichana kuwa mle. | **X** | **Nyekundu** |

**Kisha, uliza kikundi maswali haya:**

- Kwa nini wasichana huchagua kwenda sehemu hizo? (Rejelea sehemu zilizowekwa alama za vitone vikubwa).
- Uliionaje nafasi hiyo? Wasichana wanaipenda? Kwa nini wanaipenda au hawaipendi?

o Uliza (ikihitajika):
  - Je, wafanyakazi ni wanaume, wanawake (ikiwa ni pamoja na wale wa kujitolea) au ni mchanganyiko?
  - Ni nani yuko kwenye nafasi hiyo salama?
  - Je, unajihisi bila wasiwasi na salama kwa kiasi gani ukiwa hapo?
  - Je, kuna wasichana wowote ambao hawawezi kufika kwenye nafasi hizi?
  - Je, nafasi hiyo iko katika eneo ambalo ni rahisi na salama kwako kufika? Ikiwa haiko, kwa nini?
  - Je, unahitaji kusafiri muda gani ili kufika kwenye nafasi salama?
  - Je, unajihisi salama unapotembea kwenda kwenye nafasi hiyo?
  - Ni mara ngapi wasichana huenda kwenye nafasi salama na kwa sababu gani?

## Hatua ya 7. Taratibu za kuwasilisha malalamiko katika jamii

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Taratibu za kina za kuwasilisha malalamiko katika jamii (CBCM) na zana saidizi za kuhamasisha zimetengenezwa, kujaribiwa na jamii na zinatumiwa na mashirika yote |

**Muhimu! Kumbusha kikundi kisishiriki maelezo yoyote ya kibinafsi kuwahusu wao au wengine na washiriki tu habari ambayo wanahisi kuwa ni salama kushiriki. Usishiriki habari kuhusu visa au matukio maalum.**

- **Swali (chagua swali 1 kati ya haya 3 ambalo unaonelea linafaa/ linaeleweka vyema na kikundi chako):**

o Je, umewahi kuona mtu anayefanya kazi kwenye kambi (k.m., mpishi, mlinzi, n.k.) akimpa mtu yeyote maji, chakula au vifaa ili kupata upendeleo? AU/

o Je, umewahi kuona mtu anayefanya kazi kwenye kambi (k.m., mlinzi, mtu anayesambaza bidhaa, n.k.) akihadaa mtu yeyote kwa manufaa yake binafsi (hii inaweza kuwa kuomba upendeleo ili kumpa kitu anachodhibiti, kama vile chakula au vifaa?) AU/

- o Ni wapi ambapo wasichana wanajihisi wakiwa na wasiwasi wakiwa na wahudumu wa kibinadamu katika jamii yako?

**Kisha waambie wasichana waangalie ramani nzima:**

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Weka alama kwa nukta 3 kwenye ramani ambapo umesikia kuwa wanawake na wasichana wananyanyaswa.<br>Uliza ikihitajika: Shuleni/vituo vya kujifunzia, sokoni, nyumbani, vituo/maeneo ya kusambaza chakula, vituo vya maji, au sehemu nyingine yoyote ambayo una wasiwasi nayo. | ● ● ● | **Nyekundu** |

**Kisha, uliza kikundi maswali haya:**

- Je, unaweza kusema zaidi kuhusu wasiwasi huu? Ni nani ananyanyasa wanawake na wasichana?
- Je, kuna mtu yeyote amewahi kuzungumza nawe au kukupa taarifa kuhusu dhuluma na udhalilishaji wa kingono?
- o Uliza: Ikiwa ndiyo, ulijulia wapi na kutoka kwa nani?

Uliza: Wazazi, familia, shirika lisilo la kiserikali (NGO), tukio, n.k. (Ruka swali ikiwa hawajapokea habari kuhusu suala hili.)

- Je, umewahi kusikia kuhusu udhalilishaji na dhuluma ya kingono?
- o **Uliza:** Kama ndiyo, umesikia nini?
- o **Uliza:** Ikiwa hapana, fafanua udhalilishaji na dhuluma ya kingono (kama inavyofafanuliwa na kupitia mifano kwa njia inayoambatana na umri); uliza ikiwa kuna neno kwa lugha ya wenyeji linalotumika, na ikiwa lipo, tumia neno hilo.

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Wanajamii wanaoripoti kutokuwa na wasiwasi katika kutumia utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na wanaoelewa jinsi ya kuripoti malalamiko na mchakato wa kufuatilia |

- Je, mtu anaweza kufanya nini akishuhudia au kushuku kuwa udhalilishaji na dhuluma ya kingono inafanyika katika jamii yako?
- o **Uliza:** Ni kwa njia gani anaweza kuwasilisha malalamiko (yaani, ana kwa ana, kwa simu)? Kwa nani?
- o **Uliza:** Msichana katika jamii yako anaweza kufanya nini akipitia hali hii? Je, wasichana wanajua ni wapi na jinsi ya kuripoti udhalilishaji na dhuluma ya kingono?
- o **Uliza:** Wasichana wanaweza kwenda wapi ili kupata usaidizi?
- o **Uliza:** Je, unafikiri wasichana watajisikia huru kuripoti? Wasichana wanaamini mahali hapo? (Chora taswira hapa kulingana na majibu ya awali, kama vile dereva aliyeomba upendeleo na ambaye shirika lake hutoa huduma nzuri). Je, wasichana wanaamini kwamba kitu kizuri kitafanyika ikiwa wataripoti?

**Kisha, waombe washiriki:**

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Waweke alama ▲ kwenye ramani wakitumia kuonyesha mahali malalamiko yanaweza kuwasilishwa. | ▲ | **Bluu** |
| Waweke alama ■ kwenye ramani wakitumia kuonyesha mahali manusura anaweza kwenda kuwasilisha malalamiko juu ya yale ambayo amepitia au bado anapitia na kupata usaidizi. | ■ | **Bluu** |

### Hatua ya 8. Ushauri wa kuhakikisha mazingira salama zaidi

- Ni nini kitafanya jamii yako kuwa salama zaidi kwa wasichana?
- Je, kuna jambo lolote kwenye mada hizi ambalo sikuuliza lakini ungependa kulijadili?

**Hitimisha majadiliano**

- Shukuru washiriki kwa muda wao na kujali katika mazungumzo.
- Tambua michango na umakini wa wahojiwa na utoe muhtasari wa mazungumzo. Wahakikishie na uwakumbushe kwamba hakuna kitu kwenye ramani au kumbukumbu ambacho kinaweza kuwatambulisha na kwamba hawatatajwa.
- Wakumbushe washiriki kuhusu madhumuni ya mkutano. Wakumbushe kwamba ungependa kuweka ramani kwa madhumuni hayo.
- Tena, waeleze kwamba huenda ukafanya zoezi hili na makundi mengine katika jamii.
- Waulize washiriki tena ikiwa wametoa idhini yao ya kuturuhusu tutumie maelezo yanayotokana na ramani na majadiliano.
- Wakumbushe washiriki makubaliano yao ya kudumisha usiri na kwamba wasishiriki habari au majina ya washiriki wengine na wajamii wengine.
- Ikiwa mtu yeyote atataka kuzungumza faraghani, waambie kwamba mratibu na mnakili kumbukumbu watapatikana baada ya mkutano.
- Wajulishe washiriki kuhusu ni wapi wanaweza kukupata, iwapo mtu yeyote angependa kuzungumza nawe zaidi kuhusu kazi unayofanya.
- Uliza ikiwa kuna maswali, mawazo ya kufunga, maarifa, mambo waliyoona au maoni ambayo mtu yeyote angependa kuongeza kabla ya kufunga.
- Washukuru tena na ufunge mjadala.

# Mwongozo wa Majadiliano ya Kikundi cha Wanawake

**MUHIMU:** Hakikisha **umepata idhini** kutoka **kwa** washiriki wote **kabla ya** kuanza kikao cha Majadiliano ya Kikundi Lengwa (FGD). Inashauriwa kuwa usiwe na **zaidi ya washiriki wanane** katika kikao chako cha FGD. Angalia *Sehemu ya 2. Hati ya Mwongozo wa Utekelezaji* wa mchakato wa kupata Idhini na *Kiambatisho cha Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Barometer na Idhini* ya kutumiwa na Fomu ya Utoaji Idhini.

## Nyenzo zinazohitajika:

- Karatasi ya kuandikia
- Kalamu za kutia alama za rangi tofauti [Ikiwa huna za rangi tofauti, tumia alama tofauti kwenye ramani]

## Kuanza kwa kikao cha FGD

**Wakati washiriki wote wamekusanyika, mratibu wa FGD anafaa kuanza kwa utangulizi huu [tafadhali rekebisha palipoonyeshwa]:**

Habari? Jina langu ni ________ na ninafanya kazi katika _______. Ninaandamana na mwenzangu _____ ambaye anafanya kazi katika [shirika lile lile/lingine] na atakuwa akituandikia kumbukumbu. Mwenzangu ___________ atakuwa akikalimani [ikiwa mkalimani atahitajika].

Tuko hapa leo ili kujadiliana nawe baadhi ya vipengele vya usaidizi wa kibinadamu ambao umepokea. Tutakuwa tukichora ramani pamoja ili kutusaidia kuelewa usaidizi unaopatikana katika jamii yako na masuala yaliyopo ya usalama kwa wanawake na wasichana. Tutatumia taarifa hii kutusaidia kutetea [kuuliza] wadau muhimu kutoa usaidizi wa kibinadamu ulio salama na unaopatikana kwa urahisi zaidi kwa wanawake na wasichana.

Majadiliano na ramani hii itakuwa siri. Mratibu (mimi), mnakili kumbukumbu na mkalimani sote pia tumeahidi kudumisha usiri. Hili linamaanisha kwamba taarifa yoyote mtakayoshiriki nasi leo haitashirikiwa na mtu mwingine yeyote. Huhitaji kutupatia majina yako au taarifa yoyote ya kibinafsi. Huhitaji kutuambia kuhusu hadithi zako mahususi. Ramani na majadiliano yetu hayatatutambulisha kwa hivyo hayawezi kuhusishwa nawe binafsi. Katika ramani na katika kumbukumbu zetu, hakuna utambulisho wa mtu utakaotajwa.

Kushiriki kwako katika mkutano huu ni kwa hiari kabisa. Ikiwa unahisi wasiwasi wakati wowote, uko huru kuondoka, na haitaathiri kwa njia yoyote huduma na usaidizi unaopokea na unaostahili. Majadiliano yatadumu kwa muda usiozidi saa moja. [Kama unafikiri utahitaji dakika 90, kwanza jadili hili na washiriki wa FGD ili uhakikishe kuwa wana muda wa kutosha].

Tutakuwa tukifanya zoezi hili na makundi mengine ya wanawake na wasichana katika jamii.

Je, kuna kitu chochote ambacho ungehitaji ili uwe salama na ushiriki bila wasiwasi? Je, kuna jambo lingine tunaloweza kufanya ili kukusaidia ujisikie bila wasiwasi? Je, una maswali yoyote ambayo ungependa kuuliza kabla hatujaendelea?

*Hakikisha kuwa maswali yote yamejibiwa kikamilifu na uangalie tena ili uhakikishe kuwa hakuna chochote kitakachoachwa bila kujibiwa.*

## Zana ya Majadiliano ya Kikundi Lengwa: Wanawake

### 1. Maelezo ya msingi ya kikundi

**Tarehe:**

**Mahali:** ____________________________________________

**Mratibu:** ___________________________________________

**Mnakili kumbukumbu:** _________________________________

**Je, ukalimani unahitajika? NDIYO HAPANA**

Ikiwa ndiyo, ni ukalimani kutoka _______________ (lugha) hadi ______________(lugha)

**Mkalimani:** __________________________________

**Idadi ya washiriki:** _______

**Umri wa washiriki wa kikundi lengwa (chagua aina zote zinazofaa):**

- ☐ Miaka 20-24
- ☐ Miaka 25-40
- ☐ Zaidi ya miaka 40

### 2. Ramani na majadiliano

#### Hatua ya 1. Kuchora jamii na huduma

Kipe kikundi kalamu na karatasi ya chati ya kupindua, ambayo inapaswa kuwa imechorwa muhtasari kwa KALAMU NYEUSI wa nyumba chache za kuwakilisha jamii. Eleza uwakilishi huu kwenye ramani ili kikundi kielewe.

*Hakikisha kila mtu anaweza kuona/kufikia ramani.*

**Kisha waalike washiriki waongeze kwa kutumia KALAMU NYEUSI vipengele vingine vyote muhimu katika maisha na jamii yao, ikijumuisha huduma na vistawishi vinavyopatikana na mahali vilipo**. Pia waongeze nyumba zaidi, barabara, njia, maeneo ya kawaida ndani na nje ya makazi/eneo.

Ikihitajika, wahimize waongeze vitu kama vile: vyoo; mabafu; vituo vya maji; vituo vya usambazaji; vituo vya afya; nafasi za watoto, wanawake au wasichana; vituo vya jamii; viwanja vya kucheza; masoko; shule; na kadhalika.

Washiriki watakapohisi kuwa ramani inawakilisha jamii yao, nenda kwenye hatua inayofuata.

#### Hatua ya 2. Mashauriano na wanawake na wasichana

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Kadirio la idadi ya watu ambayo vistawishi na miundombinu ya WASH (maji, usafi wa mazingira na ustawi) inashughulikia maswala na mahitaji ya usalama ya wanawake na wasichana kupitia usanifu na mpangilio unaofaa na ufikiaji sawa<br><br>Kadirio la idadi ya watu ambayo jinsi kambi hiyo imewekwa, jinsi inavyodumishwa na miundombinu iliyopo, inashughulikia maswala na mahitaji ya usalama ya wanawake na wasichana kupitia usanifu, mpangilio na ufikiaji unaofaa |

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Soma swali hapa chini. Kwenye ramani, weka alama ya kitone cheusi kwenye huduma na/au vistawishi vyote ambavyo wasichana waliripoti kuwa walishauriwa wakati wa mchakato wa kuvianzisha au kuvijenga katika jamii. | • | **Nyeusi** |

**Tumia maswali haya kukusaidia katika jukumu hili:**

- Wafanyakazi wa misaada walipokuja katika eneo lako, je walizungumza na wanawake na wasichana katika jamii yako kuhusu mojawapo ya sehemu zifuatazo ulizochora kwenye ramani?

o Kidokezi (ikihitajika): Je, waliuliza maswali kuhusu usalama wa wasichana na kile ambacho wasichana wangependelea?

  - Vistawishi (WASH - vyoo, bafu, vituo vya maji)
  - Mpangilio wa kambi (kwa mfano, taa, barabara/njia, ushikaji doria)
  - Huduma (k.m., aina - nafasi salama, vituo vya afya, n.k.; nafasi/mahali; ufikiaji)
  - Taarifa (k.m., mbinu, lugha, ufikiaji)
  - Usambazaji (vifaa vya hadhi, vitu visivyo vyakula (NFI), chakula)

Kisha, **weka alama ya kitone cheusi kando ya kila kituo ambapo wanawake na wasichana walishauriwa**.

### Hatua ya 3. Wasiwasi na sehemu na maeneo yasiyo salama kwa wanawake na wasichana

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Ukiangalia ramani, weka alama ya MDUARA kwa kutumia MSTARI THABITI eneo au mahali popote ambapo si salama kwa wanawake na wasichana wakati wa mchana. | ◯ | **Nyekundu** |
| Ukiangalia ramani, weka alama ya MDUARA kwa kutumia MSTARI WA VITONE eneo au mahali popote ambapo si salama kwa wanawake na wasichana usiku. | ◌ | **Nyekundu** |

**Vidokezo vinavyoweza kutumiwa (ikihitajika) - Unaweza kuuliza maswali haya ili kusaidia kikundi kufikiria ni maeneo gani ambayo si salama katika jamii yao:**

- Je, una wasiwasi wa aina gani kuhusu hatari zinazowakabili wanawake na wasichana katika jamii yako? Je, ni mambo gani ambayo huwafanya wanawake wajisikie kuwa na hofu au kutokuwa salama zaidi? Orodhesha haya na utie alama kwenye ramani ikiwa kuna jambo jipya.
- Ni nini huwafanya wanawake na wasichana kuhisi wasiwasi au woga wakiwa nyumbani? Katika jamii yao?
- Je, wanawake na wasichana wanaweza kutembea kwa usalama hadi kwenye vituo vya afya/nafasi salama kwa chini ya dakika 20? (*Uliza**:** Ikiwa hawatembei kwenda kwenye vituo vya afya, uliza jinsi wanavyofika kwenye vituo vya afya, ni vituo vipi wanavyoweza kufikia, inachukua muda gani kufika hapo, wanaandamana na nani, n.k.*.)
- Je, wanawake wanahisi salama wanapoenda kuchota maji? Kama sivyo, kwa nini? Na wasichana je? Wakati wa kuchota maji, je, huwa mara nyingi unasubiri kwa muda mrefu? Ikiwa ndivyo, unasubiri kwa muda gani (kwa mfano, mara nyingi kuna foleni na mitungi ya maji iliyopangwa, na wanawake na wasichana wakisubiri kuchota maji)?
- Je, huwa unachota maji kabla ya macheo au baada ya machweo? *(Ruka ikiwa maji ya bomba yanapatikana majumbani).*
- Je, muda wa wastani wa kusubiri kutumia choo ni zaidi ya dakika 10? *(Ruka ikiwa maji ya bomba yanapatikana majumbani).*

## Hatua ya 4. Vifurushi vya hadhi (ruka ikiwa hakuna vifurushi vya hadhi ambavyo vimesambazwa)

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Kadirio la idadi ya wanawake na wasichana ambayo imepokea vifurushi vya hadhi vinavyofaa kulingana na mapendeleo na mahitaji yao |

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Weka alama ya + kwenye ramani katika maeneo ambapo vifurushi vya hadhi vimesambazwa. | + | Buluu |
| Weka alama ya X kwenye ramani ikiwa eneo ambapo vilisambazwa lilikuwa si salama kwa wanawake na wasichana. | X | Nyekundu |

**Kisha, uliza kikundi maswali haya:**

- Unapowafikiria wanawake na wasichana unaowajua—wanafamilia (mama, dada, binamu, shangazi, n.k.), marafiki, majirani—je, wengi wao wamepokea vifurushi vya hadhi?
- Je, unaweza kutuambia ni nini kilikuwa ndani ya kifurushi cha hadhi ulichopokea?
    - **Uliza:** Uliridhika kwa kiasi gani na vitu ambavyo vilijumuishwa kwenye kifurushi hicho? Kwa nini uliridhika au hukuridhika? *Ongoza majadiliano ndani ya kikundi ili kukubaliana juu ya kiwango cha kuridhika. Ikiwa kikundi hakiwezi kukubaliana, kumbuka sifa tofauti zilizotolewa na idadi ya washiriki.*
- Je, unakumbuka nini kuhusu utaratibu wa kwenda kuchukua kifurushi chako cha hadhi?
    - **Swali:** Ni nani aliyesambaza kifurushi chako cha hadhi? Ni nani aliyehusika katika usambazaji wa vifurushi hivi?
    - **Uliza:** Je, vifurushi hivi vilisambazwa na wanaume au wanawake?
- Je, usambazaji wa vifurushi hivi umeathiri vipi (ikiwa umeathiri) uhusiano kati ya jamii ya wahamiaji na jamii ya wenyeji?
    - **Uliza:** Ni aina gani ya ujumbe kwa jamii ulitumiwa kuhusu usambazaji ili kusaidia jamii kuelewa na kusaidia katik usambazaji wa vifurushi hivi?

## Hatua ya 5. Usambazaji wa vyakula na vitu visivyo vyakula (NFI) (ruka hatua hii ikiwa hakujakuwa na usambazaji)

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Sehemu ya watu wanaoelezea wasiwasi wao kuhusu usalama ndani ya na karibu na maeneo ya usambazaji wa NFI na yale yanayohusiana na Usalama wa Chakula na Kilimo (FSA) |

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Weka alama ya ~ kwenye ramani katika maeneo ambapo ugawaji wa NFI/ chakula umefanywa | ~ | Buluu |
| Weka alama ya X kwenye ramani ikiwa eneo hilo la usambazaji halikuwa salama kwa wanawake na wasichana | X | Nyekundu |

**Kisha, uliza kikundi maswali haya:**

- Usambazaji ulikuwa lini? Ni nini kilisambazwa ndani ya mwezi uliopita?
    - **Uliza:** Ikiwa “hamna,” alika kikundi kitoe maoni yao kuhusu hili. Kwa nini wanafikiria hakujakuwa na usambazaji wowote?

- Ni nini kilisambazwa? Ni nani aliyesambaza?
- Je, jamii iliarifiwa vipi kuhusu mahali, wakati na namna ya kuendea vitu vilivyosambazwa?
- Uliza: Wakati wa kuendea vitu vilivyosambazwa, kuna nyakati maalum zilizotengewa wanawake kukusanya vitu hivyo na/au kuna mambo mengine hasa yanayofanywa kwa ajili ya wanawake wakati wa kwenda kwenye maeneo ya usambazaji?
- Je, jambo hili limeathiri vipi, ikiwa limeathiri, usalama wa wanawake na wasichana katika jamii yako?

### Hatua ya 6. Nafasi salama (ruka ikiwa hakuna nafasi salama)

| | |
|---|---|
| **Kipimo cha Barometa** | Kadirio la idadi ya watu ambao nafasi salama kwa wanawake na wasichana - pamoja na ushughulikiaji wa visa na usaidizi wa kisaikolojia na kijamii - zimeanzishwa, ni salama kufikiwa na zimewekwa umbali unaofaa<br><br>Idadi ya wafanyakazi wa kike katika huduma na programu za kukabiliana na ukatili wa kijinsia (UWAKI), huku wanawake wakichukua tu nafasi zote za mstari wa mbele katika kutoa usaidizi na huduma |

**Nenda kwenye nafasi salama ambazo kikundi kilikuwa kimewekea alama kwenye ramani:**

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Chora kitone kikubwa katika sehemu zote ambapo mwanamke au msichana katika jamii yako anaweza kwenda ikiwa anaogopa na anataka usaidizi. (Kumbuka: Hizi zinaweza kuwa sawa au tofauti na nafasi salama ambazo tayari zimetambuliwa). | ● | Kijani |
| Chora mstari kwenye ramani kuelekea nafasi zozote za wanawake na wasichana ambazo si salama kwao kusafiri. | ——— | Nyekundu |
| Weka alama ya X kando ya nafasi yoyote kati ya hizo ambazo si salama na kuna wasiwasi kwa wanawake kuwa mle. | X | Nyekundu |

### Kisha, uliza kikundi maswali haya:

- Je, wanawake wote na/au wasichana wanafikia nafasi salama? Je, kuna baadhi ya wanawake na/au wasichana ambao hawaendi au hawawezi kufikia nafasi salama? Kwa nini?
- Je, wanawake na/au wasichana wanapenda nini kuhusu nafasi salama (k.m., huduma, shughuli, taarifa, n.k.)?
- Je, kuna sababu zozote ambazo wewe au wanawake wengine huchagua kutokwenda katika nafasi salama (k.m., muda wa kusafiri, usalama, wafanyakazi, mahali nafasi hiyo ilipo, n.k.)?

o Vidokezi zaidi (ikiwa tu vinahitajika):

- Je, wafanyakazi ni wanaume, wanawake (ikiwa ni pamoja na wale wa kujitolea) au ni mchanganyiko?
- Ni nani yuko kwenye nafasi hiyo salama?
- Je, unajihisi bila wasiwasi na salama kwa kiasi gani ukiwa hapo?
- Je, kuna wanawake au wasichana wowote ambao hawawezi kufikia nafasi hizi?
- Je, nafasi hiyo iko katika eneo ambalo ni rahisi na salama kwako kufika? Ikiwa haiko, kwa nini?
- Je, unahitaji kusafiri muda gani ili kufika kwenye nafasi salama?
- Je, unajihisi salama unapotembea kwenda kwenye nafasi hiyo?
- Ni mara ngapi wanawake na wasichana wanaenda kwenye nafasi salama na kwa sababu gani? Kuna shughuli fulani ambayo ni maarufu?

## Hatua ya 7. Taratibu za kuwasilisha malalamiko katika jamii

| **Kipimo cha Barometa** | Taratibu za kina za kuwasilisha malalamiko katika jamii (CBCM) na zana saidizi za kuhamasisha zimetengenezwa, kujaribiwa na jamii na zinatumiwa na mashirika yote |
|---|---|

**Muhimu! Kumbusha kikundi kisishiriki maelezo yoyote ya kibinafsi kuwahusu wao au wengine na washiriki tu habari ambayo wanahisi kuwa ni salama kushiriki. Usishiriki habari kuhusu visa au matukio maalum.**

- **Swali (chagua swali 1 kati ya haya 3 ambalo unaonelea linafaa/ linaeleweka vyema na kikundi chako):**

o Je, umewahi kuona mtu anayefanya kazi kwenye kambi (k.m., mpishi, mlinzi, n.k.) akimpa mtu yeyote maji, chakula au vifaa ili kupata upendeleo? AU/

o Je, umewahi kuona mtu anayefanya kazi kwenye kambi (k.m., mlinzi, mtu anayesambaza bidhaa, n.k.) akitumia mamlaka aliyo nayo kwa manufaa yake binafsi (hii inaweza kuwa kuomba upendeleo ili kumpa kitu anachodhibiti, kama vile chakula au vifaa?) AU/

o Ni wapi ambapo wanawake na wasichana wanajihisi wakiwa na wasiwasi wakiwa na wahudumu wa kibinadamu katika jamii yako?

**Kisha waombe washiriki waangalie ramani nzima:**

| Jukumu | Alama | Rangi |
|---|---|---|
| Kulingana na tajriba yako, weka alama kwa nukta 3 kwenye ramani ambapo umesikia visa vya udhalilishaji na dhuluma ya kingono vinatokea katika jamii yako<br><br>Uliza ikihitajika: Shuleni/vituo vya kujifunzia, sokoni, nyumbani, vituo/ maeneo ya kusambaza chakula, vituo vya maji, au sehemu nyingine yoyote ambayo una wasiwasi nayo. |  | **Nyekundu** |

**Kisha, uliza kikundi maswali haya:**

- Je, unaweza kusema zaidi kuhusu wasiwasi huu? Je, unajua kama visa hivi vinatokea mara kwa mara? Ni kikundi kipi kinachotekeleza dhuluma hizi (k.m., watu katika jeshi, jamii, wahusika wa kibinadamu, n.k.)
- Je, kuna mtu yeyote amewahi kuzungumza nawe au kukupa taarifa kuhusu dhuluma na udhalilishaji wa kingono?
  - o **Uliza:** Ikiwa ndiyo, ulijulia wapi na kutoka kwa nani?
  - o **Ulizza:** Shirika lisilo la kiserikali (NGO), rafiki, jirani, mtu mwingine, tukio fulani, nk. (Ruka swali ikiwa hawajapokea habari kuhusu suala hili.)
- Je, umewahi kusikia kuhusu dhana ya udhalilishaji na dhuluma ya kingono?
  - o **Uliza:** Kama ndiyo, umesikia nini?
  - o **Uliza:** Ikiwa hapana, fafanua udhalilishaji na dhuluma ya kingono (kama inavyofafanuliwa na kupitia mifano); uliza ikiwa kuna neno kwa lugha ya wenyeji linalotumika, na ikiwa lipo, tumia neno hilo.

| **Kipimo cha Barometa** | Wanajamii wanaoripoti kutokuwa na wasiwasi katika kutumia utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na wanaoelewa jinsi ya kuripoti malalamiko na mchakato wa kufuatilia |
|---|---|

- Kulingana na tajriba yako, mtu anaweza kufanya nini akishuhudia au kushuku kuwa udhalilishaji na dhuluma ya kingono inafanyika katika jamii yako?
  - o **Uliza:** Ni kwa njia gani anaweza kuwasilisha malalamiko (yaani, ana kwa ana, kwa simu)? Kwa nani?

- Je, mwanamke anaweza kufanya nini ikiwa atapitia udhalilishaji na dhuluma ya kingono?
    - o **Uliza:** Ni kwa njia gani anaweza kuwasilisha malalamiko (yaani, ana kwa ana, kwa simu)? Kwa nani?

**Kisha, waombe washiriki:**

| Jukumu | Symbol | Color |
|---|---|---|
| Waweke alama kwenye ramani wakitumia ▲ kuonyesha mahali malalamiko yanaweza kuwasilishwa. | ▲ | **Bluu** |
| Waweke alama kwenye ramani wakitumia ■ kuonyesha mahali manusura anaweza kwenda kuwasilishamalalamiko juu ya yale ambayo amepitia au bado anapitia na kupata usaidizi. | ■ | **Bluu** |

**Kisha, uliza kikundi maswali haya:**

- Je, habari kuhusu kuwasilisha malalamiko na kuripoti inapatikana katika lugha unayoelewa?
- Je, unajihisi kuwa unajua ni wapi na namna ya kuripoti udhalilishaji na dhuluma ya kingono katika jamii hii?
- Je, unadhani wanawake wanajihisi salama kiasi gani kukija ni kuripoti kwa njia hii? Je, wanawake wanaiamini njia hii? Je, wanawake wanafikiri kuwa hatua yoyote itachukuliwa?
- Na ikiwa kuna kitu kinachoweza kuzuia wanawake kuripoti? (Chora taswira hapa kulingana na majibu ya awali, kama vile dereva aliyeomba upendeleo na ambaye shirika lake hutoa huduma nzuri).

## Hatua ya 8. Ushauri wa kuhakikisha mazingira salama zaidi

- Je, nini kinaweza kufanywa ili kuhakikisha mazingira salama zaidi kwa wanawake na wasichana katika jamii yako?
- Je, kuna jambo lolote kwenye mada hizi ambalo sikuuliza lakini ungependa kulijadili?

**Hitimisha majadiliano**

- Shukuru washiriki kwa muda wao na kujali katika mazungumzo.
- Tambua michango na umakini wa wahojiwa na utoe muhtasari wa mazungumzo. Wahakikishie na uwakumbushe kwamba hakuna kitu kwenye ramani au kumbukumbu ambacho kinaweza kuwatambulisha na kwamba hawatatajwa.
- Wakumbushe washiriki kuhusu madhumuni ya mkutano. Wakumbushe kwamba ungependa kuweka ramani kwa madhumuni hayo.
- Tena, waeleze kwamba huenda ukafanya zoezi hili na makundi mengine katika jamii.
- Waulize washiriki tena ikiwa wametoa idhini yao ya kuturuhusu tutumie maelezo yanayotokana na ramani na majadiliano.
- Wakumbushe washiriki makubaliano yao ya kudumisha usiri na kwamba wasishiriki habari au majina ya washiriki wengine na wajamii wengine.
- Ikiwa mtu yeyote atataka kuzungumza faraghani, waambie kwamba mratibu na katibu watapatikana baada ya mkutano.
- Wajulishe washiriki kuhusu ni wapi wanaweza kukupata, iwapo mtu yeyote angependa kuzungumza nawe zaidi kuhusu kazi unayofanya.
- Uliza ikiwa kuna maswali, mawazo ya kufunga, maarifa, mambo waliyoona au maoni ambayo mtu yeyote angependa kuongeza kabla ya kufunga.
- Washukuru tena na ufunge mjadala.

# Kiolezo cha Kumbukumbu za Majadiliano ya Kikundi

**Maelezo ya msingi ya kikundi**

**Tarehe**:

**Mahali:** ________________________________

**Mratibu:** __________________________________________

**Mnakili kumbukumbu:** __________________________________________

**Je, ukalimani unahitajika?** NDIYO HAPANA

Ikiwa ndiyo, ukalimani kutoka __________________ (lugha) hadi __________________ (lugha)

**Mkalimani:** __________________________________________

**Idadi ya washiriki:** ________

**Washiriki**

- Wasichana walio balehe
- Wanawake

**Umri wa washiriki wa kikundi lengwa (chagua aina zote zinazofaa):**

- ☐ Miaka 10-14
- ☐ Miaka 15-19
- ☐ Miaka 20-24
- ☐ Miaka 25-40
- ☐ Zaidi ya miaka 40

| Nambari ya Hatua | Andika/chapa majibu ya maswali (tumia Mwongozo wa Kunakili Kumbukumbu) | Unaona nini? (hisia za washiriki) |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | | |
| 4 | | |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | | |
| 6 | | |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | | |

# Zana ya Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu

Zana hii ni mwongozo wa kufanya Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KIIs) na wahusika, wanaharakati, vikundi, mashirika na mitandao ya haki za wanawake inayofanya kazi ndani, na pamoja na jamii zao, kama sehemu ya ukusanyaji wa data ya Barometa. Madhumuni ya mahojiano haya ni kuelewa, kutokana na mitazamo na uzoefu wa wanawake hawa, kama: watu hawa na vikundi hivi vimeshirikishwa na kuhusishwa katika usaidizi wa kibinadamu katika eneo lao; kama usaidizi wa kibinadamu unakidhi mahitaji ya wanawake na wasichana; na ni mabadiliko gani wangependa kuona katika mfumo wa kibinadamu katika siku zijazo. Inapendekezwa kuwa ufanye mahojiano na **mhusika binafsi/ mtetezi wa haki za kibinadamu za wanawake au mtu binafsi au kikundi kidogo cha wanawake wasiozidi watatu** kutoka kwa kundi, shirika au mtandao mmoja. Kuhusisha zaidi ya washiriki watatu kunaweza kusababisha mazungumzo yasiyo na kina au umakini. Ikiwa unaendesha mahojiano haya ya KII katika lugha zingine, tafsiri zana hii kabla ya kuanza.

Unaweza kuhitaji yafuatayo: Mkalimani; Mnakili kumbukumbu; na nyenzo kama vile chati ya kupindua, karatasi za madokezo zinazonata au kalamu, kulingana na jinsi washiriki wangependa kuhojiwa. Kwa mfano, wengine wanaweza kupendelea mazungumzo, wengine wanaweza kupendelea kuchora picha, na wengine huenda wakapendelea mchanganyiko wa mbinu zote mbili. Maswali yanakusudiwa kuwa mwongozo, na utahitaji kuyarekebisha au kupatia mengine kipaumbele, kulingana na muktadha wako.

## Anza

Jitambulishe (Mratibu, Mnakili Kumbukumbu na Mkalimani, ikiwa unaye); tambulisha shirika lako pia. Alika washiriki wajitambulishe. Kisha:

- Toa muhtasari mfupi wa kipimo cha Barometa na madhumuni ya mahojiano ya KII (kwa mfano, ili kuelewa jinsi wanaharakati, vikundi, mashirika na mitandao inayoshughulikia masuala ya wanawake inakabiliwa na janga la kibinadamu na utoaji usaidizi; ikiwa na jinsi wanashirikishwa na mfumo wa kibinadamu na wanaobuni sera; vikwazo na changamoto wanazokabiliana nazo; na nini kinahitaji kubadilishwa ili kukidhi mahitaji na haki za wanawake na wasichana katika mazingira walimo).
- Eleza kwamba mahojiano yatakuwa ya siri na hayatawatambulisha washiriki. Aidha maelezo yote watakayotoa hayatawatambulisha na hayataweza kuhusishwa nao binafsi au mashirika yao. Eleza kwamba kumbukumbu zote za mahojiano zinachapwa kila mwisho wa siku na nakala zote zilizoandikwa kuharibiwa; nakala pepe ya kumbukumbu zilizochapwa huwekwa mahali ambapo panalindwa kwa nenosiri.
- Eleza kwamba utakuwa ukitumia taarifa na mchango wao kama sehemu ya utetezi utakaofanya ukitumia Barometa.
- Eleza kwamba utawasiliana nao baada ya kukamilisha ukusanyaji wa data ili kuwaalika washiriki katika uthibitishaji wa data, uandaaji wa mapendekezo na utetezi, ikiwa wangependa kushiriki zaidi.
- Eleza kwamba hatutahitaji zaidi ya saa 1.5, na ikiwa watahitaji kuondoka mapema zaidi ya hapo, tutamaliza wakiwa tayari.
- Waulize washiriki jinsi wangependa kushughulikia mahojiano na maswali elekezi (hapa chini). Muhimu zaidi, wacha mshiriki/washiriki wakuongoze katika mbinu utakayotumia. Unaweza kupendekeza njia zifuatazo: mazungumzo wazi ambapo mratibu (wewe) anauliza maswali ya mwanzo na vidokezi; kuzungumza huku mkileta vipengele vya kuona, kuchora ramani na kuongeza vipengele kwenye mjadala; au mbinu yenye mpangilio zaidi ya maswali na majibu.

Waulize kama kuna chochote wanachohitaji ili kujisikia salama na bila wasiwasi katika mkutano na mahali mlipo, na kama wana maswali yoyote kabla ya kuanza. Hakikisha umejibu maswali yoyote waliyo nayo kabla ya kuanza.

**1. Utambulisho, historia na mizizi ya kikundi/shirika/ mtandao**

- Niambie kuhusu kikundi/shirika/mtandao/harakati zako. Unafanya kazi wapi? Unafanya kazi gani?
    - ***Vidokezi:*** *Je, kikundi/shirika/mtandao/harakati yako ilianzishwaje? Ni nini kilichochea kuanzishwa kwake? Maono na malengo yenu ni yapi? Umefikaje mahali ulipo leo? Ni watu wangapi wanaohusika, na unafanya kazi na nani?*
- Je, unaweza kusema ni changamoto gani kubwa unayokutana nayo katika kazi yako? Je, unaipunguzaje?
- Je, unaweza kusema ni hadithi gani kubwa ya mafanikio uliyopata kufikia sasa? Je, umekuwa na athari gani katika jamii hadi sasa?

**2. Uchunguzi kifani wa janga la kibinadamu**

- Je, umewahi kukumbana au kushuhudia janga la kibinadamu hapo awali? Eleza kwa ufupi jinsi hali hiyo ilivyokuwa.
- Je, ni baadhi ya masuala gani kuu ambayo wanawake na wasichana wanakabiliana nayo wakati wa janga hili la kibinadamu?
    - *Je, ni aina gani ya usaidizi ambao wanawake na wasichana wanahitaji wakati wa janga la sasa?*
- Je, kikundi/shirika/mtandao/uanaharakati wako unashughulikiaje janga hilo (au unataka kuchukua hatua zipi)? Ikiwa hauhusiki, ni nini kikundi/shirika/mtandao/uanaharakati wako unaweza kuleta katika usaidizi unaotolewa wa kibinadamu?
- Je, mgogoro umeathiri vipi kikundi/shirika/mtandao/uanaharakati wako?
    - *Kidokezi: Je, unakabiliwa na changamoto mpya? Je, unakabiliwa na upinzani au kulipiza kisasi kwa kazi yako au uanaharakati wako? Je, uanaharakati wako unabadilika kutokana na mgogoro wa sasa?*

**3. Huduma za usaidizi na utoaji misaada**

- Una maoni gani kuhusu usaidizi wa kibinadamu? Je, unakidhi mahitaji na vipaumbele halisi vya wanawake na wasichana?
    - ***Vidokezi:*** *Je, wanawake na wasichana wanafurahia/ wameridhishwa na usaidizi huo? Je, wanapata huduma yoyote? Je, huduma hizi ziko salama na zinapatikana kwa kiasi gani kwa wanawake na wasichana? Je, sekta tofauti (k.m., ukatili wa kijinsia (UWAKI); afya; maji, usafi wa mazingira, usafi (WASH); bidhaa zisizo chakula (NFI), n.k.) zinasaidia kwa ufanisi wa juu au wa chini? Je, mipango/miongozo ya kibinadamu/taratibu za kawaida za uendeshaji (SOPs), n.k. zinaonyesha mahitaji unayoona na unayohitaji?*
    - ***Vidokezi zaidi:*** *Je, mgogoro/ usaidizi huu wa sasa unalingana vipi na ule uliotolewa awali mahali hapa? Je, mafunzo ya awali yanajumuishwa katika usaidizi unaotolewa sasa na jumuiya ya kibinadamu ili kuboresha?*
    - Je, kuna njia salama za kulalamika kuhusu utayarishaji wa programu za kibinadamu na/au mwenendo mbaya wa wahudumu wa kibinadamu? Je, malalamiko (nyeti) yanashughulikiwa ipasavyo na kwa usiri?
    - *Je, kuna sera yoyote ya ulinzi inayotumika?*

**4. Ushirikishwaji, uongozi na maamuzi**

- Je, wanawake na wasichana wanashauriwa ili kuchangia na kuamua usaidizi wa kibinadamu kwa njia yoyote, ikiwa ni pamoja na huduma na usaidizi unaokusudiwa kwao?
    - ***Kidokezi:*** *Kwa kipimo cha 1 (hata kidogo) - 10 (wakati wote), ni mara ngapi unaweza kusema wameshauriwa?*
- Je, kiwango chako cha kuhusika na kushiriki katika usaidizi wa kibinadamu kimekuwa kipi?
    - ***Vidokezi:*** *Na wahusika wengine wa kibinadamu? Taratibu za uratibu wa kibinadamu? Wafadhili? Wale wanaoandaa mipango na miongozo ya hatua za kibinadamu? Watunga sera na serikali?*
    - ***Vidokezi zaidi:*** *Je, wanaharakati/vikundi/mashirika/mitandao mingine ya mashinani, ya eneo husika au ya kitaifa inafikia mojawapo ya michakato na watu hawa? Ikiwa inafanya hivyo, ni kwa njia gani?*

- Je, ni vikwazo na changamoto gani unakumbana nazo katika kufikia mchakato wowote, watu na fursa zozote kati ya hizo?
- Je, unafahamu fursa za ufadhili na rasilimali za kibinadamu kwa ajili ya kikundi/shirika/mtandao/uanaharakati wako? Je, unakabiliwa na changamoto au vikwazo vyovyote katika kupata rasilimali hizi?
  - ***Kidokezi:*** *Je, zimeundwa na kuwekwa kwa njia ambazo unaweza kufikia?*
  - ***Kidokezi:*** *Je, unaweza kupata rasilimali za kutosha kusaidia kazi yako?*

**5. Mabadiliko**

- Kwa kuzingatia kile ambacho HAKIFANYI kazi kwa wanawake na wasichana katika hali ya sasa, ni mabadiliko gani ungependa kuona? Nini kinahitaji kufanywa kwa njia tofauti? Fikiria maeneo yafuatayo *(waulize wale ambao ni muhimu kwa muktadha)*:
  - Usaidizi wa sasa wa kibinadamu kwa wanawake na wasichana
  - Ugawaji na ufikiaji wa rasilimali
  - Kuhusishwa na kushirikishwa kwa wanawake na wasichana katika usaidizi kamili wa kibinadamu, kutoka ngazi za jamii hadi serikali
  - Wanawake wanaoongoza mchakato wa kibinadamu
- Je, ungependa kuwa na aina gani ya ushiriki katika usaidizi huu wa kibinadamu, au kwa mapana zaidi katika janga hili? Ni nini kitakusaidia kuwa na ushawishi, sauti au mamlaka zaidi katika viwango tofauti vya kufanya maamuzi?
- Ni hatua gani madhubuti zingehitajika kuchukuliwa ili kufika hapo? Na ni nani anayehitaji kuchukua hatua hizi?
- Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa kushiriki?

**Kufunga**:

Asante kwa kushiriki na kwa majibu yako ya kweli. Wape maelezo ya mawasiliano ya mratibu iwapo wahojiwa wangependa kuwasiliana naye tena kwa maelezo yoyote ya ziada, kufuatilia maendeleo ya kipimo cha Barometa, na kutaarifiwa na kuhusishwa katika hatua zaidi (kama vile hatua ya uthibitishaji).

# MWISHO

Jina la Mhoji …………………………………………………………………….

Cheo ……………………………………………………………………………………

Tarehe……………………………………. Sahihi……………………………………………

# Kiolezo cha majadiliano ya watoa taarifa muhimu

**Maelezo msingi ya mtu binafsi au kikundi**

**Tarehe:** ____________________________

**Eneo:** _________________________

**Mratibu:** ______________________________

**Mnakili wa kumbukumbu:** ______________________________

**Je, ukalimani unahitajika?** NDIYO HAPANA

Ikiwa unahitajika, utafanywa kutoka __________________ (lugha) hadi ____________________(lugha)

**Mkalimani:** ______________________________

**Idadi ya washiriki:** ________

**Jina la kikundi / shirika / mtandao wa wanawake:** ________________________

| Nambari ya swali | Andika / chapa majibu ya maswali (tumia mwongozo wa waandishi wa kumbukumbu) | Unaona nini? (majibu ya mshiriki) |
|---|---|---|
| 1 | | |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | | |
| 3 | | |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | | |
| 5 | | |

# Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia

## Mbinu za Kuzuia Unyanyasaji, Udhalilishaji na Dhuluma ya Kingono na Sera za Usalama

| **Vipimo** | **Kushughulikia Unyanyasaji, Udhalilishaji na Dhuluma ya Kingono** | **Shughuli** | **Hali** | **Alama** |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 1 | Je, katika muktadha wako, mratibu/wakala ina hati inayotangaza dhuluma, udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono kuwa kipaumbele kwa jumuiya ya usaidizi wa kibinadamu? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Halihusiki" |
| Swali la 2 | Je, uzuiaji wa unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono umejumuishwa katika Mpango wa Usaidizi wa Kibinadamu na tathmini ya mahitaji ya kibinadamu, na kutengewa bajeti? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui<br>☐ Halihusiki ikiwa<br>☐ hakuna hati kama hizo | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Halihusiki" |
| **Kipimo** | **Mitandao ya Kuzuia Unyanyasaji na Dhuluma ya Kingono (PSEA)** | **Shughuli** | **Hali** | **Alama** |
| Swali la 3 | Katika muktadha wako, kuna Mtandao wa PSEA unaofanya kazi au kisawe chake?<br>(Visawe vinaweza kuwa: mkusanyiko wa mashirika ya kibinadamu/ya wanawake yanayoshughulikia PSEA katika sekta mbalimbali) | Ukaguzi wa hati/ uchunguzi wa Jopo Kazi la PSEA au Mkutano wa Mtandao | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |
| Swali la 4 | Je, Mtandao wa PSEA una washiriki kutoka kwenye sekta zote zinazoongoza? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |
| **Kipimo** | **Michakato na Taratibu za Kuwasilisha Malalamiko katika Jamii** | **Shughuli** | **Hali** | **Alama** |
| Swali la 5 | Je, katika muktadha wako, zipo taratibu za wastani za utendaji za Mifumo ya Malalamiko katika Jamii (CBCM)? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |
| Swali la 6 | Kama NDIYO, je, taratibu za wastani za utendaji za Mifumo ya Malalamiko katika Jamii (CBCM) zimesambazwa katika sekta zote? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |
| Swali la 7 | Je, taratibu za wastani za utendaji ziliundwa kwa kuhusisha angalau mhusika mmoja, shirika au mtandao wa haki za wanawake unaofanya kazi katika muktadha wako? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 8 | Je, kuna njia ngapi za kuwasilisha malalamiko na ni zipi hizo (ana kwa ana, maandishi, barua pepe)? | Ukaguzi wa hati/uchunguzi | ☐ _____<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “aina 1 ya njia au zaidi”<br>☐ 0 kwa “njia 0”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 9 | Je, kuna taratibu zilizopo za kushughulikia masuala ya kusema (yaani, kuripoti jambo ambalo linaonekana kuwa tatizo)?<br><br>(Njia zinazofaa kwa jamii katika muktadha wako zinaweza kujumuisha: simu za dharura, masanduku ya malalamiko/mapendekezo, barua pepe, au sehemu za kutoa taarifa ana kwa ana). | Ukaguzi wa hati/ uchunguzi wa upatikanaji wa taratibu hizo katika jamii | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| **Kipimo** | **Upatikanaji wa Taratibu za Kuwasilisha Malalamiko katika Jamii** | **Shughuli** | **Hali** | **Alama** |
| Swali la 10 | Katika muktadha wako, je, kuna Utaratibu jumuishi wa kuwasilisha malalamiko katika Jamii ambao unatumiwa na mashirika yote ya kibinadamu? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 11 | Je, nyenzo za Taratibu za Kuwasilisha malalamiko katika Jamii zinaweza kufikiwa na jamii lengwa? (“Inayoweza kufikiwa” inamaanisha kuwa nyenzo ziko katika lugha inayotumiwa katika jamii na inafaa kwa viwango vya kusoma na kuandika katika jamii; kwamba kuna ufikiaji wa kutosha wa simu za rununu; kwamba picha zinatumiwa katika miktadha ambapo viwango vya kusoma na kuandika ni vya chini, n.k.) | Ukaguzi wa hati/ uchunguzi wa nyenzo katika mazingira | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 12 | Je, maelezo yote kuhusu idhini (pamoja na fomu za idhini) yametolewa katika lugha za wenyeji ambazo watu wengi wanaweza kusoma? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| **Kipimo** | **Maeneo Salama kwa Wanawake na Wasichana** | **Shughuli** | **Hali** | **Alama** |
| Swali la 13 | Katika muktadha wako, je, maeneo salama kwa wanawake na wasichana katika usaidizi wa kibinadamu yana itifaki za usiri za kushughulikia matukio ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |

| Kipimo | Rufaa kwa Jamii | Shughuli | Hali | Alama |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 14 | Katika muktadha wako, je, kuna mfumo unaofanya kazi wa rufaa ulio katika jamii kwa ajili ya wanawake na wasichana ili waweze kupata huduma za kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia (UWAKI) kwa usalama NA kwa wakati ufaao?<br>(Kwa vile usalama na wakati ni muhimu, chagua "HAPANA" ikiwa mojawapo haipo). | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |
| **Kipimo** | **Ukaguzi wa Usalama** | **Shughuli** | **Hali** | **Alama** |
| Swali la 15 | Katika muktadha wako, je, kulikuwa na ukaguzi wa usalama uliofanywa katika wiki mbili zilizopita? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ndiyo"<br>☐ 0 kwa "Hapana"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |
| Swali la 16 | Je, ukaguzi wa usalama unafanywa angalau mara moja kila mwezi au mara nyingi zaidi? | Ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa "Ukaguzi unao-fanywa kila mwezi au mara nyingi zaidi"<br>☐ 0 kwa "chini ya mara moja kwa mwezi au haufanywi"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Sijui" |

## Mazingira ya Usaidizi wa Kibinadamu

| Kipimo | Kuzuia na Kupunguza UWAKI | Shughuli | Hali | Alama |
|---|---|---|---|---|
| | **Maji na Usafi wa Mazingira (WASH)** | | | |
| **Ikiwa unaweza kuzipata, unaweza kukagua picha/ taswira za juu/ ramani zozote zinazopatikana za sehemu husika zilizochapishwa na wahusika wa WASH au wengine ili kusaidia kujibu baadhi ya maswali haya.** | | | | |
| Swali la 17 | Je, maeneo ya kuoga yana makufuli yanayofanya kazi kwa upande wa ndani wa milango? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa "Ndiyo, yote"<br>☐ 0.75 kwa "Ndiyo, mengi"<br>☐ 0.50 kwa "Ndiyo, baadhi"<br>☐ 0 kwa "Hapana, hamna"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Haihusiki" |
| Swali la 18 | Je, maeneo ya vyoo yana makufuli yanayofanya kazi kwa upande wa ndani wa milango? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa "Ndiyo, yote"<br>☐ 0.75 kwa "Ndiyo, mengi"<br>☐ 0.50 kwa "Ndiyo, baadhi"<br>☐ 0 kwa "Hapana, hamna"<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa "Haihusiki" |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 19 | Je, kuna sehemu tofauti za wanaume na wanawake kuoga? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 20 | Je, kuna sehemu tofauti za wanaume na wanawake kwenda haja? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 21 | Je, vyoo viko zaidi ya mita 50 kutoka kwenye makazi/nyumba? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 22 | Je, vituo vya maji viko ndani ya mita 500 kutoka kwa kaya? (Ni muhimu kwa vituo vya maji kuwa karibu na kaya. Hakikisha umezingatia angalau vituo vitatu vya maji na umbali wake hadi kaya)<br>(Hakikisha kwamba Wakusanya Data wanafahamu umbali wa mita 500 ni upi). | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 23 | Je, maeneo ya jikoni vya kutumiwa pamoja yapo ndani ya mita 500 kutoka vituo vya maji? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 24 | Je, pampu za mikono na pampu za maji zinatumiwa na wanawake na zinaweza kutumika kwa urahisi? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 25 | Je, sehemu ya kuteka maji ipo ndani ya eneo lengwa/jamii? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Haihusiki | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 26 | Je, maeneo ya kuogea yana mwangaza wa taa ambazo zimeonekana kufanya kazi ndani NA katika sehemu yote? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 27 | Je, maeneo ya vyoo yana mwangaza wa taa ambazo zimeonekana kufanya kazi ndani NA kuzingira vyoo? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 28 | Je, sehemu za kuogea zimejengwa kwa nyenzo imara (kwa mfano, mbao, chuma, n.k.)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 29 | Je, sehemu za vyoo zimejengwa kwa nyenzo imara (kwa mfano, mbao, chuma, n.k.)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 30 | Je, muda wa wastani wa kusubiri maji ni dakika 30 au chache? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Haihusiki (NA) | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 31 | Je, familia hufulia nguo mahali pengine mbali na nyumba zao? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Haijulikani / Haihusiki | 0 kwa “Ndiyo”<br>1 kwa “Hapana”<br>Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haijulikani/Haihusiki” |
| | **Mkao wa Kambi** | | | **Alama** |
| Swali la 32 | Ni asilimia ngapi ya timu za Uratibu wa Kambi na Usimamizi wa Kambi, wafanyakazi na uongozi ni wanawake? | Ukaguzi wa hati | ☐ 2/3 au zaidi ni wanawake<br>☐ Chini ya 2/3<br>☐ Haihusiki / Sijui | ☐ 1 kwa “zaidi ya 2/3 au 66.66%”<br>☐ 0 kwa “chini ya 2/3 au hakuna”<br>☐ RUKA kwa “Haihusiki” au “Sijui” |
| Swali la 33 | Je, eneo/jamii ina mwangaza wa kutosha wa taa za umma/za binafsi? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hakuna taa<br>☐ Haihusiki | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ RUKA kwa “Haihusiki” |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 34 | Je, kuna jengo la kinga (kwa mfano, uzio, ukuta, n.k.) karibu na eneo kwa ajili ya faragha na heshima? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, lote<br>☐ Ndiyo, mengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki | ☐ 1 kwa “Ndiyo, lote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 35 | Kuna nafasi / njia za kutembea kati ya makazi / nyumba na majengo mengine? (Nafasi inakusudiwa kuhakikisha kuwa kuna faragha na ufikiaji salama katika eneo). | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 36 | Je, makazi/nyumba zina kuta zilizojengwa kwa nyenzo imara (km, mbao, chuma, n.k.)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, zote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki | ☐ 1 kwa “Ndiyo, zote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 37 | Je, makazi/nyumba zina milango salama yenye makufuli? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |
| Swali la 38 | Je, makazi/nyumba zina sehemu za kulala za binafsi (kwa mfano, zilizotengwa kwa kuta, mapazia, n.k.)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, zote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki | ☐ 1 kwa “Ndiyo, zote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Haihusiki” |

| Kipimo | Maeneo salama kwa wanawake na wasichana | Shughuli | Hali | Alama |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 39 | Je, kuna sehemu iliyotengwa ambapo wanawake na wasichana wanaweza kukusanyika ili kujumuika, kujifunza ujuzi mpya na kusaidiana (k.m., kituo cha wanawake, nafasi salama za wanawake na wasichana, n.k.)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana” |
| Swali la 40 | Je, nafasi salama ya wanawake na wasichana ipo karibu au kando na kituo cha polisi, kambi ya kijeshi au eneo la kidini, au mahali pengine ambapo wanaume huwa wanakusanyika? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana” |
| Swali la 41 | Je, nafasi salama kwa wanawake na wasichana ipo umbali wa kutembea usiozidi dakika 10 kutoka sehemu/ jamii ambapo wanawake na wasichana wanaolengwa wanatoka? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana” |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 42 | Je, nafasi salama kwa wanawake na wasichana inafikika kwa urahisi (k.m., njia wazi, mwangaza)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana” |
| Swali la 43 | Je, nafasi salama kwa wanawake na wasichana ina jina la busara lisilo nyeti, lisiloibua unyanyapaa (yaani, hakijaitwa kituo cha UWAKI/ SGBV)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 44 | Je, nafasi hiyo imefanywa kuwa ya faragha (k.m., kupitia uzio, kuta za faragha, n.k.)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna” |
| Swali la 45 | Je, kuna wahudumu wa kike wa usalama katika nafasi hiyo salama wakati wa saa za kazi? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, zote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo, zote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ RUKA kwa “Sijui” |
| Swali la 46 | Je, nafasi hii ni ya wanawake na wasichana pekee? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 47 | Je, huduma na usaidizi wa UWAKI unapatikana saa 24 kwa siku, siku 7 za wiki? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 48 | Ikiwa maeneo ya huduma za kukabili UWAKI hayajafunguliwa saa zote/ siku zote, je, kuna ratiba iliyo dhahiri? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 49 | Je, sehemu hiyo inatoa yoyote kati ya yafuatayo?<br>Usaidizi wa Kisaikolojia (PSS) kwa vikundi au watu binafsi<br>Ushughulikiaji wa visa | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, yote<br>☐ Ndiyo, mingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo, yote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, mingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ RUKA kwa “Haihusiki” / “Sijui” |
| Swali la 50 | Je, nafasi hiyo inatoa shughuli au huduma nyingine zozote (k.m., burudani, kujenga ujuzi, usaidizi wa nyenzo, n.k.)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 51 | Ikiwa kuna shughuli zinazokusudiwa kufanyika siku ya kuangalia, je, wanawake na wasichana wanashiriki katika shughuli hizo? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 52 | Kwa wafanyakazi waliopata mafunzo ya msingi, je, walipata usaidizi wa kuwajengea uwezo baadaye? (Ikiwa unaweza, waulize wafanyakazi waliopo ili ufahamu. Ikiwa sivyo, jibu, “Sijui.”) | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |

| Kipimo | Huduma ya afya | Shughuli | Hali | Alama |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kufukia Mfumo wa Taarifa za Afya katika Wilaya/ Mfumo wa Taarifa za Afya unaopatikana kwa umma katika eneo lako kunaweza kukusaidia kujibu baadhi ya maswali yafuatayo.<br><br>Kwa baadhi ya maswali yaliyo hapa chini, huenda ukahitajika kuwauliza wafanyakazi waliopo. Ikiwa haiwezekani na huwezi kupata jibu, weka alama “Sijui.”** | | | | |
| Swali la 53 | Je, kituo cha afya hufunguliwa saa zote kila siku? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana” |
| Swali la 54 | Je, kituo cha afya kinatoa vidonge vyovyote vya dharura vya kuzuia mimba (pamoja na kinga dhidi ya VVU baada ya tukio linaloweza kuambukiza pamoja na dawa za magonjwa ya zinaa)? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 55 | Je, kituo kina vifaa kamili, vya kisasa vya kinga ya baada ya tukio linaloweza kuambukiza kwa ajili ya huduma kwa waliobakwa? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana (havina)<br>☐ Hapana (vipo lakini vimepitwa na wakati)<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 56 | Je, kituo kina wahudumu wa afya wa kike walio na mafundisho? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 57 | Je, kituo kina itifaki iliyo wazi ya kutoa huduma za kimatibabu na njia ya rufaa kwa walioathiriwa na UWAKI ili wapate huduma za ziada zinazohitajika, ikiwa ni pamoja na msaada wa kisaikolojia/afya ya akili, ulinzi na usalama, sheria, ulinzi wa watoto, n.k.? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |
| Swali la 58 | Je, huduma zozote kati ya zifuatazo zinapatikana?<br>Huduma salama ya kutoa mimba (SAC)<br>Huduma baada ya kutoa mimba (PAC)<br>Huduma ya kina ya utoaji mimba (CAC)<br>Upangaji uzazi | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, huduma ☐ zote zinapatikana kwenye vituo vya afya<br>☐ Ndiyo, huduma nyingi zinapatikana katika vituo vingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna<br>☐ Haihusiki/ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo, zote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ RUKA kwa “Haihusiki” / “Sijui” |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 59 | Je, kituo hicho kina chumba cha mashauriano cha faragha / siri kwa ajili ya kutoa huduma na mashauriano pamoja na ufichuzi? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Haihusiki/ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ RUKA kwa “Haihusiki” / “Sijui” |
| Swali la 60 | Je, kituo cha afya kipo umbali usiozidi saa 1 kwa kutembea kwa wanawake na wasichana katika jamii inayolengwa? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana” |
| Swali la 61 | Je, huduma za afya zinapatikana bure? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana<br>☐ Sijui | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana”<br>☐ Swali LITARUKWA jibu likiwa “Sijui” |

| Kipimo | Wafanyakazi | Shughuli | Hali | Alama |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 62 | Katika miradi ya kukabili UWAKI kwa wanawake na wasichana, je, watoa huduma wote walio mstari wa mbele na wahudumu katika nafasi salama ni wanawake? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, wote<br>☐ Ndiyo, wengi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna | ☐ 1 kwa “Ndiyo, wote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, wengi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna” |

| Kipimo | Huduma za lishe | Shughuli | Hali | Alama |
|---|---|---|---|---|
| Swali la 63 | Je, huduma zinapatikana kwa wanawake wajawazito na wanaonyonyesha ambao wana utapiamlo? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, zote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna | ☐ 1 kwa “Ndiyo, zote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna” |
| Swali la 64 | Ikiwa huduma za lishe ziko kivyake, je, ziko karibu na huduma za afya NA za Maji na Usafi wa Mazingira? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo, zote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna | ☐ 1 kwa “Ndiyo, zote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna”<br>☐ Alama iwe 0 kama huduma za lishe HAZIKO karibu na vituo vya afya na Maji na Usafi wa Mazingira; au zipo karibu na mojawapo tu). |
| Swali la 65 | Je, huduma za lishe ni sehemu ya njia zinazotumiwa kwa rufaa ya UWAKI? | Uchunguzi wa eneo / vvistawishi/ ukaguzi wa hati | ☐ Ndiyo, zote<br>☐ Ndiyo, nyingi<br>☐ Ndiyo, baadhi<br>☐ Hapana, hamna | ☐ 1 kwa “Ndiyo, zote”<br>☐ 0.75 kwa “Ndiyo, nyingi”<br>☐ 0.50 kwa “Ndiyo, baadhi”<br>☐ 0 kwa “Hapana, hamna” |
| Swali la 66 | Je, kuna wafanyakazi wa kike wanaohudumu katika huduma za lishe? | Uchunguzi wa eneo / vistawishi | ☐ Ndiyo<br>☐ Hapana | ☐ 1 kwa “Ndiyo”<br>☐ 0 kwa “Hapana” |

# Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi

## Maandalizi:

**Hakikisha kuwa una nakala za kutosha za utafiti huu kabla hujaanza siku yako ya kukusanya data. Utahitaji nakala moja ya karatasi ya utafiti kwa kila mfanyakazi anayejaza utafiti.**

**Muhimu! Kabla ya kuanza, sisitiza mambo haya kwa anayeshiriki katika utafiti.**

- Utafiti huu ni wa siri.
- Hakuna data inayoweza kukutambulisha itashirikiwa na mwajiri wako au mashirika mengine au watu binafsi.
- Taarifa kuhusu jinsia yako, rika la kiumri na wadhifa pekee ndizo zinazoweza kutumika katika uchanganuzi wa data.
- Ikiwa baadhi ya maswali yanakufanya ujisikie mwenye wasiwasi, tafadhali usiogope kusema na tunaweza kusimamisha utafiti wakati wowote.

**Pia kumbuka yafuatayo unapofanya utafiti huu:**

- Endapo tukio la unyanyasaji wa kingono litafichuliwa, toa taarifa muhimu kuhusu huduma na usaidizi unaopatikana. Kuwa tayari kutoa maelezo ya mawasiliano ya kituo chao cha kushughulikia ripoti, ikiwa kipo. (Hakikisha kuwa una anwani hizo kabla ya kuanza tafiti).
- Taarifa zote zinazohusiana na ufichuzi wa mtu binafsi zinapaswa kuwekwa siri.

## Taarifa za MSINGI

**Je, ukalimani unahitajika? NDIYO LA**

Ikiwa ndiyo, ukalimani kutoka ____________________ (lugha) hadi ____________________(lugha)

**Mwanamke/Mwanamume:**

- ☐ Mfanyakazi wa Kike
- ☐ Mfanyakazi wa Kiume

**Mfanyakazi wa Kitaifa au wa Kimataifa:**

- ☐ Mfanyakazi wa Kitaifa
- ☐ Mfanyakazi wa Kimataifa

**Aina ya Shirika:**

- ☐ Shirika la Umoja wa Mataifa au Walinda Amani
- ☐ NGO ya Kimataifa
- ☐ NGO ya Kitaifa/NGO ya Eneo
- ☐ Asasi ya Kijamii
- ☐ Kikundi au Shirika la Wanawake (kitaifa, eneo, kijamii)
- ☐ Nyingine (kama nyingine, tafadhali jaza hapa)________________________________________

**Urefu wa Muda wa Kufanya Kazi Nchini katika Usaidizi wa Kibinadamu:**

- ☐ Chini ya miezi 6
- ☐ Kati ya miezi 6 na mwaka 1
- ☐ Kati ya mwaka 1 na 2
- ☐ Kati ya miaka 2 na 5
- ☐ Zaidi ya miaka 5

**Sekta:**

- ☐ Maji na Usafi wa Mazingira (WASH)
- ☐ (Uratibu wa Kambi na Usimamizi wa Kambi (CCCM)
- ☐ Lishe
- ☐ Ulinzi
- ☐ Ukatili wa Kijinsia
- ☐ Ulinzi wa Watoto
- ☐ Usambazaji wa Bidhaa Zisizo Chakula (NFI)
- ☐ Nyingine (kama nyingine, tafadhali jaza sekta)______________________________

**Cheo cha Sasa Kazini:**

- ☐ Uongozi wa Kibinadamu
- ☐ Usimamizi/Meneja
- ☐ Mratibu
- ☐ Msaidizi
- ☐ Kujitolea
- ☐ Nyingine (kama nyingine, tafadhali jaza hapa)_______________________________

**Umri (chagua moja):**

- ☐ Chini ya miaka 19
- ☐ Miaka 20-24
- ☐ Miaka 25-30
- ☐ Miaka 31-35
- ☐ Miaka 36-45
- ☐ Zaidi ya miaka 45

## Ufafanuzi wa unyanyasaji wa kingono na udhalilishaji na dhuluma ya kingono

**Eleza fasili hizi mbili kwa mhojiwa kabla ya kuanza utafiti naye ili uhakikishe kuwa fasili zinaeleweka na kuchukuliwa kuwa tofauti na aina nyingine za ukatili wa kijinsia (UWAKI).**

**Unyanyasaji wa kingono (SH)** na **udhalilishaji na dhuluma ya kingono (SEA)** zimefafanuliwa mwanzoni mwa uchunguzi. Pia tutatumia fasili hizi na vifupisho kwa muda uliosalia wa utafiti.

| | |
|---|---|
| **Unyanyasaji wa Kingono** | Kwa madhumuni ya utafiti huu, neno unyanyasaji wa kingono linachukuliwa kutokea ndani ya mashirika kutoka kwa mfanyakazi mmoja hadi kwa mwingine: Unyanyasaji wa kingono unajumuisha aina yoyote ya unyanyasaji wa kingono au mgusano wa kingono bila ridhaa ambao hauleti au kujumuisha kujamiiana. Mifano ni pamoja na jaribio la ubakaji, pamoja na kubusu kusikotakikana, kupapasana, au kushika sehemu nyeti na makalio.<br><br>Aina hii ya tukio haijumuishi ubakaji (yaani, pale ambapo mtu ameingiliwa kwa nguvu). Dhuluma ya kijinsia haitashughulikiwa katika utafiti huu. |
| **Udhalilishaji na Dhuluma ya Kingono** | Kwa madhumuni ya utafiti huu, tunatumia ufafanuzi ufuatao kutoka katika Taarifa Rasmi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ya 2003 kuhusu ulinzi dhidi ya udhalilishaji na dhuluma ya kingono:<br><br>"Neno 'udhalilishaji wa kingono' linamaanisha matumizi yoyote halisi au jaribio la kutumia vibaya nafasi ya udhaifu, utofauti wa uwezo, au uaminifu, kwa madhumuni ya ngono, ikijumuisha, lakini si tu, kufaidika kifedha, kijamii au kisiasa kutokana na kumtumia mtu mwingine kingono.29"<br><br>"Neno 'dhuluma ya kingono' linamaanisha tukio halisi au tishio la kimwili la kingono, iwe kwa nguvu au katika hali zisizo na usawa au za kulazimishwa."30 Katika utafiti huu wote, tutarejelea udhalilishaji na dhuluma ya kingono kama mada moja. |

29 Taarifa Rasmi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu ulinzi dhidi ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono (PSEA) (ST/SGB/2003/13)
30 Kama hapo juu

## Anza Utafiti

Tunakuomba ujibu maswali yaliyo hapa chini kuhusu shirika ambako umeajiriwa kwa sasa. Hutaulizwa kutoa maelezo yoyote yanayokutambulisha wewe au shirika lako. Tafadhali jaribu kujibu kila swali katika utafiti na ujaze majibu yako waziwazi kwenye karatasi ili data iweze kuingizwa kwa usahihi katika mfumo wa kukusanya data. Ikiwa kuna maswali yoyote ambayo hutaki kujibu kwa sababu yoyote, tafadhali yaache wazi. Asante kwa muda wako na kwa kushiriki majibu yako.

### Weka Mviringo Kwenye Jibu Unalochagua Kwa Kila Swali

### Kujitolea na Uwajibikaji

1. Kwa kipimo cha 1 (Ni muhimu sana) hadi 5 (Si muhimu hata kidogo), suala la unyanyasaji wa kingono lina umuhimu kiasi gani katika shirika lako?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Ni muhimu sana** | **2. Ni muhimu kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Si muhimu sana** | **5. Si muhimu hata kidogo** |

2. Kwa kipimo cha 1 (Ni muhimu sana) hadi 5 (Si muhimu hata kidogo), suala la udhalilishaji na dhuluma ya kingono lina umuhimu kiasi gani katika shirika lako?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Ni muhimu sana** | **2. Ni muhimu kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Si muhimu sana** | **5. Si muhimu hata kidogo** |

3. Ikiwa mtu fulani atashtakiwa au atatekeleza tendo la unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, shirika langu litachukua wajibu wa kuhakikisha kuwa mwathiriwa/manusura aliyeripoti tukio hilo amelindwa.
   a) Ndiyo
   b) Hapana
   c) Singependa kujibu (NA)

4. Ikiwa mtu fulani atashtakiwa au atatekeleza tendo a unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, shirika langu litachukua wajibu wa kuhakikisha kuwa mtu huyo amewajibikia kitendo hicho.
   a) Ndiyo
   b) Hapana
   c) Singependa kujibu (NA)

**Utaratibu wa Kuwasilisha Malalamiko: Urahisi, Usiri na Hatari**

5. Kwa kipimo cha 1 (ninahimizwa sana) hadi 5 (sihimizwi hata kidogo), shirika lako limekuhimiza kwa kiasi gani kuripoti madai ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, iwapo yatatokea na wakati yanatokea?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Ninahimizwa sana** | **2. Ninahimizwa kiasi** | **3. Sina maoni yoy-ote** | **4. Sihimizwi sana** | **5. Sihimizwi hata kidogo** |

6. Kwa kipimo cha 1 (nina imani sana) hadi 5 (sina imani hata kidogo), una imani kwa kiasi gani kuwa taratibu za kuripoti visa vya unyanyasaji wa kingono katika shirika lako zinaweza kuwa na matokeo ya haki?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Nina imani sana** | **2. Nina imani kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Sina imani sana** | **5. Sina imani hata kidogo** |

7. Kwa kipimo cha 1 (nina imani sana) hadi 5 (sina imani hata kidogo), iwapo utaripoti kisa cha unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, una imani kwa kiasi gani kuwa malalamiko yako yatasalia siri?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Nina imani sana** | **2. Nina imani kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Sina imani sana** | **5. Sina imani hata kidogo** |

8. Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), utakuwa na wasiwasi kiasi gani kujumuisha jina lako iwapo utawasilisha malalamiko kuhusu unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Sina wasiwasi wowote** | **2. Sina wasiwasi sana** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nina wasiwasi kiasi** | **5. Nina wasiwasi sana** |

9. Je, ushawahi kuwasilisha malalamiko rasmi kuhusu unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?
   a) Ndiyo
   b) Hapana (Ruka hadi swali la 11)

10. Ikiwa jibu lako la swali ya 9 ni Ndiyo, kwa kipimo cha 1 (niliridhika kabisa) hadi 5 (sikuridhika hata kidogo), uliridhika kwa kiasi gani na jinsi shirika lilivyoshughulikia malalamiko yako?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Niliridhika kabisa** | **2. Niliridhika kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Sikuridhika sana** | **5. Sikuridhika hata kidogo** |

11. Je, ushawahi kuwa shahidi katika malalamiko rasmi ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?
   a) Ndiyo
   b) Hapana

12. Je, wewe au mfanyakazi mwenzako mshawahi kutuma malalamiko yasiyo rasmi kuhusu unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono? (Yasiyo rasmi inamaanisha kupitia njia nyingine kando na zile zilizobainishwa kama rasmi)
   a) Ndiyo
   b) Hapana (Ruka hadi swali la 14)

13. Ikiwa jibu lako la swali la 12 ni Ndiyo, kwa kipimo cha 1 (nilihimizwa sana) hadi 5 (sikuhimizwa hata kidogo), shirika lako lilikuhimiza kwa kiasi gani uwasilishe malalamiko rasmi?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Nilihimizwa sana** | **2. Nilihimizwa kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Sikuhimizwa sana** | **5. Sikuhimizwa hata kidogo** |

14. Kwa kipimo cha 1 (inawezekana sana) hadi 5 (haiwezekani hata kidogo), kwa maoni yako inawezekana kwa kiasi gani kwa mtu kufutwa kazi ikiwa malalamiko ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono yatawasilishwa dhidi yake?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Inawezekana sana** | **2. Inawezekana kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Haiwezekani sana** | **5. Haiwezekani hata kidogo** |

15. Kwa kipimo cha 1 (unaweza kuathiri sana) hadi 5 (hauwezi kuathiri hata kidogo), uwezekano wa unyanyapaa ndani ya shirika lako unaweza kuathiri kwa kiasi gani uamuzi wako wa kuripoti (au kutoripoti) kisa cha unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Unaweza kuathiri sana** | **2. Unaweza kuathiri kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Hauwezi kuathiri sana** | **5. Hauwezi kuathiri hata kidogo** |

16. Kwa kipimo cha 1 (unaweza kuathiri sana na siwezi kuripoti) hadi 5 (hauwezi kuathiri hata kidogo na ninaweza kuripoti), uwezekano wa ulipizaji kisasi ndani ya shirika lako unaweza kuathiri kwa kiasi gani uamuzi wako wa kuripoti (au kutoripoti) kisa cha unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Unaweza kuathiri sana na siwezi kuripoti** | **2. Unaweza kuathiri kiasi na sina uhakika ninaweza kuripoti** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Hauwezi kuathiri na labda ninaweza kuripoti** | **5. Hauwezi kuathiri hata kidogo na ninaweza kuripoti** |

17. Kulingana na uliyoona, kwa kipimo cha 1 (wamechukua hatua) hadi 5 (wameficha kimakusudi), usimamizi wa shirika lako umeshughulikia vipi uvumi wa kuwepo kwa unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono? Ikiwa HUJUI jibu, RUKA hadi swali la 18.

| 1. Mipango yenye utaratibu imewekwa | 2. Mipango fulani imewekwa, lakini kulingana na tukio | 3. Sina maoni yoyote | 4. Hakuna hatua zinazochukuliwa | 5. Kumekuwa na juhudi za kimakusudi za kuficha tukio |
|---|---|---|---|---|

18. Je, unahisi kuwa una mwongozo wa kutosha kuhusu taratibu na njia za kuripoti madai ya unyanyasaji au dhuluma ya kingono?

    a) Ndiyo

    b) Hapana

    c) Sijui

19. Je, shirika lako lina sera zozote za kuwalinda wapiga ripoti? *(Mpiga ripoti: sera ya kuwalinda watu, wakiwemo wafanyakazi, ambao wataripoti visa vya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono dhidi ya kisasi)*

    Ndiyo, zipo na ninazifahamu

    Hapana, sijui kama zipo (Ruka hadi swali la 21)

20. Ikiwa jibu lako la swali la 19 ni NDIYO, kwa kipimo cha 1 (nimelindwa sana) hadi 5 (sijalindwa hata kidogo), unajihisi kwa kiasi gani kuwa umelindwa na sera za shirika lako za wapiga ripoti, ikiwa utaripoti madai ya kunyanyaswa au kudhulumiwa kingono?

| 1. Nimelindwa sana | 2. Nimelindwa kiasi | 3. Sina maoni yoyote | 4. Sijalindwa sana | 5. Sijalindwa hata kidogo |
|---|---|---|---|---|

**Hatua Zinazochukuliwa na Shirika**

21. Je, unajua mwathiriwa/manusura yeyote wa unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono ambaye alipata huduma za kushughulikia ukatili wa kijinsia kama vile ushauri nasaha au matibabu?

    a) Ndiyo, walipewa huduma hizi

    b) Hapana, hawakupewa huduma hizi (Ruka hadi swali la 24)

    c) Sijui/sina uhakika (Ruka hadi swali la 24)

22. Ikiwa jibu lako la swali la 21 ni NDIYO, mwathiriwa/manusura alipewa huduma hizo za kushughulikia ukatili wa kijinsia papo hapo (kama sehemu ya mazungumzo ya kufichua)?

    a) Ndiyo

    b) Hapana

    c) Sijui/sina uhakika

23. Ikiwa jibu lako la swali la 21 ni NDIYO, je, mwathiriwa/manusura wa unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono alisaidiwa katika kujifanyia uamuzi kuhusu huduma na usaidizi aliouhitaji?

    a) Ndiyo

    b) Hapana

    c) Sijui/sina uhakika

## Kushirikishwa kwa Wanawake katika Kutunga na Kutekeleza Sera

24. Kwa maoni yako, kwa kipimo cha 1 (hushughulikiwa sana) hadi 5 (hayashughulikiwi kamwe), masuala ya usalama na ulinzi wa wanawake yanashughulikiwa kwa kiasi gani na sera na desturi za usalama na ulinzi zilizopo katika shirika lako? Ikiwa HUJUI jibu lake, RUKA hadi swali ya 25.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Hushughulikiwa sana** | **2. Hushughulikiwa kiasi, japo kuna sehemu zinazohitaji kuboreshwa** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Hayashughulikiwi sana; kuna mapengo mengi** | **5. Hayashughulikiwi kamwe** |

25. Kwa maoni yako, kwa kipimo cha 1 (hushughulikiwa sana) hadi 5 (hayashughulikiwi kamwe), kukija ni masuala ya usalama na ulinzi, ni kwa kiasi gani ukweli na hali wanazopitia wanawake huzingatiwa katika sera na desturi zilizopo katika shirika lako? Ikiwa HUJUI jibu lake, RUKA hadi swali ya 26.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Hushughuliki-wa sana** | **2. Hushughulikiwa kiasi, japo kuna sehemu zinazohitaji kuboresh-wa** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Hayashughulik-iwi sana; kuna mapengo mengi** | **5. Hayashughu-likiwi kamwe** |

26. Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), ni mara ngapi ambazo viongozi/wasimamizi/walinda usalama hukuuliza maoni yako kuhusu mahitaji ya usalama na ulinzi ya wafanyakazi wa kike?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Kila wakati** | **2. Mara kwa mara** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nadra** | **5. Kamwe** |

27. Je, usimamizi wa shirika lako ushawahi kukuuliza maoni yako kuhusu wasiwasi wa wanawake kuhusu ulinzi wakati wanasafiri au kutembea, wakati wa kubuni sera za kutembea na kusafiri?

a) Ndiyo

b) Hapana

28. Je, usimamizi wa shirika lako ushawahi kukuuliza maoni yako kuhusu wasiwasi na mahitaji ya wanawake wakati wa kubuni sera za malazi?

a) Ndiyo

b) Hapana

29. Je, usimamizi wa shirika lako ushawahi kukuuliza maoni yako kuhusu wasiwasi wowote wanawake walio nao kuhusiana na ulinzi na faragha wakati wa kubuni sera za ofisini?

a) Ndiyo

b) Hapana

30. Ikiwa umejibu NDIYO katika mojawapo ya maswali kati ya swali la 27 hadi la 29, je, kuna yoyote kati ya maoni au mapendekezo ambayo umetoa ambayo yamejumuishwa katika desturi na sera za usalama na ulinzi? Ikiwa HUKUJIBU NDIYO katika mojawapo ya maswali hayo, RUKA hadi swali la 31.

a) Ndiyo

b) Hapana

### Utambuzi wa Hatari

31. Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), unahisi kwa kiasi gani kuwa shirika lako linachukua hatua za kushughulikia usalama na ulinzi wa wafanyakazi wenzako wa kike?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Kila wakati** | **2. Mara kwa mara** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nadra** | **5. Kamwe** |

32. Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), unahisi kwa kiasi gani kuwa shirika lako linaweka wafanyakazi wenzako wa kike katika hatari yoyote ya kunyanyaswa kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Kila wakati** | **2. Mara kwa mara** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nadra** | **5. Kamwe** |

33. Kwa kipimo cha 1 (kila wakati) hadi 5 (kamwe), unahisi kwa kiasi gani kuwa shirika lako linazuia au kupunguza hatari za wanawake wanaonufaika na kazi yenu kunyanyaswa, kudhalilishwa na kudhulumiwa kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Kila wakati** | **2. Mara kwa mara** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nadra** | **5. Kamwe** |

34. Je, ushawahi kujihisi mwenye woga au unatishwa na wafanyakazi wanaolinda usalama?

a) Ndiyo

b) Hapana

35. Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), una wasiwasi kiasi gani kuhusu uchunguzi wa kuthibitisha ambao shirika lako linafanyia wafanyakazi wanaolinda usalama? Uwapo HUNA HABARI kuhusu uchunguzi wowote wa kuthibitisha, RUKA hadi swali la 36.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Sina wasiwasi wowote** | **2. Sina wasiwasi sana** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nina wasiwasi kiasi** | **5. Nina wasiwasi sana** |

36. Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), una wasiwasi wowote kuhusu uchunguzi wa kuthibitisha ambao shirika lako linafanyia madereva na wafanyakazi wengine? Uwapo HUNA HABARI kuhusu uchunguzi wowote wa kuthibitisha, tafadhali chagua NA.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Sina wasiwasi wowote** | **2. Sina wasiwasi sana** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nina wasiwasi kiasi** | **5. Nina wasiwasi sana** |

**Ikiwa anayehojiwa ni mwanamume, utatamatishia maswali hapa.**

37. Je, shirika lako hukupatia mbinu ya usafiri kama sehemu ya kazi yako?

a) Ndiyo

b) Hapana (Ruka hadi swali la 39)

38. Ikiwa umejibu NDIYO katika Swali la 37, kwa kipimo cha 1 (nina wasiwasi sana) hadi 5 (sina wasiwasi wowote), una wasiwasi kiasi gani kuhusu uwezekano wa kunyanyaswa kingono unapotumia mbinu ya usafiri uliyopewa na shirika lako? (Ruka hadi Swali la 40)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Nina wasiwasi sana** | **2. Nina wasiwasi kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Sina wasiwasi sana** | **5. Sina wasiwasi wowote** |

39. Ikiwa umejibu HAPANA katika Swali la 37, iwapo utahitaji shirika lako likupatie mbinu ya usafiri ili ujihisi salama zaidi, unaonelea kama watakupatia ikiwa utawaomba?

a) Ndiyo

b) Hapana

40. Kwa kipimo cha 1 (sina wasiwasi wowote) hadi 5 (nina wasiwasi sana), una wasiwasi wowote wa kusafiri na wafanyakazi wenza wa kiume? Ikiwa HUSAFIRI na wafanyakazi wenza wa kiume, RUKA hasi swali la 41.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Sina wasiwasi wowote** | **2. Sina wasiwasi sana** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Nina wasiwasi kiasi** | **5. Nina wasiwasi sana** |

41. Kwa kipimo cha 1 (nina uhakika kabisa) hadi 5 (sina uhakika hata kidogo), iwapo utahitaji kuomba aina fulani ya malazi (k.m., hoteli au malazi tofauti) ili kupunguza hatari ya kunyanyaswa au kudhulumiwa kingono, una uhakika kiasi gani kuwa shirika lako litakubali ombi lako? Ikiwa hutumii au HUHITAJI malazi kama sehemu ya kazi yako, RUKA hasi swali la 42.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Nina uhakika kabisa** | **2. Nina uhakika kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Sina uhakika sana** | **5. Sina uhakika hata kidogo** |

42. Kwa kipimo cha 1 (salama kabisa) hadi 5 (siko salama hata kidogo), uhajihisi salama kwa kiasi gani ukiwa mahali unapofanyia kazi (ofisini, eneo la kazini, katika jengo) kukija ni suala la kunyanyaswa, kudhalilishwa na kudhulumiwa kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Salama kabisa** | **2. Salama kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Siko salama sana** | **5. Siko salama hata kidogo** |

43. Kwa kipimo cha 1 (salama kabisa) hadi 5 (siko salama hata kidogo), uhajihisi salama kwa kiasi gani unapotembea katika eneo la dharura kukija ni suala la kunyanyaswa kingono?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1. Salama kabisa** | **2. Salama kiasi** | **3. Sina maoni yoyote** | **4. Siko salama sana** | **5. Siko salama hata kidogo** |

# Zana ya Washiriki ya Kutoa Maoni

## Utangulizi

Asante kwa kushiriki katika utafiti wa Barometa wa Sikiliza!.

Tungependa kupata maoni yako kuhusu ushiriki wako ili kutusaidia tuelewe ni nini kinachoendelea vizuri na kile tunachohitaji kuboresha kwa wakati ujao. Huhitaji kufichua utambulisho wako wakati wa kujibu maswali. Mapendekezo yako yatatusaidia kurekebisha na kusasisha utafiti wa Barometa.

### 1. Maelezo ya jumla

| | |
|---|---|
| **Mimi ni:**<br>☐ Mwanajamii<br>☐ Mtoa huduma<br>☐ Mfanyakazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa au shirika la kimataifa lisilo la kiserikali<br>☐ Mfanyakazi wa shirika lisilo la kiserikali katika eneo<br>☐ husika au la kitaifa<br>☐ Mfanyakazi wa kikundi, mtandao au shirika la wanawake la eneo husika au la kitaifa | **Kwa wafanyakazi/watoa huduma, unafanya kazi katika sekta gani:**<br>☐ UWAKI/VAWG<br>☐ Ulinzi wa watoto<br>☐ Ulinzi<br>☐ Afya<br>☐ Maji, Usafi wa Mazingira (WASH)<br>☐ Bidhaa Zisizo Chakula (NFI)<br>☐ Usalama wa chakula na lishe<br>☐ Makazi<br>☐ Uratibu<br>☐ Nyingine (ikiwa ni nyingine, tafadhali itaje): |
| **Jinsia**:<br>☐ Kike<br>☐ Kiume | **Shughuli uliyoshiriki:**<br>☐ Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FGD)<br>☐ Mahojiano ya Watoa Taarifa Muhimu (KII)<br>☐ Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi<br>☐ Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia |

### 2. Kuelewa

**2.1 Je, ulielezewa vizuri kuhusu Barometa na lengo lake?**

☐ Ndiyo

☐ Hapana

**2.2 Kwa mizani ya 1 (sikuelewa hata kidogo) hadi 5 (nilielewa kabisa), unahisi ulielewa kwa kiwango kipi shughuli uliyoshiriki [futa kama inavyohitajika: FGD/ KII/ Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi/ Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia] na sababu za kufanya shughuli huyo?**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

Unaweza kutuambia mengi zaidi kuhusu hili?

### 3. Hali uliyopitia

**3.1 Je, maswali yalikufaa wewe na hali/ukweli/mambo ambayo umepitia?**

☐ Ndiyo

☐ Hapana

Unaweza kutuambia mengi zaidi kuhusu hili?

Je, kulikuwa na kitu kingine chochote ambacho unadhani tulipaswa kukuuliza? Au ambacho hatukupaswa kukuuliza?

**3.2 Je, maswali yalikuwa muhimu na yenye manufaa kwako?**

☐ Ndiyo

☐ Hapana

Unaweza kutuambia mengi zaidi kuhusu hili?

Je, kulikuwa na kitu kingine chochote ambacho unadhani tulipaswa kukuuliza? Au ambacho hatukupaswa kukuuliza?

**3.3 Je, ilikuwa rahisi kwa kiasi gani kwako kushiriki katika shughuli hii?**

☐ Rahisi sana

☐ Rahisi

☐ Haikuwa rahisi hata kidogo

Unaweza kutuambia mengi zaidi kuhusu hili?

**3.4 Ni nini ulichofurahia zaidi katika shughuli hii?**

**3.5 Ni nini ambacho hukufurahia katika shughuli hii?**

### 4. Wakati ujao

**Ili kutusaidia kuboresha mchakato na shughuli, tungependa kusikia maoni yako kuhusu jinsi tunavyoweza kufanya vyema zaidi wakati ujao.**

**4.1 Je, unafikiri tunaweza kufanya shughuli hii ya [FGD/KII/Utafiti wa Maoni ya Wafanyakazi/Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia] kwa njia tofauti?**

☐ Ndiyo

☐ Hapana

☐ Sina hakika

Unaweza kutuambia mengi zaidi kuhusu hili?

**4.2 Je, tunawezaje kushirikiana na [wanajamii/wafanyakazi/watoa huduma] wakati ujao?**

**4.3 Je, kuna mada au suala lolote ambalo halikujumuishwa kwenye shughuli au kipimo cha Barometa ambalo unaamini linafaa kujumuishwa?**

**4.4 Je, kuna kitu chochote ulichohitaji au kutaka kutoka kwetu wakati wa kushiriki ambacho hukupata?**

**4.5 Je, una maoni, mawazo au chochote cha ziada ambacho ungependa kutuambia?**

**Asante kwa kuchukua muda kushiriki maoni yako nasi.**

# Karatasi ya Taarifa kwa Mshiriki wa Barometa na Idhini

## Karatasi ya Taarifa kwa Mshiriki wa Barometa ya Sikiliza!

**[inafaa kujazwa na timu ya Barometa]**

**Barometa ya Sikiliza!: Kupima jinsi wanawake na wasichana walioathiriwa na majanga na wanawake wanaofanya kazi katika dharura wanafikia uwezo wao, bila unyanyasaji na ukosefu wa usawa**

**Mashirika yanayotoa mwaliko:** [jina la shirika lako/jina la mshirika]

**Mratibu na maelezo ya mawasiliano:** [jina la mratibu kutoka kwa shirika lako na maelezo yake ya mawasiliano]

**Tarehe:** [tarehe]

**Mpendwa mshiriki mtarajiwa,**

Tungependa kukualika kushiriki katika tathmini ya haraka ya hali ya sasa ya utoaji usaidizi wa dharura katika muktadha wa kibinadamu huko [nchi/eneo/dharura]. Tunakualika ukamilishe Utafiti wa Maoni ya Wafanyakazi ambao lengo lake ni kukusanya data kulingana na hali halisi ambazo wafanyakazi wa kike wanaokabiliana na majanga ya kibinadamu wamepitia. Utafiti huu ni dodoso la kina linalotumiwa kukusanya taarifa kuhusu kama wafanyakazi wa kike wanajihisi salama na kuwa wana usaidizi wa kutosha; kiwango cha umakini wa shirika katika masuala kama vile unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono; na jinsi usaidizi wa kibinadamu ulivyoandaliwa kushughulikia changamoto hizo na kupatia kipaumbele mahitaji ya wafanyakazi wa kike, wanawake na wasichana wanaosaidiwa. Tunalenga kufanya uchunguzi huu katika muda wa wiki mbili zijazo kuanzia [tarehe].

Kabla ya kuamua kama utashiriki au hutashiriki, tungependa kukupa maelezo kuhusu sababu za kufanya tathmini hii ya haraka na itahusisha nini. Tafadhali chukua muda kusoma habari ifuatayo kwa makini na uijadili na wafanyakazi wenzako, marafiki na jamaa kama utakavyo. Tafadhali wasiliana nasi (maelezo yako hapo juu), ikiwa kuna jambo lolote lisiloeleweka, au ikiwa ungependa maelezo zaidi.

Ukiamua kuwa ungependa kushiriki katika utafiti huu, unaweza kufanya utafiti mtandaoni bila kukutambulisha [kiungo kimetolewa kwenye barua pepe au mwishoni mwa laha hili—au kama hutaandaa utafiti mtandaoni, basi ondoa chaguo hili kwenye laha] au upange mkutano wa ana kwa ana na mmoja wa wanawake katika timu yetu ya wanaokusanya data ambaye atakamilisha utafiti huu na wewe (tafadhali angalia maelezo yetu ya mawasiliano hapo juu). Nakala ya utafiti imejumuishwa pamoja na laha hili ili uikague na uikamilishwe ana kwa ana ikiwa utaamua chaguo hilo.

***Usiri na kutotambulishwa***

Usiri wako na kutotambulishwa vimepewa kipaumbele na ni muhimu sana kwetu katika tathmini hii ya haraka. Utafiti huu hautakutambulisha hata kidogo. Hakuna maelezo ya kibinafsi yatakayokusanywa, na hakuna mtu atakayeulizwa kutoa taarifa mahususi kuhusu shirika alimo. Taarifa zote zitakazokusanywa na kutumika

hazitamtambulisha aliyezitoa. Hakuna data inayoweza kukutambulisha itashirikiwa na mwajiri wako au vyanzo vingine. Ukiamua kufanya utafiti huu ana kwa ana na mmoja wa wanatimu yetu, wao na sisi tunatii kanuni za usiri.

Taarifa kuhusu jinsia, umri na wadhifa wako pekee ndizo zinazoweza kutumika katika uchanganuzi wa data.

### *Kushiriki kwa Hiari*

Kushiriki katika utafiti huu ni kwa hiari kabisa. Ni juu yako kuamua kushiriki au kutoshiriki. Ukiamua kushiriki, bado uko huru kujiondoa wakati wowote bila kutoa sababu, ingawa unapaswa kujihisi huru kutoa sababu ili utafiti wa baadaye uweze kuboreshwa. Ukiamua kushiriki, unaweza kuchagua kutojibu maswali yoyote ambayo haujihisi huru kujibu. Hakutakuwa na athari zozote mbaya za kutoshiriki katika utafiti au kujiondoa kwenye utafiti mapema. Muhimu vile vile, hakutakuwa na fidia au manufaa ya ziada kwa washiriki kwa kushiriki katika utafiti.

### *Ni hasara na hatari zipi zinazoweza kutokana na kushiriki?*

Kushiriki katika utafiti huu kutahitaji kujitolea muda: kukamilisha utafiti mtandaoni kutachukua dakika 10-25; au kuandaa kikao wa kufanya utafiti ana kwa ana, shughuli ambayo inaweza kukuhitaji usafiri ili ukutane na mshiriki wa timu ya Sikiliza ambaye atafanya utafiti. Ingawa utafiti hauwaulizi washiriki kufichua hali walizopitia wao binafsi, baadhi ya maswali katika utafiti yanagusia masuala ambayo unaweza kuyaona nyeti au ya kibinafsi. Baadhi ya maswali yatauliza kuhusu mitazamo yako kuhusu mazingira ya kazi na usaidizi wa kibinadamu kukija ni masuala ya unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono, na ukatili wa kijinsia. Ukiamua kushiriki na uathiriwe na masuala au maswali yoyote, tumejumuisha maelezo ya mahali unapoweza kupata usaidizi [maelezo ya simu za dharura za usaidizi; maeneo ya huduma; watu wa kuwasiliana nao na mashirika yao]. Unaweza pia kuwasiliana nasi moja kwa moja (tazama maelezo ya mawasiliano hapo juu) ikiwa ungependa kuzungumza nasi badala yake.

### *Je, kushiriki kunaweza kuwa na faida gani?*

Kushiriki katika utafiti kutatupatia taarifa muhimu na mtazamo wa pamoja, kutoka kwa sampuli ya kikundi cha wafanyakazi wa kike na wa kiume juu ya ahadi za kitaasisi; ufanisi wa taratibu za kuwasilisha malalamiko; na viwango vinavyotambulika vya hatari, usalama na uchukuaji hatua kuhusiana na unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kijinsia. Tutatumia matokeo haya, pamoja na tathmini nzima ya haraka, kuchochea wadau wakuu na wafanya maamuzi waboreshe harakati ya utoaji usaidizi katika muktadha wa kibinadamu kwa ajili ya wanawake na wasichana, na wafanyakazi wa kike wanaotoa misaada.

### *Utafiti wa Barometa ni sehemu ya mradi mkubwa zaidi wa Sikiliza!.*

Sikiliza! ni mradi ulioanzishwa na shirika la IRC ili kukuza sauti na uwezo wa wanawake na wasichana wakimbizi ili kuchochea mageuzi ya kitaasisi, hatua za mashirika, na kuongeza rasilimali ili kupunguza na kukabiliana na unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kijinsia katika mazingira ya kibinadamu. Kiini cha mradi huu sio tu kunasa sauti za wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na wanawake wanaofanya kazi katika dharura—ila ni kusikiliza na kushughulikia mahitaji na hali zao. Wazo hili linakusudiwa kujumuishwa katika kazi zote tunazofanya kupitia mradi wa Sikiliza!.

Sikiliza! ni mradi wa miaka mitatu (2019-2021) unaotekelezwa na shirika la IRC na washirika wengine wanaofanya kazi kwa pamoja na kikundi cha ushauri cha wahusika wa haki za wanawake, kwa lengo la jumla la kukuza sauti na uwezo wa wanawake na wasichana wakimbizi ili kuchochea mageuzi ya kitaasisi, hatua za mashirika, na kuongeza rasilimali ili kupunguza unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya kingono katika mazingira ya kibinadamu. Malengo ya mradi ni:

(a) Kuanzisha utafiti wa Barometa ya Sikiliza! ambao hupima hatua za kushughulikia ukatili wa kijinsia (UWAKI) na uchukuaji hatua na uzuiaji wa udhalilishaji na dhuluma ya kingono katika miktadha ya kibinadamu;

(b) Kuunda kielelezo cha kubadilisha utamaduni wa shirika ili kukuza usawa wa kijinsia na kutovumilia kabisa udhalilishaji wa kingono na kuzuia dhuluma ndani ya mashirika ya kibinadamu; na

(c) Kusaidia mashirika ya haki za wanawake kuongoza marekebisho na uboreshaji wa taratibu za kuzuia, kuripoti, kuchunguza na kushughulikia visa vya udhalilishaji na dhuluma ya kijinsia kwa kuzingatia sauti na maoni ya wanawake na wasichana.

Utafiti huu ni sehemu ya Lengo la 1. Maelezo zaidi kuhusu mradi wa Sikiliza yanaweza kupatikana kwenye [https://gbvresponders.org/womens-movement-building/listen-up/]

***Kuhusu Barometa - tathmini ya haraka ya usaidizi wa kibinadamu katika visa vya ukatili wa kijinsia na kuzuia unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono.***

Barometa **ya Sikiliza!**, sehemu ya mradi mpana wa Sikiliza!, ni zana ya kupanga na kutathmini ambayo inachunguza hali walizopitia wanawake na wasichana ili kubainisha kama mazingira ya usaidizi katika dharura za kibinadamu yanaweza kuzuia, kupunguza na kukabiliana na UWAKI, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono. Utafiti wa Barometa hutathmini mazingira wala si mashirika. Utafiti huu umebuniwa ili kufanya tathmini ya haraka ya uwezo na udhaifu wa usaidizi wa kibinadamu kwa ajili ya wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na wale wanaofanya kazi katika mazingira ya dharura za kibinadamu na wale walio katika eneo chanzo ambako msaada wa dharura unapelekwa, kwa madhumuni ya kuandaa mapendekezo ya kutumika katika utetezi. Utafiti huu unatumia zana na shughuli nne za kukusanya data: Mwongozo wa Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FDG); Mwongozo wa Mahojiano na Watoa Taarifa Muhimu (KII); Utafiti wa Kuchunguza kwa Kuangalia; na Utafiti wa Mtazamo wa Wafanyakazi. Kwa umahususi, utafiti wa Barometa unaweza kutumiwa kama zana ya utetezi na vikundi, mashirika na mitandao ya wanawake pamoja na wahusika wengine wanaokabiliana na UWAKI ili kuwawajibisha wale wanaohusika katika utoaji usaidizi wa kibinadamu kwa wanawake na wasichana.

Kipimo cha Barometa kilibuniwa na kurekebishwa na wataalamu wanaoshughulikia masuala ya UWAKI, usawa wa kijinsia, unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma za kingono na wanaohusika katika utoaji usaidizi katika dharura, kwa kuzingatia Nadharia ya Mabadiliko iliyobuniwa na wanaharakati wa haki za wanawake kutoka maeneo ya Kusini mwa Dunia kwa ushirikiano na Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (IRC). Mashirika matatu ya haki za wanawake na timu tatu za Ulinzi na Uwezeshaji za Wanawake za IRC nchini Nigeria, Lebanon na Uganda, na shirika la VOICE, yalifanyia Barometa majaribio na kushirikiana katika kuirekebisha na kuikamilisha.

Asante kwa kuchukua muda wako kusoma hati hii. Tafadhali wasiliana nasi ikiwa ungependa habari zaidi au kujadili utafiti au kipimo cha Barometa zaidi.

[Jina, shirika, maelezo]

[maelezo ya kiungo cha utafiti]

[Nakala pepe ya utafiti iliyoambatishwa kwenye laha hili]

## Msaada, usaidizi na kuripoti

Ikiwa unahitaji msaada au usaidizi wowote, au unataka kuripoti unyanyasaji wa kingono au aina zingine za UWAKI, unaweza kuwasiliana na wafuatao:

[Ongeza maelezo ya usaidizi na huduma zinazopatikana za unyanyasaji wa kingono au aina zingine za UWAKI katika muktadha wako; pamoja na maelekezo ya maelezo ya mashirika yenyewe].

# Fomu ya Utoaji Idhini ya Mshiriki katika kipimo cha Barometa cha Sikiliza!

[Mfano: Badilisha hati kabla ya kutumia katika vikao vya FGD]

Habari? Jina langu ni ________ na ninafanya kazi katika _______. Ninaandamana na mwenzangu _____ ambaye anafanya kazi katika [shirika lile lile/lingine] na atakuwa akituandikia kumbukumbu. Mwenzangu ___________ atakuwa akikalimani [ikiwa mkalimani atahitajika].

Tungependa kujadiliana nawe baadhi ya vipengele vya usaidizi wa kibinadamu ambao umepokea. Mjadala huu utajumuisha [wanawake/wasichana] wengine 5-6 kutoka katika jamii yako. Tutakuwa tukichora ramani pamoja ili kutusaidia kuelewa usaidizi unaopatikana katika jamii yako na masuala yaliyopo ya usalama kwa wanawake na wasichana. Tutatumia taarifa hizi ili kutusaidia kuyauliza mashirika kutoa usaidizi wa kibinadamu ulio salama zaidi, wenye usawa na ambao ni rahisi kwa wanawake na wasichana kuufikia. Tutakuwa tukifanya zoezi hili na makundi mengine ya wanawake na wasichana katika jamii.

Ukikubali kushiriki, utashiriki katika majadiliano ambayo yatadumu kwa muda usiozidi saa moja. Ikiwa hutaki kuendelea kushiriki kwa sababu yoyote, unaweza kuondoka wakati wowote. Kushiriki katika mjadala ni kwa hiari kabisa na si lazima ujibu maswali yoyote ambayo hutaki kujibu. Hatutakuuliza kwa nini hutaki kushiriki. Hakutakuwa na athari zozote mbaya ikiwa utachagua kutoshiriki au kujiondoa wakati wowote. Tutachukua tahadhari ili kuweka maelezo yoyote unayotoa wakati wa majadiliano siri. Huhitaji kutupatia majina yako au taarifa yoyote ya kibinafsi. Huhitaji kutuambia kuhusu hadithi zako mahususi. Majadiliano yatafanyika mahali ambapo ni faragha ili mtu yeyote asisikie tukizungumza kama kikundi. Mtu akitukaribia au akija mahali hapo, tutasimamisha mazungumzo hadi tuweze kuendelea faraghani. Hatutajumuisha taarifa nyingine yoyote ya utambulisho katika kitu chochote tutakachotoa kutokana na mazungumzo haya. Tutachukulia kwa heshima kila unachosema leo na tutashiriki tu majibu utakayotoa kama majibu ya jumla pamoja na yale yatakayotoka kwa watu wote watakaozungumza nasi. Tunakuomba uweke kila kitu siri pia, na kwamba ujiepushe na kutumia majina ya wenzako wakati wote wa mazungumzo, ili tudumishe usiri.

Je, kuna kitu chochote ambacho ungehitaji ili uwe salama na ushiriki bila wasiwasi? Je, kuna jambo lingine tunaloweza kufanya ili kukusaidia ujisikie bila wasiwasi? Je, una maswali yoyote ambayo ungependa kuuliza kabla hatujaendelea?

*Hakikisha kuwa maswali yote yamejibiwa kikamilifu na uangalie tena ili uhakikishe kuwa hakuna chochote kitakachoachwa bila kujibiwa.*

Kwa ruhusa yako, tutaandika kumbukumbu ili kuhakikisha kwamba hatukosi kile unachosema lakini hatutanakili taarifa yoyote inayoweza kukutambulisha. Je, unaturuhusu tuandike kumbukumbu za majadiliano yetu?

